# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## Kikao cha Nne – Tarehe 2 Februari, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**SPIKA:** Hati za Kuwasilisha Mezani, Waziri Mkuu, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ummy Nderiananga.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 45 la Tarehe 10 Novemba, 2023
2. Toleo Na. 46 la Tarehe 17 Novemba, 2023
3. Toleo Na. 47 la Tarehe 24 Novemba, 2023
4. Toleo Na. 48 la Tarehe 01 Disemba, 2023
5. Toleo Na. 49 la Tarehe 08 Disemba, 2023
6. Toleo Na. 50 la Tarehe 15 Disemba, 2023
7. Toleo Na. 51 la Tarehe 22 Disemba, 2023
8. Toleo Na. 52 la Tarehe 29 Disemba, 2023
9. Toleo Na. 01 la Tarehe 05 Januari, 2024
10. Toleo Na. 02 la Tarehe 12 Januari, 2024
11. Toleo Na. 03 la Tarehe 19 Januari, 2024; na
12. Toleo Na. 04 la Tarehe 26 Januari, 2024.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2023)*.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa niaba yake Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2023)*.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, lakini tutaanza na swali namba 49 badala ya 48 halafu tutarejea 48. Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Serikali kuvisaidia vikundi vya uzalishajimali – Tanga**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuvisaidia vikundi vya uzalishaji mali vikiwemo vya ufugaji ambavyo wanawake wamehamasika ili wafuge kwa tija?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Mkoa wa Tanga na maeneo mengine nchini, zimekuwa zikitoa mikopo ya uwezeshaji kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani. Mikopo hiyo imekuwa ikitumika kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji ikiwemo ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023, Halmashauri za Mkoa wa Tanga zilitoa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri yenye thamani ya shilingi bilioni 4.569 ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.827 zilikopeshwa kwa vikundi vya wanawake ambapo vikundi 102 vya wanawake vyenye wanufaika 875 vinavyojishughulisha na kazi za ufugaji vimekopeshwa kiasi cha shilingi milioni 575.39.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuviwezesha vikundi mbalimbali kwenye shughuli za uchumi na uzalishaji ikiwemo vikundi vya akina mama ili kutengeneza ajira, kipato na hivyo kupunguza umaskini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Swali la kwanza; kwa kuwa mchakato huu wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10 umesitishwa ni mrefu sasa, na kwa kuwa akina mama bado wanahangaika na mikopo ya kausha damu huko mitaani. Je, ni lini sasa Serikali itaanza tena zoezi hili la utoaji mikopo ili kuondoa adha kwa akina mama wa Mkoa wa Tanga na Watanzania kwa ujumla? *(Makofi)*

Swali la pili; kwa kuwa Halmashauri huwa zinatenga mikopo ya asilimia 10 kutoka kwenye mapato ya ndani kila robo ya mwaka, na kwa kuwa mchakato huu pia umesimama kwa muda mrefu. Je, Serikali inahakikisha Halmashauri zinaendelea kutenga fedha za asilimia 10 ili wakianza mchakato huu akina mama waweze kupatiwa mikopo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zodo. Swali lake la kwanza juu ya mchakato kusitishwa, ni kweli mchakato huu ulisitishwa baada ya Mheshimiwa Rais kupokea ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* na kuonesha kwamba kuna fedha nyingi ambazo zilikuwa hazijarejeshwa za mikopo hii, hivyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassah yalikuwa, yafanyike mapitio sasa ya namna ya mikopo hii inavyotolewa.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa aliunda timu, ambayo ilifanya mapitio ya namna ya mikopo inavyotolewa, timu ile ikawasilisha taarifa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na sasa mapendekezo yale yamewasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivi tunavyozungumza Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, amekumbushia kwa Mheshimiwa Rais ili jambo hili liweze kurudi sasa na kuanza utekelezaji wake. Kama kuna Sheria ya kubadilika iletwe mbele ya Bunge hapa ili sheria hizo ziweze kubadilika.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la fedha hizi je bado hutengwa. Ndiyo, fedha hizi bado zinatengwa kwa sababu, kwa mujibu wa Sheria ile ya Fedha ya Serikali za Mitaa, fedha hii iko *ring fenced* na inaendelea kutengwa. Pale mikopo hii itakapoanza kutolewa tena basi fedha hii ipo, nawatoa mashaka hayo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kitu pekee cha kuwatoa wanawake wa Tanzania waendelee haraka, ni mifugo midogomidogo ikiwemo kuku, mbuzi na ng'ombe. Wanawake wa Kilimanjaro wanasubiri sana msaada huo kutoka Serikalini.

Je, ni lini sasa ile mitamba niliyoahidiwa hapa Bungeni itatolewa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mitamba ni ya TAMISEMI au ni ya Uvuvi? Ni ya Mifugo na Uvuvi eeh?

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri. Kwa sababu ameiunganisha na mikopo kwa hiyo na swali linahusu mikopo, wote wawili hawapo? Mheshimiwa Shally Raymond, hakuna anayeweza kujibu swali lako kwa hiyo Waheshimiwa Mawaziri watakapokuja, tutawapa nafasi ili wakujibu swali lako. Kama hawakuja, litaenda kama swali la msingi.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, wakati tunasoma Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024, Wizara ya Mifugo ilitoa maelezo ya namna gani tunakwenda kuboresha sekta ya mifugo kwa ujumla. Kwa hiyo, kwa sababu Mheshimiwa Shally ameuliza swali hili ambalo ni *specific* kwenye eneo hilo la mitamba, tunaomba tulichukue na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo atapatiwa taarifa hii na atampatia majibu Mheshimiwa Shally Raymond. *(makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu yatatolewa kwa Mheshimiwa Shally bila kuwa swali la msingi kama nimekuelewa vizuri. Mtampelekea wenyewe majibu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo kwa sababu hapa limeletwa kama swali la nyongeza na siyo swali la msingi.

**SPIKA:** Ni sawa. Mimi naweza kuagiza mambo mawili, moja, ninyi mumpelekee ama lije kama swali la msingi. Kwa hiyo kwa maelezo yako kama nimekuelewa vizuri ni kwamba badala ya kuja kama swali la msingi, ninyi Serikali mtampelekea majibu Mheshimiwa Shally Raymond.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, tuko tayari kupata Mwongozo wa Kiti chako.

**SPIKA:** Sawa. Mpelekeeni majibu, kama hakuyapata atauliza tena.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana. Bado tuko Ofisi ya Rais TAMISEMI, sasa tunarejea kwenye swali namba 48. Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake.

Na. 48

**Kukamilisha ujenzi wa Wodi Vituo vya Afya Mwanhalanga na Negezi**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa wodi za wagonjwa, nyumba za Madaktari, maabara na *mortuary* katika Vituo vya Afya vya Mwanhalanga na Negezi utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilipeleka shilingi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wazazi lenye huduma za upasuaji wa dharura katika Kituo cha Afya Mwanhalanga na shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa majengo matano katika Kituo cha Afya Negezi, ambapo ujenzi umekamilika na majengo yanatumika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa miundombinu mbalimbali ikiwemo wodi za kulaza wagonjwa, nyumba za watumishi, maabara na majengo ya kuhifadhia maiti katika vituo vya afya Mwanhalanga na Negezi, katika Halmashauri ya Kishapu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuipongeza Serikali kwa majibu mazuri kuhusiana na miradi hii miwili Mwanhalanga na Ukenyenge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tu kushukuru kwamba shilingi milioni 500 kwa ajili ya Kituo cha Ukenyenge zilijenga yale majengo matano lakini upungufu bado ni mkubwa sana na hivyo kupelekea Kituo hiki kuendelea kubaki na kutokuwa na hadhi kama Kituo cha Afya. Tunahitaji majengo kwa ajili ya wodi za akina mama na akina baba lakini tunahitaji pia *walkways* kwa baadhi ya Wodi ambazo

zitakuwa zinaunganishwa na hizi njia za kuwafikisha Madaktari na wagonjwa maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kuhusiana na Kituo cha Afya cha Mwanhalanga. Kituo hiki cha afya kina majengo mawili tu na bado wagonjwa ni wengi sana. Ni lini Serikali itakwenda kujenga majengo maalum kwa ajili ya wodi za akina mama, wodi za akina baba, *mortuary* pamoja na nyumba za watumishi ili tuongeze ari ya watumishi kutenda kazi katika maeneo haya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Butondo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza napokea pongezi zake kwa Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo kwa kweli imefanyika katika Sekta ya Afya kwa ujenzi wa Vituo vya Afya kikiwemo hiki Kituo cha Afya cha Negezi ambacho kimepokea shilingi milioni 500. Ninamhakishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunatambua majengo haya bado hayatoshi, hayajakidhi mahitaji, bado tunahitaji wodi, bado tunahitaji *mortuary* na majengo mengine.

Mheshimiwa Spika, safari ni hatua Mheshimiwa Mbunge, Serikali inaendelea kutenga fedha kwenye bajeti, tuhakikishe kwamba fedha hizi zinapelekwa kwa ajili ya kukamilisha miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusiana na Kituo cha Afya cha Mwanhalanga, tunafahamu, tulishapeleka fedha lakini bado kuna majengo ambayo tumeshaweka mpango mkakati kwa ajili ya kutenga fedha ya ukamilishaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mgeta kimejengwa toka mwaka 2018 mpaka leo kimejengwa *mortuary* imekamilika hakina majokofu manne ya *mortuary*. Ni lini Serikali itapeleka majokofu manne ya *mortuary* pamoja na kwamba vituo hivyo vilipewa shilingi milioni 400 ya kujenga na milioni 300 ya vifaa vya tiba...

**SPIKA:** Umeshauliza swali Mheshimiwa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Mgeta kimejengwa, kimekamilika, kimeanza kutoa huduma lakini jengo la kuhifadhia maiti limekamilika, tayari Serikali imeshapeleka fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Halmashauri ya Bunda. Moja ya kazi ambayo itafanyika ni kununua jokofu kwa ajili ya kuhifadhia maiti katika kituo hiki cha Mgeta. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Magendo, Kibaha Vijijini tumepokea jokofu la kuhifadhia maiti lakini *mortuary* haijajengwa; je, lini tutapata pesa kwa ajili ujenzi?

**SPIKA:** Naibu Waziri Mheshimiwa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakamo kuwa Serikali ilishatoa maelekezo kwa Halmashauri zetu kote nchini, kwamba Mheshimiwa Rais anapopeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya, lakini anapopeleka fedha kwa ajili ya vifaatiba, kuna baadhi ya miundombinu ambayo iko ndani ya uwezo wa mapato ya ndani ya Halmashauri kama majengo ya *mortuary*.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumuelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kibaha, kutenga fedha kwenye mapato ya ndani kujenga jengo la *mortuary* ambalo ni jengo la gharama ya kawaida kabisa ili wananchi waendelee kupata huduma katika eneo hilo. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hili jokofu mmepelekaje wakati jengo halipo? Ama limetunzwa wapi sasa hilo jokofu? Mheshimiwa Mwakamo, hilo jokofu mmelitunza wapi? Stoo ama lipo kwenye wodi mahali? *(Kicheko)*

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa amesambaza vifaa, alipolifikisha basi lilitafutiwa utaratibu wa kuhifadhiwa ili tulitafutie namna ya kulipatia jengo la kuliweka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Susuni na Mwema zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, hazina kabisa Kituo cha Afya na hivyo kusababisha wananchi kutembea kuja kutafuta huduma Tarime Mjini. Nataka kujua ni lini Serikali itapandisha hadhi Zahanati ya Kiongera ambayo imekarabatiwa ili kuwa Kituo cha Afya na kuweza kurahisisha huduma kwa wananchi hawa?

**SPIKA:** Naibu Waziri Mheshimiwa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, ujenzi wa vituo vya afya katika Kata, tunajenga kimkakati, kwanza kwa kufanya tathmini ya vigezo kwa maana ya idadi ya watu, umbali kutoka kituo kingine, pia maeneo yale ambayo ni magumu kufikika. Kwa kuwa, Kata hii ya Susuni na Mwema hatujapata tathmini yake ya kutosha, naomba tuichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge tukafanye tathmini tuone kama inakidhi vigezo, tuziingize kwenye mpango mkakati, aidha kupandisha hadhi zahanati au kufanya ujenzi katika Kata hizo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 50

**Kukamilisha ujenzi wa Kituo Afya cha Migoli – Ismani**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamalizia ujenzi wa Kituo cha Afya cha Migoli katika Jimbo la Ismani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilipeleka shilingi milioni 400 katika Halmashauri ya Iringa kwa ajili ya ujenzi wa majengo matatu ya Kituo cha Afya Migoli. Ujenzi wa jengo

la wagonjwa wa nje umekamilika na linatoa huduma, majengo ya wodi ya wazazi na upasuaji yako asilimia 90 ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la wazazi na upasuaji, ujenzi wa vyoo, ujenzi wa kichomea taka na shimo la kutupia kondo la nyuma.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa miundombinu katika Kituo cha Afya cha Migoli.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na jengo la *OPD* kukamilika, jengo la wazazi pamoja na upasuaji bado hayajakamilika. Akina mama pamoja na wananchi wanapata adha kubwa kwenda katika hospitali ya wilaya ama kwenda Hospitali ya Rufaa ya Iringa Mjini: Je, lini Serikali itakamilisha majengo haya ili wananchi hao wapate huduma?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hadi sasa tumebakiza miezi mitano ili tukamilishe mwaka wa fedha na asilimia 100 aliyosema italetwa, bado haijaletwa: Ni lini sasa hiyo fedha asilimia 100 itapelekwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Victor Tendega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimejibu katika majibu yangu ya msingi kwamba ni kweli jengo la *OPD* limekamilika, jengo la wazazi na

upasuaji halijakamilika, na Serikali katika mwaka huu wa fedha imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia na vile vile nampongeza Mheshimiwa Lukuvi asubuhi ameniambia shilingi milioni 100 tayari imeshapokelewa katika halmashauri yake. Kwa hiyo, nawapongeza kwa ushirikiano huo mzuri wa kuwahudumia wananchi wa Wilaya ya Iringa.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na shilingi milioni 100, ndiyo hiyo ambayo tumeambiwa imeshafika. Kwa hiyo, tutafuatilia utekelezaji ili jengo likamilike mapema wananchi waanze kupata huduma, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali hii ya Awamu ya Sita inatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Katibu Mkuu Daniel Chongolo ambaye ni mstaafu, alivyopita Jimbo la Kalenga aliahidi kuleta shilingi milioni 500 kujenga Kituo cha Afya Kata ya Lyamgungwe ndani ya miezi mitatu: Je, Serikali itatekeleza lini agizo hili ambalo ni halali kabisa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Kiswaga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inatekeleza kwa ufanisi mkubwa sana Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na maeneo yote ambayo Serikali imeahidi kujenga vituo vya afya baada ya kujiridhisha na vigezo, tutakwenda kupeleka fedha kwa awamu kwa ajili ya kujenga vituo hivyo. Kwa hiyo, nimhakikishie

Mheshimiwa Kiswaga kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI, itakwenda kufanya tathmini eneo hilo kuona kama linakidhi vigezo na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi, nenda moja kwa moja kwenye swali bila hadithi. Mheshimiwa Enosy Swalle, swali la nyongeza

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kata ya Mtwango tumejenga kituo cha afya kwa mapato ya ndani, pia tumejenga jengo kwa ajili ya *mortuary,* lakini hatuna jokofu. Kwa kuwa nimemsikia Mheshimiwa Waziri kwamba Kibaha Vijijini kuna jokofu na hawana jengo la *mortuary;* je, Serikali iko tayari kuchukua hili jokofu kwenda pale Mtwango? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze wananchi wa Jimbo la Lupembe na Mheshimiwa Mbunge kwa kujenga Kituo cha Afya cha Mtwango kwa mapato ya ndani. Pia nimhakikishie tu kwamba tunafahamu kwamba kuna jengo la kuhifadhia maiti halina mashine kwa maana ya jokofu la *mortuary* na tayari Serikali hii imeshapeleka fedha zaidi bilioni 150 kwenye halmashauri zote kote nchini ndani ya miezi mitatu, minne iliyopita kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vya kipaumbele yakiwemo majokofu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatoa kipaumbele kupata jokofu katika Kituo cha Afya cha Mtwango, ahsante. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali lilikuwa, kuna jokofu mahali halina chumba, kwa hiyo, limehifadhiwa, halafu kuna mahali kuna chumba ambapo hakuna jokofu. Haliwezi kutolewa hili jokofu ambalo kwa sasa limehifadhiwa halihifadhi maiti likapelekwa kwenye chumba ambacho kipo tayari? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; jokofu hili lilipelekwa na Bohari ya Dawa kwa maana ya *MSD* na tulishapata taarifa na tayari taratibu za kulihamisha kupeleka sehemu ambayo tayari jengo limekamilika zinaendelea. Baada ya Kibaha kukamilisha jengo watapelekewa tena jokofu lao. Kwa hiyo, naomba nisilete *commitment* kwamba tunapeleka Lupembe, lakini tunapeleka sehemu ambayo tayari *MSD* wameshafanya tathmini na wameona uhitaji kwa sasa ili lisikae bila kufanya kazi, ahsante.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Sillo, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali ilipeleka shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Gidas: Je, ni lini itamalizia awamu ya pili ya shilingi milioni 250 ili kukamilisha majengo yale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Sillo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kweli Serikali ilishapeleka shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Gidas na inahitaji shilingi milioni 250 ya awamu ya pili kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo yaliyobaki katika hicho kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote ambao walipata fedha za awamu ya kwanza ya shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, kwamba Serikali imeshaweka mkakati katika mwaka ujao wa fedha kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo kwa awamu ya pili. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuja Chiungutwa alitoa ahadi ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya kumalizia Kituo cha Afya cha Chiungutwa na pia shilingi milioni 100 pia kwa Kituo cha Afya cha…

**SPIKA:** Mheshimiwa swali la nyongeza huwa ni moja.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, lini…

**SPIKA:** Subiri, subiri. Kwanza huwezi kwenda mbili; pili, kwa sababu ni swali la nyongeza huwezi kuweka maswali mawili katika swali moja. Chagua kimojawapo kati ya hivyo umwulize Mheshimiwa Naibu Waziri ili akujibu.

**MHE. ISSA ALLY MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ni lini pesa hizi shilingi milioni 100 zitakwenda kwenye Kituo cha Afya cha Chiungutwa?

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Mchungahela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Makamu wa Rais aliahidi shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukamilishaji wa Kituo cha Afya

cha Chiungutwa na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hiyo imeshatengwa kwenye bajeti ya mwaka huu 2023/2024 na fedha zitakapopatikana zitapelekwa katika kituo hiki kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pale kwenye kituo chetu cha Bweri pamoja na Makoko ni vituo ambavyo sasa vimekaa muda mrefu pasipo kumaliziwa; je, ni lini Serikali italeta fedha ili tuweze kumalizia hivyo vituo wananchi waweze kupata huduma bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Bweri na Makoko ambavyo havijakamilika, kwanza utaratibu ambao tumeweka Serikalini ni kwamba vituo vyote ambavyo havijakamilika tunafanya tathmini ya kujua havijakamilika kwa sababu gani; je, ni matumizi mabaya ya fedha? Kama ni matumizi mabaya ya fedha tunachukua hatua kwa watumishi waliohusika.

Mheshimiwa Spika, pili, kama ni inatokana na *inflation,* tumeelekeza halmashauri kutenga fedha kwa awamu, badala ya kusubiri fedha za Serikali kuu pekee kwenda kukamilisha majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitumie fursa hii kwanza nichukue hoja hii kwamba tutafanya tathmini kujiridhisha, na pili, nimwelekeze

Mkurugenzi wa Halmashauri hii ya Manispaa ya Musoma kuhakikisha wanaanza kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu iliyobaki ili vituo vianze kutoa huduma kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali, swali la nyongeza.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Serikali ilituahidi kutupatia fedha kwa ajili ya kujenga Kituo chetu cha Afya cha Choma; je, ni lini fedha hizo zitafika kwenye Kituo cha Afya cha Choma? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gulamali, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilishaahidi kupeleka fedha shilingi milioni 500 kwenye Kituo cha Afya cha Choma na tayari nimeshawasiliana na Mheshimiwa Mbunge mara kadhaa kwamba imeshaingizwa kwenye orodha ya fedha za Benki ya Dunia ambazo tunatarajia wakati wowote mwezi wa Pili au wa Tatu zitatoka kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi hiyo imezingatiwa na Serikali itatekeleza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 51

**Ujenzi wa Soko la Kisasa Holili Wilayani Rombo**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la kisasa Holili Wilayani Rombo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na Soko la kisasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo eneo la Holili. Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023 ilitenga na kutoa shilingi milioni 75 fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa vyoo na kumwaga jamvi eneo la kuuzia mazao.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kujenga na kuendeleza miundombinu inayohitajika ili kuwezesha soko hilo kuwa la kisasa na kukidhi mahitaji, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa ujenzi wa soko hili ulitokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan wakati huo akiwa ni Makamu wa Rais; na kwa kuwa Waziri Mkuu alipokuja kwenye ziara wananchi wa Rombo walikumbushia ahadi yao: Je, nini kauli ya Serikali kuhusu ujenzi wa soko hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, shilingi milioni 75 ni fedha ndogo sana katika ujenzi huu. Je, Serikali kwa nini isiweke ujenzi wa soko hili katika miradi ya kimkakati ili kutimiza ahadi ya viongozi hawa wawili? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba ahadi za viongozi wetu wa kitaifa ni kipaumbele katika utekelezaji ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa kuwa ni kweli fedha ambayo imetengwa ni kidogo, nitumie fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rombo kufanya tathmini ya kina na upembuzi yakinifu wa gharama zinazohitajika, kwa ajili ya ujenzi wa soko hili na kuziwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kuona kama fedha itatoka *Central* Government au wanaweza kugharamia kwa mapato ya ndani, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa hii nafasi. Halmashauri ya Meru iliwasilisha michoro ya soko la kisasa TAMISEMI mwaka jana mwezi Novemba, kwa maana ya mwaka 2023; soko hili linategemewa kujengwa Eneo la Madira; je, ni lini ujenzi wa soko hili utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pallangyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na utaratibu wa kuwasilisha miradi ya kimkakati lakini tunafanya tathmini na upembuzi kuona kama fedha kwanza ya Serikali ipo, na pia kama halmashauri zenyewe zinaweza zikagharamia kupitia mapato ya ndani. Kwa hiyo, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anatoa taarifa kwamba limeshawasilishwa Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba tulichukue suala, tutalifanyia kazi tufuatilie, andiko liko wapi, limefikia hatua gani, ili tuweze kuona namna gani tunafanya ili kwenda kujenga soka la kisasa katika eneo hili la Madira, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana.

Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Mchango wa Mji wa Tunduma katika uchumi wa nchi**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, Serikali ina Mkakati gani wa kufanya utafiti maalum katika Mji wa Tunduma ili kubaini ni namna gani unaweza kuchangia kukuza uchumi wa nchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Mipango, hususan kifungu cha 6, pamoja na majukumu mengine, Tume ya Mipango ina jukumu la kufanya utafiti kuhusu suala lolote ambalo Tume inaona ni muhimu katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia hili, Tume ya Mipango imejipanga kufanya tafiti mbalimbali na kuratibu tafiti zitakazofanywa na taasisi nyingine za umma na binafsi kwa lengo la kubaini fursa za maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Serikali, kupitia Tume ya Mipango, itafanya tafiti mbalimbali kubaini fursa za maendeleo katika miji ikiwemo Mji wa Tunduma kwa lengo kubaini ni jinsi gani mji huu na miji mingine nchini inaweza kuongeza kasi ya maendeleo na kuchangia kukuza uchumi wa nchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, kulingana na majibu ambayo yametolewa na Waziri, nataka kufahamu, ni upi mkakati maalum na wa haraka wa Serikali kuuingiza Mkoa wa Songwe kiujumla wake katika mpango wa uwekezaji wa kimkakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nataka kufahamu: Je, Serikali imeshafanya vitu gani katika kuongeza biashara na uwekezaji katika Mkoa wa Songwe katika maeneo yafuatayo: eneo la madini, dhahabu na makaa ya mawe, kilimo cha mpunga, uvunaji wa chumvi na mazao mengine ya kibiashara yanayoendelea katika Mkoa wa Songwe? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, maswali ya nyongeza yanahusu fursa za uwekezaji katika Mkoa wa Songwe na ametaja maeneo *specific;* madini, chumvi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninahitaji kumwandalia taarifa hizi kwa kina ili nisije nikatoa majibu ambayo ni ya kurukaruka. Kwa hiyo, naomba tupate nafasi kwa sababu kwa kweli ni swali ambalo ni jipya kidogo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Ilemela katika kuunga mkono uwekezaji ilitenga eneo la ekari 52 katika eneo la Nyamungoro, eneo lenye miundombinu yote; maji, barabara na liko kwenye *main road* ya kwenda Musoma kwa ajili ya kuweka *industrial park* na tayari andiko lilishafika katika Ofisi za Serikali; ni lini mradi huu utatekelezwa ili tuongeze ajira na kukuza TEHAMA kwa watu wa Mwanza na ukizingatia ni ukanda wa maziwa makuu ni *hub* katika eneo hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ah, sasa leo haya maswali sijaelewa. Hilo ni la kwako au ni la viwanda? Maana nasikia *industrial park* hapa, ama ni la kwako? Mheshimiwa Waziri, kama siyo lako tutaikabidhi Wizara, kama ni la kwako tusaidie majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, maendeleo ya *Industrial Park* tunafanya pamoja na Wizara ya Viwanda, ipo chini ya *EPZA*. Nalifahamu hili eneo na nilishafika na tayari lipo katika Taasisi yetu ya *EPZA* wakilifanyia kazi, linaenda kwenye bodi na baada ya hapo tutalitolea maelekezo maalum kwamba ni lini hasa ratiba itatoka ya utekelezaji. Naamini katika mpango na bajeti ambao tutawasilisha kwenye Mkutano ujao, tutaeleza mpango maalum kuhusu *Industrial Park* ya Manispaa ambayo Mheshimiwa Angeline Mabula ameieleza.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, sasa aulize swali lake.

Na. 53

**Changamoto ya Maji Jimbo la Momba**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya maji katika vijiji 42 vya Jimbo la Momba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Momba lina jumla ya Vijiji 72 ambapo mpaka sasa vijiji 30 vinapata huduma ya Majisafi na Salama kupitia miradi ya maji ya bomba. Katika kuhakikisha vijiji vyote vinapata huduma ya maji, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya Maji katika vijiji 12 vya Muungano, Ipata, Ntinga, Chindi, Makamba, Naming'ongo, Yala, Isanga, Kalungu, Lwatwe, Samag'ombe na Kakozi kwa gharama ya shilingi bilioni 9.45. Utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeanza kazi ya utafiti wa maji chini ardhini na uchimbaji wa visima virefu katika vijiji 16 vya Mkutano, Nzoka, Chilangwi, Itumba, Miunga, Mfuto, Machimbo, Mpwinje, Njeleke, Isunda, Chafuna, Msungwe, Sante, Siliwiti, Chole na Mtungwa ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024

kwa shilingi milioni mia sita. Kukamilika kwa uchimbaji wa visima hivyo kutawezesha usanifu wa miundombinu ya usambazaji, kufanyika katika mwaka wa fedha 2024/2025 na utekelezaji wake kuanza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa masikitiko makubwa ndani ya Bunge lako Tukufu naomba niseme kwamba Mama yetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ana kauli yake ya kumtua ndoo mwanamke kichwani, lakini Wizara ya Maji ndani ya Jimbo la Momba mmeipinga kauli hii kwa vitendo, imeikataa kabisa hiyo kauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hapa nimekuja na *clip* kwenye simu yangu naomba uletewe hapo mbele wewe kama Spika wetu ili angalau wewe uweze kuangalia uone. Kama maji haya ambayo wana-Momba wanatumia, binadamu wa kawaida wanafaa kutumia kutumia haya maji. Mwezi wa sita ulinipa nafasi ya kusimama hapa kuomba mwongozo kwa Wizara ya Maji ili wanichimbie visima vya dharura, mpaka leo hivyo visima pamoja na watoto kuteseka hakuna hata tone la maji.

Mheshimiwa Spika, mradi ambao Wizara ya Maji wanasema huu wa bilioni 9.5 mwaka jana mwezi ya nne waliniondoa hapa Bungeni kwenda kukabidhi mradi kwa mkandarasi na tukaitwa mkutano mkubwa kwa wananchi na wakaahidi kwamba, kufikia mwaka huu mwezi wa sita mradi wa maji utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, leo tunavyoongea wiki moja iliyopita ndiyo wametupatia milioni mia tano kati ya bilioni 9.5 na leo mbele ya Bunge lako tukufu Wizara ya Maji wanasema kwamba mradi huu utakamilika Desemba. Mimi nikienda kwa wananchi ndiyo naonekana tapeli. Sasa kati ya mimi na Wizara ya Maji wakina nani ni waongo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hii *clip* uiangalie kwa niaba ya Bunge ili uone hii *clip* wewe uwe shahidi ikikupendeza ili uoneshwe hapa ili Mheshimiwa Rais aone kama Watanzania tulio mchagua, mimi Mbunge wa kike mtoto wake, wanawake wameniamini wanaweza wakatumia maji haya. Mimi naomba hii *clip* uone na Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa aione hii *clip*…

**SPIKA:** Mheshimiwa haya umeeleweka, umeeleweka Mheshimiwa. Haya msaidizi kaniletee *clip,* Mheshimiwa Naibu Waziri una maelezo gani kuhusu jambo hili? Mheshimiwa Naibu Waziri, Waziri amesimama. Mheshimiwa Waziri wa Maji. *(Makofi)*

*(Hapa Spika alikabidhiwa simu iliyokuwa na clip yenye kuonesha akinamama wa Momba wakichota maji)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa nafasi hii lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna anavyojibu maswali yake vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kubwa Bunge lililopita tulipata *concern* ya Mheshimiwa Mbunge, Dada yangu Condester na mimi kama Waziri wa Maji nilifika Jimboni kwake na tukafika maeneo mbalimbali kuona hali ipo miradi ambayo inaendelea lakini kwa udharula nilitoa kiasi cha shilingi bilioni moja kuhakikisha kwamba tuna-*support* miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine tunaweza tukawakatisha tamaa watendaji wanaofanya kazi kubwa. Lakini kazi inafanyika na sisi kama Wizara ya Maji na ipo miradi ya kimkakati kuhakikisha kwamba tunalisaidia Jimbo la Momba.

Mheshimiwa Spika, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo kwa Wananchi wa Momba kupata Huduma ya Maji Safi na Salama

katika kuhakikisha kwamba tunamtua mwanamama ndoo kichwani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa hapa hizo *clip* na nafikiri, hebu msaidizi njoo mfikishie Mheshimiwa Waziri pale ili apate hii picha.

*(Hapa Waziri wa Maji alikabidhiwa simu iliyokuwa na clip yenye kuonesha akinamama wa Momba wakichota maji)*

**SPIKA:** Lakini hoja ya Momba Waheshimiwa nadhani mtakumbuka kuna kipindi zilitajwa takwimu hapa ndani kuhusu maji, akasimama Mbunge wa Momba kuelezea kwamba hizi takwimu kwake yeye hazina uhalisia. Akasimama tena kama alivyosema kwenye Bunge nadhani ni Bunge la Bajeti ama lipi? Alisimama tena akaeleza maelezo yakatoka kwamba vikachimbwe visima kwa sababu magari yameishanunuliwa na Mheshimiwa Rais, vikachimbwe visima vya dharura yakatoka majibu hapa.

Mheshimiwa Waziri, anasema alishatoa bilioni moja maana yake hii milioni mia tano ni ya kuongezea kwenye ile bilioni moja ili utekelezaji uendelee. Lakini hali ya hawa wananchi nimekuletea hizo *clip* hapo siyo hali inayokubalika kwenye hivyo visima wanavyochota maji na kwa hiyo hali iliyoko hapo maana yake kwenye ardhi hiyo yapo maji. Kwa sababu hawa wanawake wametumbukia kwenye hicho kisima maana yake ikienda gari ikachimba hicho kisima hata kama ni kimoja, viwili, vitatu kwa wakati miradi mikubwa ikiendelea wachimbiwe hivyo visima nadhani nimekuletea hiyo *clip* umeishaipata au umeishaipata *clip*?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, sisi haya ni maelekezo na tunayapokea na kama ana ufahamu Mheshimiwa Mbunge, mimi nilifika na tukatembea maeneo mengi na tukaweka mkakati. Kikubwa hayo ni maelezo jukumu letu ni kwenda kuyatekeleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, sasa kwa sababu kipindi hiki ni cha mvua lazima pia tuwe na uhalisia. Mheshimiwa Condester haya maji yanachotwa kipindi hiki au ni kipindi cha kiangazi? Ili na mimi nitoe maelekezo ambayo yanaeleweka hapa mbele, haya ni ya kipindi hiki cha mvua ama kipindi cha kiangazi? Hizi *clip* ni za sasa hivi au za kipindi cha kiangazi?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, hizo *clip* nimechukua mwaka jana Mwezi wa Kumi na Mbili. Kwa hiyo, kipindi cha mvua watu ambao hawana mabati…

**SPIKA:** Hamuoni sasa hii yaani ni kipindi hiki?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, wakati mvua zimeishaanza.

**SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Waziri ameishapokea hayo maelekezo kwa sababu magari yapo kila Mkoa, gari lililoenda Songwe ama Mkoa wa jirani liazimwe lipelekwe likawachimbie kisima hawa wamama nadhani umeona hiyo hali iliyoko hapo. Kwa hiyo, nadhani hilo linaweza kufanyika ndani ya muda mfupi. Kwa sababu tayari hapo pana maji yale mambo ya usanifu, yakinifu, upembuzi, sijui nini hapo maji yapo na kwa sababu tayari wanayatumia hayo kawachimbieni hayo hayo wakati mnaendelea na utafiti wenu ili wananchi wa Momba waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi niulize ni lini Vijiji vya Mdundwalo, Maposeni, Malamala na Kimbango Nyasa vitapatiwa hivyo visima vya maji? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ntara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Dkt. Ntara tayari usanifu unafanyika, gari la kuchimba visima liko kule tumeishachimba kisima kikatoka maji machache sana kiasi kwamba hayawezi hata kupanda kwenye kichotea maji hata kimoja. Niwapongeze sana *Regional Manager (RM)* Ruvuma niliwaagiza, kwa sababu Dkt. Ntara hili swali ameishaniuliza mara nyingi tukiwa kwenye kiti. Tumeishafanyia kazi na wananchi wametoa ushirikiano kuna mto unaitwa Mpulanginga, huu mto umeonekana una maji ya kutosha kwa maeneo ya Mdundwalo na Maposeni. Lakini vilevile maeneo haya mengine ya Nyasa vilevile baada ya gari kumaliza hapa tunarajia liende huko likaweze kuchimba visima ili wananchi wapate maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nirejee tena maswali mafupi moja kwa moja kwenye swali halafu zile shukurani za kwangu nimeishazipokea na majina nikishawataja Wabunge ili tukomboe wakati wasitajwe mara ya pili upande wako Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Suma Ikenda, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Wilayani Rungwe kuna tatizo kubwa la maji hasa Kata ya Bulyaga, Makandana, Bagamoyo, Kawatere, Msasani na Ibigi. Sasa je, ni lini ujenzi wa tenki ambalo linatakiwa kuhudumu Kata hizo utakamilika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suma Ikenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Suma Fyandomo kwa kufuatilia Mradi wa Maji Tukuyu lakini ushirikiano mkubwa sana wa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo, Mheshimiwa Mwantona amefuatilia pia kwa karibu Mradi wa Maji Tukuyu Mjini na hili tenki ujenzi unaendelea na fedha milioni mia tano tunarajia kupeleka tena mgao wa mwezi huu. Kwa hiyo, nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge na mradi huu unakwenda kukamilika na wananchi wa Tukuyu wanaenda kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize swali swali la nyongeza. Ningependa kufahamu Serikali mnamkakati gani wa ziada kumaliza changamoto kwenye zile Kata tano za Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa ziadi kuhakikisha zile Kata tano zinapata maji ni kwenda kupeleka miradi ya muda mfupi ya uchimbaji wa visima ili wananchi waendelee kupata maji wakati utaratibu wa kutumia Ziwa Tanganyika unaendelea kufanyiwa kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Je, ni lini sasa Serikali itatatua changamoto ya maji ambayo ipo kwa muda mrefu katika Kata ya Lipwidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia lini Kata hii aliyoitaja tunapeleka maji? Mheshimiwa Shamsia kwanza nikupongeze kwa sababu umeishafuatilia sana lakini jitihada zinazoendelea pale Jimboni umeziona viongozi wetu wa Mkoa wa Mtwara wanaendelea kufanyia kazi na Kata hii inakwenda kupatiwa huduma ya maji safi na salama muda siyo mrefu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Halmashauri ya Itigi haijachimbiwa visima katika bajeti mbili zilizopita na gari la Mkoa wa Singida limekuwa likienda huku huku mara Msomera mara wapi? Sasa lini Serikali itakwenda kuchimba visima katika Halmashauri ya Itigi, katika Jimbo langu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahaya Massare, Mbunge wa Itigi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili eneo ambalo linatakiwa likachimbwe visima lipo kwenye mpango na kwa sababu gari lipo pale Mkoani tunarajia likimaliza upande umoja liliopo litakwenda katika maeneo haya na maeneo yote ambayo yanatakiwa kuchimbwa visima, visima vitachimbwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 54

**Kukamilika Mradi wa Maji wa Igongwi - Njombe**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Igongwi utakamilika katika Tarafa ya Igominyi Wilayani Njombe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji nijibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na Utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Igongwi katika Halmashauri ya Mji wa Njombe unaolenga kutatua tatizo la maji kwa wakazi 9,717 waishio katika Vijiji vya Kitulila, Madobole, Luponde na Njoomlole. Hadi sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia 78.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mradi huo imekamilisha ujenzi wa vyanzo vinne vya maji, uchimbaji wa mtaro na ulazaji wa bomba kuu kilometa 49.7, ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilometa 26 kati ya 35, ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 32 kati ya 55, ujenzi wa matenki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita 100,000 kati ya matenki manne pamoja na ujenzi wa miundombinu sita ya mfano ya kuvuna maji ya mvua iliyojengwa katika Shule za Msingi Madobole na Kitulila, Ofisi ya Serikali ya Kijiji Madobole na Zahanati ya Kijiji cha Kitulila. Kazi zote zilizosalia zinatarajiwa kukamilika kabla au ifikapo mwezi Juni, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Sisi watu wa Mkoa wa Njombe tunatambua kazi kubwa iliyofanywa na Serikali katika Mradi huu wa Maji wa Igongwi. Lakini vilevile tunatambua sababu mojawapo ya kusababisha mradi huu wa Igongwi kutokuendelea ni kutokana na kutopeleka fedha kwenye Mradi wa Maji wa Ruvuyo Wilaya ya Ludewa ambako ndiyo chanzo cha maji kinatokea. Je, lini Serikali itapeleka pesa kwenye Mradi wa Ruvuyo ili kuweza kuruhusu mradi huo wa Igongwi uendelee?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pil; Kuna baadhi ya Vijiji ambavyo viko ndani ya Jimbo la Njombe Mjini kikiwepo Kijiji cha Ihanga havikuwekwa kwenye mradi wa maji vijijini kimakosa. Je, lini Serikali itaweka vijiji hivi ambavyo viko kwenye Jimbo la Njombe Mjini havikuhesabika kama viko vijijini kuwekwa kwenye Mradi wa Maji Vijijini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze kwa ufuatiliaji. Mheshimiwa Neema hili umeishawahi kuniuliza mara kadhaa na nimeishalifanyia kazi kulingana na ufuatiliaji wako. Ili huu mradi upate kuendelea ni kweli fedha hapa katikati zilisimama lakini tumshukuru sana Mheshimiwa Rais tayari fedha Januari hii tumeanza kupokea ndani ya Wizara. Kwa hiyo, ni moja ya maeneo ambayo tutakwenda kupeleka fedha kwa awamu ili kazi ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, Eneo la Njombe mjini hivi vijiji ambavyo havikuhesabika katika miradi ya vijijini, ilifanyika hivyo kwa sababu ya jiografia yake. Lakini kwa ushirikiano wako wewe pamoja na Mbunge wa Jimbo wote mmeweza kufikisha suala na Viongozi wa

Mkoa wa Njombe wameishapewa maelekezo kuona kwamba vijiji hivi navyo vinapelekewa huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mliohamia kwenye viti vya Mawaziri nilitoa maelezo hapa mbele. Subirini kipindi cha maswali na majibu kiishe kelele zinakuwa nyingi sana.

Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mradi wa Maji Awamu ya Pili wa Jimbo la Bukoba Mjini unaohudumia Kata tano; Kata ya Buhembe, Nyanga, Kashai, Kahororo na Nshambya umekwama tokea mwaka jana japokuwa mkandarasi yuko *site*.

Je, Serikali ipo tayari kupeleka fedha kiasi cha shilingi milioni 253 kwa dharula ili wananchi wa kata hizi tano waweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Lugangira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi unaendelea kutekelezwa ndiyo maana umeweza kusema yule Mkandarasi yuko pale lakini suala la kupeleka fedha milioni 253 ni jukumu la Wizara nikuhakikishie Mheshimiwa Neema hizi fedha zitapelekwa ili kazi ziweze kuendelea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi, sasa aulize swali lake.

Na. 55

**Changamoto ya mawasiliano ya simu Micheweni**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya mawasiliano ya simu Micheweni, vijiji vya Sizini, Dodeani, Michungani, Mapofu, Msuka na Makangale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolijia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Jimbo la Wingwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Sizini kipo katika mradi wa awamu ya sita ambapo mnara katika kijiji hicho unajengwa na mtoa huduma ambaye ni Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)*. Mnara huo upo katika hatua mbalimbali za ujenzi, ambapo utakamilika na kuwashwa ifikapo Aprili, 2024. Aidha, Serikali imetekeleza ujenzi wa mnara katika kijiji cha Dodeani kupitia mradi wa awamu ya nne ya *UCSAF* ambapo mnara ulijengwa katika Shule ya Dodeani.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Serikali itavifanyia tathmini vijiji vya Michungani, Mapofu, Msuka na Makangale kuangalia mahitaji halisi ili kuvifikishia huduma ya mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye majibu Serikali imesema itavifanyia tathimini vijiji vilivyobakia je ni lini tathimini hii itaanza?

Mheshimiwa Spika, vilevile asilimia kubwa ya wananchi wa Wilaya ya Micheweni hutumia mitandao ya simu ya halotel na tigo lakini huduma zake zimekuwa ni hafifu mitandao hii. Je, Serikali inachukua jitihada gani kuwaondolea usumbufu wananchi wa maeneo ya vijiji hivi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipengele cha kwanza ni lini tutafanya tathimini? Tayari tumeishamaliza kufanya tathimini katika vijiji 2,116 na hivyo naelekeza timu ya wataalam kutoka Wizarani kwetu wakishirikiana na *UCSAF* waende wakafanye tathimini mara moja katika kata ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziomba.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha pili ni cha kiufundi na kibiashara, pia ni cha kisheria, kwa sababu kinaangukia katika upande wa sheria kwa mujibu wa Sheria Namba 12 ya Mwaka 2003, na kwa kanuni zetu za mwaka 2018 inampatia *TCRA* mamlaka ya kuhakikisha kwamba inaangalia ubora wa huduma ya mawasiliano. Hivyo, basi nitumie fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri kuwaelekeza *TCRA* kwenda kufanya tathmini na kujiridhisha na *quality of service* katika maeneo hayo ili tujue ni hatua gani

tunazichukua kulingana na majibu ambayo watayaleta, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la mawasiliano katika Wilaya ya Ukerewe, Kata ya Bukiko ambayo inatumia Mnara wa *Halotel 2G* na mawasiliano ni ya kusua sua sana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Furaha, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kupandisha hadhi minara ambayo inatoa huduma ya *2G* kwenda kwenye *3G* mpaka *4G*. Tayari Serikali kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali tumepandisha hadhi minara 304. Hivyo tunaamini kwamba itakapokamilika tutaangalia baadhi ya meaeneo ambayo bado yana uhitaji huo. Kwa Kata ya Lukiko ambayo ipo katika Jimbo la Ukerewe tumeiingiza kwenye utekelezaji kwa kuhakikisha kwamba tunakwenda kupeleka mnara pale, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, katika jibu lake kwa Mbunge wa Wingwi, ameeleza kwamba atapeleka wataalamu katika maeneo ambayo ameyataja.

Je, wataalamu hao watafika katika Kijiji cha Mkia wa Ng'ombe ambao upo katika Jimbo la Konde, ambako pia tatizo ni sawa na la huko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hili ni ombi, na Serikali ya Chama cha Mapinduzi dhamira yake ni kuhakikisha kwamba inawahudumia Watanzania katika maeneo mbalimbali. Hivyo Wizara tunapokea ombi hilo na tutahakikisha kwamba, wataalamu wetu wanafika katika eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwenye Kata ya Kilindi Asilia na Kata ya Luhande kwenye Vijiji vya Misufini kuna changamoto kubwa ya minara, kwa maana ya mawasiliano yanakatika mara kwa mara.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, uko tayari kutuma timu yako kuangalia namna ambavyo mawasiliano yanavyopatikana muda wote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Kigua, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tuko tayari kama Wizara kutuma wataalamu wetu kwenda kufanya tathmini ili tujiridhishe na uhalisia wa tatizo na kuchukua hatua stahiki, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, tarehe 9 Januari nilituma *message* kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na kwa Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* kuhusu minara 12 ya 2G katika Jimbo la Sikonge na wote mlijibu kwamba tumepokea.

Je, sasa ni lini itapandishwa hadhi ili kuwasaidia watu wa Sikonge upande wa *internet*?

**SPIKA:** Sasa hizo *message* tutajuaje sisi kama umetuma, maana ni suala la ushahidi, uliza tu swali lako Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nilishawasilisha tayari taarifa ya minara 12. Sasa ni lini…

**SPIKA:** Bunge halitakuwa na ushahidi wa hayo mawasiliano yenu. Kwa hiyo uliza swali unalotaka ujibiwe na Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, swali ni lini minara 12 ya 2G katika Jimbo la Sikonge itapandishwa hadhi? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, binafsi naomba nikiri kwamba Mheshimiwa Kakunda anaendelea kuwasiliana na mimi katika changamoto hiyo. Tayari, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri timu yetu inaendelea kufanya tathmini na kujiridhisha namna gani tutaweza kwenda kuanza hatua kwa hatua. Hatuwezi kupandisha yote kwa pamoja

kwa sababu miradi hii ina *budget implication* na inategemea na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Kakunda taarifa yake hiyo tunaendelea kuifanyia kazi na wananchi wake watapata huduma hiyo ya *internet*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuuliza Serikali ni lini itakuja kukamilisha mawasiliano katika Kata ya Gwata, ukizingatia ipo barabarani karibu Morogoro, kwaheri Morogoro na bado watu hawapatikani? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamisi Taletale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika minara 758 bahati mbaya Kata hii hatukuiingiza, na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kutafuta fedha na kuna minara takribani 636 ambapo katika hiyo, minara 15 inaenda kwenye upande wa *TBC*.

Mheshimiwa Spika, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Kata yake tutaiingiza kwenye minara hiyo 636, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, sasa aulize swali lake.

Na. 56

**Kauli ya Serikali kuhusu Bima za Afya kwa Watoto**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza: -

Je, nini kauli ya Serikali juu ya Bima za Afya kwa watoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali kuhusu Bima ya Afya kwa Watoto ni kuwaomba Watanzania wote, viongozi wote, kisiasa, kidini na kimila kuwa suluhu pekee ni sisi wote kuungana na Serikali katika kuhamasisha umma kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote pale utekelezaji utakapoanza, naomba kuwasilisha.

**SPIKA**: Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza; tunafahamu kwamba Taifa hili miaka yote limekuwa na haja ya kuhakikisha tunajenga taifa bora la kesho. Katika kujenga taifa bora la kesho maana yake ni kwamba watoto wetu wawe na afya bora kutokana na uwepo wa mfumo mzuri.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na mfumo ambao utasaidiawa wetu kuendelea kutunzwa afya zao badala ya kukaa

na kusubiri mpaka Bima ya Afya kwa Wote iweze ikaanza kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kwa kutokuwa na mfumo sahihi kwa ajili ya watoto na afya zao.

Je, hatuoni kwamba tunafifisha, tunapunguza hali ya taifa hili kujenga vizuri watoto wetu kwa minajiri wa kuwa *citizen* bora wa taifa la kesho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna mifumo. Kuna mifumo tena mizuri, ndiyo maana jana umemuona Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekwenda pale Benjamin Mkapa na umeona watoto ambao ni masikini kabisa, wasingeweza kulipa zaidi ya milioni 50 ambazo zilihitajika kwa ajili ya kutibu *sickle cell* wametibiwa bure na wamepona. Mpaka mwaka huu, watoto zaidi ya 20 Mheshimiwa Rais wetu ametoa fedha na watarudi kwenye familia zao.

Mheshimiwa Spika, kwenye nchi hii kuna watoto milioni 31. Milioni 1.5 wako kwenye mfumo wa bima wa sasa, milioni 30.7 wako kwenye mifumo mingine, kwa maana wanatibiwa kwenye mifumo mingine iliyoko kwenye nchi yetu. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba kuna mifumo haikosi changamoto lakini hizo changamoto mimi na wewe tunavyoendelea kukabiliana nazo, kwa sababu zinatokea kila wakati. Tukikubaliana wote kwa pamoja twende kwenye *issue* ya Bima ya Afya kwa Wote, na hizi changamoto ndogo ndogo tunazokutana nazo leo, tutakwenda kutatua kwa pamoja Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti maalum, Sasa aulize swali lake.

Na. 57

**Kuweka ruzuku kwenye nishati ya gesi**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka ruzuku kwenye nishati ya gesi ili wananchi waweze kumudu kununua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 inaielekeza Serikali kuchukua hatua madhubuti za kufanikisha matumizi ya nishati safi na vifaa sahihi vya kupikia. Kwa sasa Serikali inakamilisha kuandaa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa lengo la kuhakikisha asilimi 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo Mwaka 2033. Hivyo, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kutatua vikwazo vinavyokwamisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kupunguza gharama za upatikanaji wa nishati safi, vifaa na majiko sanifu ya kupikia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali moja dogo lenye sehemu (a), (b), (c), (d) kama ifuatavyo: -

**SPIKA:** Mheshimiwa ni (a) na (b) pekee. Kwa hiyo, katika hayo manne chagua mawili.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongea na wadau ili waweze kuondoa gharama kubwa iliyopo ya ununuzi wa mtungi wa gesi na gesi yenyewe, wakati mchakato wa kupunguza au kuweka ruzuku kwenye nishati ya gesi unaendelea kwa Serikali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Shule ya Ufundi *Mtwara Tech*. imefunga mfumo wa gesi asilia suala ambalo limepunguza gharama kubwa ambayo ilikuwa inatumika wakati wakitumia nishati mbadala ya kuni na mkaa. Wakati wakitumia nishati hiyo walikuwa wanatumia shilingi milioni saba. Sasa baada ya kuweka mfumo wanatumia shilingi milioni 1.8.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mfumo huo kwenye Taasisi zote za Serikali ikiwemo Chuo cha Ualimu Matogolo na Shule za Sekondari zote katika Mkoa wa Ruvuma na nchi yote ya Tanzania? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofuatilia matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la ruzuku, ajenda ya nishati safi ya kupikia ni ajenda ya Mheshimiwa Rais mwenyewe.

Wote mnakumbuka wakati wa mkutano wa *COP28* Dubai, alizindua Mkakati wa Nishati ya Kupikia kwa Wanawake Afrika. Kwa hiyo, jambo hili tumelibeba kwa uzito sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku tayari tuna programu na miradi kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya tunayo programu ambapo mawakala wanawezeshwa kifedha ili kupunguza bei ya mitungi kwa wale wanunuaji wanaonunua gesi kwa mara ya kwanza. Tutaendelea kubuni miradi na kutafuta fedha ili kuhakikisha wananchi wanapata mitungi ya gesi kwa gharama rahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusiana na kuwekeza mifumo ya gesi katika taasisi; kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA)* tumeshaanza mradi kwa ajili ya kuweka nishati hii safi ya kupikia ya gesi kwenye magereza, kambi za Jeshi pamoja na shule za msingi na sekondari. Tutaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha tumefikia taasisi nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa taasisi alizosema za Mkoa wa Ruvuma tutazingatia pia, ili kuhakikisha wanawekewa mifumo hii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum; swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Fatma Toufiq.

Na. 58

**Wananchi wote kujua kusoma na kuandika**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ K.n.y. MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Watanzania wote wanajua kusoma na kuandika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kulingana na ripoti iliyotolewa na *NBS*, kwa sensa ya mwaka 2022 Tanzania imefikia kiwango cha asilimia 83 cha kujua kusoma na kuandika miongoni mwa watu wazima (miaka 15 na kuendelea), ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.3 kutoka asilimia 78.1 cha sensa ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Watanzania wote wanajua kusoma na kuandika, Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo kuondoa vikwazo vya kupata elimu kama vile kutolewa kwa elimu ya msingi bila ada, elimu ya lazima sasa kuwa ya miaka 10, kutekeleza programu zenye lengo la kuwafikia Watanzania waliokosa fursa za elimu. Kwa mfano, Elimu ya Watu Wazima na ujifunzaji endelevu, utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kusoma pamoja na kutoa fursa kwa wanafunzi walioacha masomo kwa sababu mbalimbali kurudi shuleni na kuendelea na masomo *(re-entry program)* kupitia Waraka Na. 2 wa mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, pamoja jitihada hizo, Serikali imeendelea kuboresha huduma za maktaba nchini katika ngazi za mikoa, wilaya na shule, ikiwa ni pamoja na maktaba mtandao, ili kuwawezesha Watanzania wengi zaidi katika maeneo mbalimbali kupata huduma ya kusoma huko waliko.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa lengo la kuongeza fursa kwa Watanzania wengi zaidi kujiunga na Elimu ya Watu Wazima, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu ya Serikali; pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwabaini wale watanzania wenye umri wa zaidi ya miaka 35 ambao hawako katika programu ya *Re-Entry* na zile programu afua zingine wasiojua kusoma na kuandika ili waweze kufikiwa?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikishwa kwamba, shule za msingi na shule za sekondari zote zinakuwa na maktaba ili kusudi wanafunzi waweze kujisomea?*)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza la Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kueleza katika majibu ya swali la msingi. Serikali inazo kwanza takwimu za kutoka *NBS* zinazotuthibitishia uwepo wa watu wasiojua kusoma na kuadika. Ongezeko hili la watu wasiojua kusoma na kuandika limekuwa likipungua kutoka asilimia 78 mwaka 2012, mpaka asilimia 83 katika Sensa ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa vile tayari sasa tunafahamu idadi hii au takwimu hizi, Serikali kupitia mpango mikakati hii ambayo nimeitaja ikiwemo na mpango wa Serikali wa Uwiano katika Elimu ya Watu Wazima na Jamii unaojulikanika kama MKEJA, ndio ambao utahakikisha sasa idadi hii ya Watanznaia wasiojua kusoma na kuandika, wale wenye umri zaidi wa miaka 35 tunaweza kuwafikia.

Mheshimiwa Spika, pia katika eneo la pili la suala la shule zetu za msingi na sekondari kuwa na maktaba, suala hili tayari Serikali imeshalifanyia kazi. Katika miundombinu ambayo inajengwa sasa hivi katika Shule zetu za msingi pamoja na sekondari ni lazima kuwe na jengo la maktaba, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri tuna zaidi ya asilimia 16 ya Watanzania ambao hawajui kusoma na kuandika. Sasa nilitaka kujua Mkakati wa Serikali wa kuhakikisha tunatenga bajeti kwenda kuhudumia Watanzania ambao wanapata elimu kutoka kwenye mfumo usio rasmi kama vile, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ambao kwa sasa hawapati ruzuku, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Tweve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tweve anatoa ushauri kwamba, Serikali tuweze kupanga bajeti kupitia Taasisi yetu ya Elimu ya Watu Wazima. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, tutakwenda kufanya tathmini ya kina namna gani tunaweza kutenga bajeti kwenye Taasisi yetu ya Elimu ya Watu Wazima, ili kuweza kulifikia kundi hili la watu wasiojua kusoma na kuandika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Najma Giga, swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na takwimu hizo za wasiojua kusoma na kuandika pamoja na mikakati mizuri ya Serikali, je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuwa na takwimu halisi za viwango vya elimu na makada zake, kuanzia

kiwango cha juu cha elimu hadi kufikia chini kwa mustakabali mzuri wa maendeleo ya Taifa letu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Waziri amesimama. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa, ningeomba nitoe maelezo kidogo kuhusu suala la takwimu kwa Mheshimiwa Najma.

Mheshimiwa Spika, tunao mfumo wa takwimu wa elimu unaitwa *BEST (Basic Education Statistics of Tanzania)* ambao kwa muda mrefu ulikuwa uki-*focus* kwenye shule ambazo zinamilikiwa na TAMISEMI na shule zinazotumia mtaala wa Taifa. Sasa hivi tunacho kikosi kazi kinafanya kazi kuhakikisha kwamba, kuna dawati la kuhakikisha kwamba, takwimu za elimu kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vikuu zinakusanywa katika *document* ambayo tutakuwa tunaitoa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, vilevile tutajumuisha watoto wanaosoma katika hizi shule zingine ambazo zinatumia mitaala kama *Cambridge*. Kazi hiyo inaendelea na hata leo mchana tunakutana kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, tunaelewa kabisa *concern* ya Mheshimiwa Najma na tunaifanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, upi sasa mkakati wa haraka zaidi kuhakikisha tunawanusuru watoto wadogo ambao wanapatikana hususan katika jamii za wafugaji na wavuvi

ambao hawajui kabisa kusoma na kuandika, kuweza kuwanusuru watoto hao ili waweze kujua kusoma na kuandika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Martha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika maboresho ya mtaala ambayo tuliyapitisha mwaka jana, unakwenda kuchukua ngazi zote za watoto wetu kuhakikisha kwamba wanakuwa shule. Katika sera pamoja na mitaala hii ni wajibu wa kila Mtanzania kuhakikisha kwamba, yule mtoto ambaye tayari ameshafika umri wa kwenda shule aweze kwenda shule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, nitoe tu maelekezo kwa Wakurugenzi wetu wote wa halmashauri, Wakuu wa Wilaya ambako ndiko hawa watoto waliko, iwe eneo la wafugaji au iwe eneo la wavuvi, kuhakikisha vijana wetu ambao tayari wameshafikia umri wa kwenda shule waweze kuandikishwa na kuweza kukaa shuleni kwa ajili ya kusoma, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Almas Maige.

Na. 59

**Sheria Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta Bungeni sheria mahsusi kwa ajili ya kuwalinda wananchi dhidi ya ukatili wa kijinsia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, majibu.

**WAZIRI KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunazo sheria zinazowalinda wananchi dhidi ya ukatili wa kijinsia ambazo ni Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16; Sheria ya Ndoa, Sura ya 29; Sheria ya Mtoto, Sura ya 13; Sheria ya Makosa ya Mtandao, Sura ya 443; na Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432. Kwa pamoja sheria hizo zina vifungu vinavyozuia makosa ya ukatili wa kijinsia. Sheria zote kwa pamoja zina vifungu vinavyoshugulika na makosa ya ukatili wa kijinsia. Hata hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta ikiwemo Wizara ya Maendeleo, Jinsia, Watoto na Makundi Maalum, Wizara ya Mambo ya Ndani, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na wadau mbalimbali tunaendelea na uchambuzi ili kubaini iwapo ipo haja ya kuwa na sheria mahsusi ya ukatili wa kijinsia au tuboreshe sheria zilizopo. Baada ya kukamilika kwa uchambuzi huo Serikali itachukua hatua stahiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja tu la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile makosa haya ya ukatili wa kijinsia sasa yanaendana na makosa ya kuporomoka kwa maadili.

Je, Serikali haioni haja ya kuboresha sheria hii iliyopo sasa ili kuchanganya tiba ya makosa haya yanayotokana na kuporomoka kwa maadili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nijibu swali la nyongeza kuwa Serikali inaona haja ya kuboresha sheria hizi, hivi sasa tupo katika mchakato wa kupitia taarifa maalum ya masuala ya maadili.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka katika Bunge hili tulizungumza sana kuhusu masuala ya maadili, masuala ya mahusiano ya jinsia moja. Nimeshaunda timu maalum pale Wizarani na wanaandaa taarifa kuona namna gani sheria hizi tuendelee kuziboresha. Kwa hiyo, haja ya kuboresha ipo na ndiyo jukumu la msingi la Bunge. Kazi ya Bunge ni kutunga sheria, kazi ya Bunge ni kurekebisha sheria, kwa hiyo, suala la kuangalia kama ipo haja au haipo kwa kweli, nichukue nafasi hii kusema tu kwamba, hilo ndilo jukumu la msingi kabisa la Wizara yangu na tunaendelea kuangalia namna gani tuendelee kuziboresha sheria zetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karagwe imeathirika sana na ukatili wa kubakwa watoto kuanzia miaka mitatu mpaka nane,

wakati huu ambapo sheria haijatungwa, hatua zipi za haraka zitachukuliwa ili kunusuru kizazi hiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, si kwamba sheria haijatungwa, ni kwamba sheria tunazo mbalimbali za masuala ya ukatili, lakini swali la msingi lilitaka sheria zote hizi za masuala ya ukatili wa kijinsia ziwe kwenye sheria hii moja. Sheria ya Mtoto inaelezea masuala ya ukatili kwa mtoto, Sheria ya Ndoa inaelezea ukatili ndani ya masuala ya ndoa. Pia tunayo Sheria ya Kanuni ya Adhabu, huko nyuma tulikuwa na Sheria ya Masuala ya Kujamiiana na yale yote makosa ya kujamiiana *(Sexual Offence Act.)* tukaingiza kwenye *Penal Code*. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, sheria tunazo na kifungu 131 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu kinaelezea vizuri kabisa masuala ya ukatili.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwamba, yako maeneo kuna ukatili wa watoto. Nichukue nafasi hii kusema tu kwamba, maeneo yote ambako kuna ukatili wa watoto kwanza tunaomba taarifa zifike katika vituo vyetu vya Polisi na vituo vyote vya haki jinai. Tunayo sheria hata ya kumlinda mtoa taarifa, tunaita *Whistleblowers Act.* Kwa hiyo, Sheria hii ya *Penal Code* hivi sasa ipo na kwa kweli, inakidhi haja pale ambapo mtoto amefanyiwa ukatili tena chini ya miaka kumi, sheria inaeleza wazi kabisa ni kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Spika, hoja ilikuwa ni kuzichanganya sheria zote ziwepo kwenye sheria hii moja. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa na kumpongeza kwamba, kujali watoto ni suala la msingi sana, lakini pia sheria zilizopo kwa kweli kwa sasa zinakidhi haja ya makosa haya ya ukatili wa kijinsia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, sasa aulize swali lake.

Na. 60

**Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati au kujenga Mahakama mpya ya Wilaya ya Ukerewe?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama inaendelea na utekelezaji wa mpango wa kujenga na kukarabati majengo katika ngazi mbalimbali. Aidha, katika ngazi ya Mahakama za Wilaya, bado tuna Wilaya ambazo hatuna majengo na hivyo, kulazimika kutumia majengo ya kuazima kwenye taasisi nyingine kama Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Wilaya ya Ukerewe kwa sasa inafanya kazi kwenye majengo ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Hata hivyo, katika mpango wetu wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama, tumepanga kujenga Mahakama ya Wilaya ya Ukerewe katika mwaka wa fedha 2024/2025. Naomba nitumie fursa hii kuishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kwa kutupatia kiwanja kwa ajili ya kujenga jengo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza niipongeze Serikali kupitia Wizara kwa kutupatia pesa za kujenga Mahakama ya Mwanzo Ilangara, ujenzi unaendelea, lakini kwa mpango vilevile wa kutupatia pesa kwa ajili ya kujenga Mahakama kwa mwaka huu, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kiwanja kilichopatikana kiko mbali na maeneo wanayoishi wananchi na kuna eneo ambalo linatumika sasa linalomilikiwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na yuko tayari kulitoa kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama. Wizara iko tayari kujadiliana na kukaa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ili eneo hili lenye ukubwa wa mira za mraba zaidi ya 3,300 liweze kutumika kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hiyo? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, eneo ambalo tunakwenda kujenga hii Mahakama ya Ukerewe lipo *Airport,* Kata ya Mkirizya, na tayari tathmini imeshafanyika na wananchi wamekwishafidiwa kwa ajili ya ujenzi. Sasa suala analolisema Mheshimiwa kwamba, kuna kiwanja kingine tuone namna gani ya ku-*shift* na huku tumeshalipa fidia kwa wananchi tayari kwa ujenzi, inaweza ikawa ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba nilichukue tulifanyie kazi kama tunaweza ku-*shift,* maana kule wananchi wameshafidiwa tayari kwa kujenga, sasa ku-*shift* mahali pengine inawezekana kukawa na masuala ya gharama na kadhalika, ikawa changamoto, lakini hata hivyo naomba nilichukue.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, sasa aulize swali lake.

Na. 61

**Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji – Ulanga**

**MHE. SALIM A. HASHAM** aliuliza:-

Je, lini serikali itajenga skimu za umwagiliaji katika Jimbo la Ulanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(ASDP II)* inaendelea kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Skimu za Euga, Ulanga, hekta 440, Minepa, Ulanga, hekta1,800 na Lupilo, Ulanga, hekta 3,000. Mara baada ya zoezi la upembuzi yakiniffu kukamilika skimu hizi zitaanza kujengwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, swali la nyongeza.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali imeliongezea Bonde la Mto Kilombero kwa maslahi mapana ya Taifa letu, kwa hiyo wananchi wa maeneo hayo wamekosa maeneo kwa ajili ya kilimo.

Je, ni lini Serikali itaenda kujenga mradi mkubwa, ili kutoa fursa kwa wananchi wa Jimbo la Ulanga, hususan kwenye Kata za Kichangani, Milola na Minepa, ili kupata sehemu ya uhakika ya uzalishaji mali?

Swali la pili, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kuboresha na kuuendeleza Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Minepa yenye

ukubwa wa zaidi ya hekta 1,800 ili kutoa fursa kwa wananchi wa vijiji hivyo kupata sehemu kubwa ya uzalishaji mali? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kama nilivyojibu katika swali langu la msingi kwamba, Skimu ya Minepa tunafanya upembuzi yakinifu na tunajua umuhimu wa skimu hiyo kwa sababu ina hekta karibu 1,800. Kwa hiyo, wakishamaliza watu wetu sisi jukumu letu ni kutafuta fedha na tutaanza ujenzi mara moja kwa sababu ya umuhimu huo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hii ya kwenye swali lake la kwanza vilevile alipouliza kuhusu eneo la Bonde la Kilombero na zile Kata za Kichangani, Milola na Minepa, wananchi bado wanauhitaji. Kwa hiyo, sisi bado tuko huko tunafanya upembuzi yakinifu, tukishakamilisha tu tutatoa taarifa hata kwa Mbunge mwenyewe na Wilaya yake, Ivilevile tutatafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 62

**Tatizo la usafiri kwa mahabusu na wafungwa nchini**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua tatizo la usafiri kwa ajili ya kusafirisha mahabusu na wafungwa katika magereza nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto iliyopo ya magari ya kusafirisha mahabusu na wafungwa kwa kuwapeleka Mahakamani na kuwarudisha gerezani. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia Jeshi la Magereza ilitenga kiasi cha shilingi 878,125,000.00 katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa magari matano ya kusafirishia mahabusu na wafungwa katika Magereza nchini. Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga fedha, kiasi cha shilingi bilioni 1.93 kwa ajili ya ununuzi wa magari 14 kwa ajili ya kusafirisha mahabusu na wafungwa katika magereza nchini. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Haki ya Tume Jinai ilibainisha changamoto kubwa sana kwa Jeshi la Magereza kwa kuwa na magari chakavu sana ambayo yamenunuliwa muda mrefu sana na bajeti inayotengwa ni ndogo na hatuna uhakika kama inawafikia. Sasa nina maswali mawili.

Swali la kwanza; je, katika fedha ambazo anasema zilitengwa kwa bajeti liyopita za milioni 882 za kununua magari matano, je, yamenunuliwa na yamekwenda gereza gani?

Swali la pili; kwa kuwa, wafungwa hao Serikali inatumia gharama kubwa sana ku-*maintain* magari chakavu na hakuna *economic benefit* inayoipata mwisho wa siku. Kwa nini, Serikali isitafute utaratibu rafiki zaidi kama kuwa na mikataba ya muda mrefu kwa gharama nafuu ya kukodisha magari ambayo ni *decent* kwa ajili ya Watanzania hawa ambao wamejikuta kwenye changamoto kwa wakati huo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwanyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, juu ya milioni 878 ninakiri kwamba fedha hizi zilichelewa kutoka lakini tunashukuru Wizara ya Fedha iliridhia ku-*double* kiwango hicho ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu 1,930,000,000 zimewekwa kwa ajili ya kununulia magari hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mchakato wa manunuzi umeendelea na maombi ya fedha hizi Wizara ya Fedha yamefanyika ili fedha zitakapopatikana malipo yaweze kufanyika na hatimaye tuweze kupata magari husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuingia mkataba wa muda mrefu ili kuboresha haki ya wafungwa kupata usafiri, tunachukua ushauri huo ili tuweze kuufanyia kazi kuona kufanya *leasing* ili ikiwezekana wakati wowote wafungwa wasikwame kwenda magerezani kwa sababu ya ukosefu wa magari, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Mustafa Mwinyikondo Rajab, Mbunge wa Dimani, sasa aulize swali lake.

Na. 64

**Kurejesha huduma za zahanati Kambi ya Jeshi Kisakasaka**

**MHE. MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarejesha huduma za afya zilizokuwa zikitolewa kwa wananchi na zahanati ya jeshi, Kambi ya Jeshi Kisakasaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mustafa Mwinyikondo, Mbunge wa Dimani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Kisakasaka ni Kiteule cha 672 Rejimenti ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tazania ambayo ina kikundi kidogo cha Maafisa na Askari. Kiteule hiki hutoa huduma za matibabu za msingi zinazojumuisha madawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa Wanajeshi waliopo katika Kiteule hicho. Maafisa na Askari waliopo katika Kiteule hicho wanapozidiwa hupelekwa katika Zahanati ya Kikosi Mama iliyopo maeneo ya Welezo umbali wa kilometa 17.

Mheshimiwa Spika, hapo awali Kiteule hiki kilikuwa kinatoa huduma za afya kwa Wanajeshi na wananchi, Huduma kwa wananchi zilisitishwa mwaka 2010 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za miundombinu kutokukidhi kutoa huduma kwa wananchi wengi na upungufu wa watalaam wa tiba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika eneo la Kisakasaka kipo Kituo cha Afya cha Fuoni Kibondeni cha Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar kilichoanzishwa mwaka 2004, ninapenda kuwaomba wananchi waendelee kupata huduma kupitia kituo hicho wakati Wizara inatekeleza mkakati wa kuimarisha huduma za afya Jeshini, kwa kufanya maboresho katika hospitali za kanda, vituo vya afya na zahanati zilizopo katika vikosi chini ya kamandi mbalimbali nchini, zikiwemo zahanati za Jeshi zilizopo Zanzibar, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mustafa Mwinyikondo Rajab, swali la nyongeza.

**MHE. MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB:** Mheshimiwa Spika, nimeridhika na majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Constatine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 63

**Wananchi wanaoishi ndani ya Eneo la Leseni *GGM***

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, lini Wananchi wa Nyambalembo, Magema, Katoma, Mizingamo, Katumai na Nyakabale wanaoishi eneo la leseni ya GGM watalipwa fidia?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikishughulikia mgogoro baina ya wananchi na Mgodi wa GGM kwa kufanya majadiliano na mgodi huo ili kutafuta muafaka wa namna bora ya kumaliza migogoro katika kila eneo husika, ikiwa ni pamoja na ulipaji wa fidia stahiki. Majadiliano hayo yanaendelea katika maeneo ambayo bado hayajapatiwa utatuzi wa pamoja kuhusiana na ulipwaji wa fidia. Majadiliano yakikamilika Wizara itatoa taarifa. Kwa maeneo ambayo hayakuwa na ubishani wa upande wowote, zoezi la uthamini wa ardhi na mali za wananchi wanaoishi katika maeneo hayo, linaendelea kwa ajili ya ulipwaji wa fidia.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, taratibu za uthamini wa ardhi na mali za wananchi wanaoishi katika eneo la Samina ambalo nalo liko ndani ya leseni ya GGM zinaendelea, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Natumia fursa hii kwanza kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Madini na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kwa ushirikiano mkubwa ambao tumeufanya hadi kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji anatumia upungufu uliomo kwenye Sheria yetu ya Madini na Sheria ya Ardhi kuendelea kuchelewesha au kukwamisha mazungumzo yanayoendelea; na kwa sababu hiyo kuendelea kuwatesa wananchi ambao wamekaa kwenye mgogoro huu kwa zaidi ya miaka 22.

Mheshimiwa Spika, sasa, kwa nini wakati tunaendelea kubishana, Serikali isichukue jukumu la kulipa fidia yenyewe, halafu ikaendelea kujadiliana upungufu wa kisheria unaoendelea kuwepo eneo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; naipongeza sana Serikali kwa tathmini ya awali inayoendelea kule Samina. Eneo linalofanyiwa tathmini linafanana kabisa na maeneo nane yaliyobaki. Kwa nini sheria ile ile ambayo imetumika kufanya tathmini kwa wananchi wa Samina isitumike kwenye maeneo mengine ambayo sasa hivi Serikali inasema bado inafanya mazungumzo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Kanyasu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali kulipa fidia, napenda kumjulisha kwamba, Serikali inapotoa leseni kwa mwekezaji, yule mwenye leseni ndiye anakuwa na Haki Madini pale na ndiye mmiliki wa madini. Hivyo, siyo tena Serikali yenye wajibu wa kulipa fidia ya aina yoyote. Kwa hiyo, kwa maridhiano kati ya mwenye leseni na wananchi na viongozi wa eneo lile, akikubali kuwalipa fidia kama anavyoomba kwamba fidia ilipwe hata kabla hajaweza kuhamishwa, hilo tunawaachia wao kupitia mfumo ulioko wa maridhiano na mahusiano mema na jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, kwamba kwa nini Serikali isilipe? Majibu ni kama hayo tu kama nilivyotangulia kusema, kwamba Serikali siyo mmiliki tena wa yale madini. Amepewa Haki ya madini yule aliyepewa leseni na ndiye mwenye dhamana ya kufanya kazi na wananchi ili waweze kulipa.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kumjulisha Mheshimiwa Mbunge na nampongeza kwa namna anavyofuatilia swali hili

kwamba, tulishaunda Kamati kati ya Wizara, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ya Geita ambayo inaendelea na mazungumzo ya kutafuta namna bora ya kuwafidia wale watu ambao ni lazima wahame, kama hao wa Samina ambao karibu hatua za mwisho zinafikiwa na hawa wengine ambao walisema hawatayahitaji maeneno yao lakini itafutwe namna bora ya kuwashika mkono au kwa ajili ya usumbufu ili waweze kuendelea na maisha yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, sasa aulize swali lake.

Na. 65

**Ujenzi wa Majosho Kijiji cha Gwandi na Takwa – Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Majosho kwenye Vijiji vya Gwandi na Takwa – Chemba?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mbunge wa Misungwi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa majosho nchini ili kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe na wadudu wengine. Kupitia mpango huo, jumla ya majosho mapya 747 yamejengwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2020/2021 hadi Juni, 2023 yakiwemo majosho matano yaliyojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba katika Vijiji vya Tumbakose,

Mlogia, Mondo, Msaada na Masimba ambapo ujenzi umekamilika na yameshaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Sipika, kwa kutambua umuhimu wa majosho katika kudhibiti magonjwa ya mifugo nchini, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itaendelea kutenga fedha za ujenzi wa majosho maeneo mbalimbali nchini yakiwemo ya Vijiji vya Gwandi na Takwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Kwanza kabisa, naomba nichukue fursa hii kuishukuru Wizara kwa majosho matano. Nina swali moja tu la nyongeza. Nataka kujua kama Wizara inajua kwa uhakika katika vijiji vyetu vyote 114, mahitaji ya majosho ni kwa kiwango gani, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, sasa aulize swali lake.

Samahani Mheshimiwa. Nimekumbushwa hapa, bado Mheshimiwa Mnyeti hajajibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Monni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli kwamba Wizara ina *Database* ya kujua wapi panahitajika josho lipi, kwa *size* gani na kwa umuhimu gani? Pia, Mheshimiwa Mbunge kama anaona kuna sehemu ambapo sisi kama Serikali tunapaswa kwenda kujenga josho, alete taarifa zake tuweze kufanyia kazi kwenye maeneo hayo. Hata hivyo, mpaka sasa *database* ya vijiji ambavyo majosho yanatakiwa kujengwa, Serikali ina hiyo *database*, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Viijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 66

**Msaada wa kitalaamu Bwawa la Nyumba ya Mungu**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa msaada wa kitaalamu kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu ili kuongeza idadi ya samaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mipango na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha samaki wanaendelea kuwepo na wanaongezeka katika maeneo yote ya maji, ikiwemo Bwawa la Nyumba ya Mungu. Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya tafiti na kuimarisha ushirikishwaji wa jamii na taasisi zisizo za kiserikali katika kusimamia na kulinda rasilimali za uvuvi kupitia Halmashauri, Serikali za Vijiji na Vikundi vya kijamii vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi *(BMU)*.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kufanya tafiti za kujua wingi na mtawanyiko wa samaki katika maziwa makuu na imejipanga kutanua wigo wa kufanya tafiti *(frame survey)* kwa maziwa madogo ili kutambua hali halisi ya uvuvi katika maziwa hayo. Aidha, tafiti hizo zinatoa taarifa sahihi ili kuiwezesha Wizara

kutekeleza mikakati ya kuongeza wingi wa samaki ikiwemo uwezekano wa kupandikiza samaki.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara itaendelea na utoaji wa elimu ya Huduma za Ugani kuhusu athari za uvuvi haramu ili kulinda mazalia ya samaki na kuruhusu samaki kukua na kuongezeka kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na nina maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia Wavuvi wa Bwawa la Nyumba ya Mungu zana na nyenzo za uvuvi kama vile nyavu, boti na vizimba, kama ilivyofanya hivi karibuni kwa wenzao wa *Lake Victoria*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; uvuvi haramu ni chanzo kikubwa cha kuzorotesha uchumi wa Samaki; na Maafisa Uvuvi wa hapa nchini na hata kule Nyumba ya Mungu, wameweka mkazo kwenye kuwakamata wavuvi na kuwapiga faini badala ya kutoa elimu endelevu ya namna bora ya kufanya uvuvi: Je, Serikali haioni umuhimu wa kuchukua hatua kupambana na hali hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nianze na hili la kwanza. Kwanza ugawaji wa nyenzo za uvuvi kama boti, nyavu na kadhalika, kama ambavyo Mheshimiwa Rais alifanya juzi kule Mwanza, Ziwa Victoria, hii ni fursa kwa Watanzania wote kwenye maziwa na mabwawa mbalimbali, wanaruhusiwa kuchukua nyenzo hizi kwa njia ya kukopa kupitia *TADB*, benki yetu ya kilimo ambapo ukiwasilisha andiko lako vizuri kwa kupitia wataalamu wetu,

unaweza kupata ushauri na baadaye ukakopeshwa nyenzo hizo ukafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii ni fursa kwa Watanzania wote ikiwemo wavuvi wa Bwawa la Nyumba ya Mungu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, kwanza nikupongeze sana kwa ufuatiliaji na namna ambavyo unaendelea kufuatilia. Umekuwa msumbufu sana kwenye hili. Tunakupongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli tupo tayari kukupa ushirikiano ili wavuvi wako waweze kupata nyenzo hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kwamba Maafisa Uvuvi kazi yao ni kuhakikisha wanasimamia shughuli za uvuvi kwenye maeneo yao pamoja na kutoa elimu kwa wavuvi wetu. Natoa wito na rai kwa Maafisa Uvuvi wote nchini kuhakikisha kwamba wanajikiza zaidi kwenye kutoa elimu na kusimamia shughuli za uvuvi na siyo kujigeuza kuwa Maafisa Masuuli na Maafisa wa Mapato, kukatisha ushuru na mambo mengine ambayo hayawahusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatoa wito kwa Maafisa wote kwamba sasa wajielekeze kwenye kazi yao ya msingi ambayo wanatakiwa kufanya kwenye maeneo yao huko wanakofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyeti, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa naleta matangazo niliyonayo hapa mbele na tutaanza na tangazo la wageni. *(Makofi)*

Kwanza, tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika; kuna wagezi wangu 24 ambao wanaitwa *Family Members Group* kutoka

Mkoa wa Mbeya, wakiongozwa na Ndugu Nyalu Laurent Mifwa ambaye ni Mwenyekiti, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; hawa ni Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar; yupo pia Dkt. Jim James Yonazi ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Islam Seif Salum ambaye ni Katibu Mkuu wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar; yupo pia Ndugu Anderson Mutatembwa, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; yupo pia Jaji Jacob Casthom Mwambegele, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi; yupo pia Mheshimiwa Jaji George Joseph Kazi ambaye ni Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar; yupo pia Mheshimiwa Jaji *(Retired)* Mbarouk S. Mbarouk ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi; yupo pia Mheshimiwa Jaji Mstaafu Francis Sales Mutungi ambaye ni Msajili wa Vyama vya Siasa, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Mohammed Ally Ahmed, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa; yupo Ndugu Ramadhan Kombway Kailima ambaye ni Mkurugenzi wa Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi; na yupo pia Ndugu Thabit Idarous Faina ambaye ni Mkurugenzi wa Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi Zanzibar, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni 11 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni viongozi wa *CBESO* kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni 30 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji,

hawa ni Uongozi wa Serikali ya Wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(DARUSO),* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Hussein Bashe ambaye ni Waziri wa Kilimo; hawa ni rafiki zake kutoka Arusha. *(Makofi)*

Tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Omari J. Kipanga ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, hawa ni wanafunzi kutoka Chuo cha Ufundi Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Omari Kigua ambaye ni Mkurugenzi wa *Chef Pride* kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Rose Tweve ambao ni Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa ambaye ni ndugu yake kutoka Tanga. *(Makofi)*

Tunao wageni wanane wa Mheshimiwa Subira Mgalu ambao ni Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kutoka Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ambao ni wapiga kura wake kutoka Tarime Vijijini, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ighondo Ramadhan ambaye ni Katibu wa CCM Kata ya Mgunga, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mwantumu Zodo ambao ni familia yake kutoka Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Simon Songe ambaye ni mpiga kura wake kutoka Simiyu, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi ambaye ni mpiga kura wake kutoka Musoma Mjini, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina ambao ni viongozi wa Tawi la Kajengwa kutoka Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* kutoka Mbozi, Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Salome Makamba ambaye ni mtoto wake anaitwa Edwin Makamba, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 130 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Cannosa ya Jijini Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao asubuhi hii Bungeni.

Ninalo jambo moja hapa, halafu tutaendela na ratiba.

Waheshimiwa Wabunge, tumepata Tuzo ya Uandaaji Bora wa Hesabu za Fedha kwa mwaka 2022, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwapa taarifa kuwa Mfuko wa Bunge - Fungu 42 umefanikiwa kupata Tuzo ya Mshindi wa Pili wa Utayarishaji Bora wa Hesabu za Fedha kwa mwaka 2022 *(Second Winner in the Ministries and Government Departments Category for the Best Presented Financial Statement Award for the Year 2022)*. *(Makofi)*

Tuzo hii imetolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi, yaani *The National Body of Accountancy and Auditors (NBAA)*,

mwezi Disemba 2023, katika mkutano wake mkuu wa mwaka 2023. Ushindi huu ni mwendelezo wa ushindi tuliyopata mwaka jana ambapo tulikuwa washindi wa tatu na sasa tumepanda kwa nafasi moja na kuwa washindi wa pili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuzo hizo zinatolewa na *NBAA* kila mwaka kwa lengo la kuhamasisha wizara, mikoa, idara, taasisi, mashirika na kampuni binafsi kuzingatia viwango vya kimataifa katika uwaandaaji wa hesabu. Kwa msingi huo Mhimili wa Bunge unaendelea na dhamira yake yakusimamia weledi wa wahasibu na wakaguzi wetu ili kuhakikisha tunakuwa mfano katika kusimamia mali za umma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kuwapongeza sana sana wahasibu wetu na Wakaguzi wetu lakini pia kumpongeza sana Katibu wa Bunge, kwa uongozi wake bora kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, japokuwa siyo kazi yetu kutangaza washindi wengine ni wakina nani lakini nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameona umuhimu wa tuzo hizi lakini nimejulishwa kwamba taasisi iliyoshinda ipo chini yake. Kwa hiyo, tunawapongeza pia Wizara ya Fedha, tunawapongeza sana Wizara ya Fedha pia. *(Makofi)*

Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza wale ambao wamefuatilia kwa umakini hizo hesabu zote hata kuweza kupata hao washindi na kutangaza tuzo hii nikuwaeleza wakaguzi na wahasibu wa vitengo vyote kujitahidi kufanya vizuri ili wote tuweke hesabu zetu vizuri kama ambavyo Bunge linaonyesha mfano mzuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naipongeza pia Tume ya Utumishi ya Bunge kwa usimamizi mzuri na pia kama nilivyosema Katibu wa Bunge, anafanya kazi nzuri na sasa Mhasibu wetu Mkuu na wahasibu wote wanaofanya kazi chini yake na wakaguzi wetu wa ndani tunawapongeza wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo sasa tuzo yenyewe ipo hapa nimeletewa. Watu wasije wakasema ameuziwa mbuzi kwenye gunia, tuzo ipo hapa na niwasomee, *The National Body of Accountancy and Auditors Tanzania, this Award is Given to the National Assembly Fund Vote No.42 as the Second Winner in the Ministries and Government Department Category for the Best Presented Financial Statement Award for the Year 2022. Awarded on the 01st December, 2023. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuzo yenu hii. Kwa hiyo itaenda kukaa pale *library* kwa muda kidogo muipitiepitie halafu tutaiweka mahali pake panapostahili, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023**

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Law Amendment Bill, 2023)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na wale Wabunge waliyokuwa wamekusudia kuchangia leo kwa ratiba

tuliyokuwa nayo uchangiaji ulikuwa unaisha jana na sasa majadiliano yanaendelea kwa maana ya kwamba, Serikali sasa ije ihitimishe hoja zote tatu, wataitwa kwa hoja moja moja.

Nimwite sasa Mheshimiwa Waziri. Anaanza Naibu na Muswada upi? Haya Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023. Hoja hiyo ije ihitimishwe. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kunijalia…

**SPIKA:** Ngoja, ngoja. Sasa ili niwe nimeelewa vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri, hukupata nafasi ya kuchangia jana, maana uhitimishi hoja hapo, bali unachangia, hukupata nafasi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya karibu. Waheshimiwa Wabunge, anachangia, hahitimishi hoja.

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kusimama leo tunapohitimisha mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, niishukuru familia yangu, mume wangu na mtoto wetu kwa kunivumilia na kunipa ushirikiano wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa imani yake kwangu. Mheshimiwa Rais, amenipa heshima kubwa kuingia katika historia yakushiriki nikiwa Naibu Waziri, kusaidia kufanya mabadiliko ya sheria hizi muhimu kwa Taifa letu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais,

ahsante sana Mama, ninakushukuru Mwenyezi Mungu akubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa miongozo yake na uongozi wake hadi leo tunapohitimisha jambo hili. Vilevile, nimshukuru Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto, kwa miongozo na *support*. Mheshimiwa Makamu wa Rais pia namshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uniruhusu namimi nikushukuru wewe kwa miongozo yako na namna ambavyo umetuongoza kwenye kuliendea jambo hili la kujadili miswada hii, ninakushukuru sana na sisi wanawake tunakuchukulia kama *role model* wetu uliyepiga hatua kubwa. Tunajivunia sana, tunakupongeza na ninakushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uniruhusu nimshukuru, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wangu niungane na Waheshimiwa Wabunge, kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa upendo, malezi, miongozo yake tangu tulipoanza kuweka mezani miswada hii. Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Jenista, ametuongoza kwa hekima, uaminifu, uzalendo na uadilifu mkubwa mpaka leo tunapohitimisha Waheshimiwa Wabunge, naungana na nyinyi kuendelea kumpongeza sana. Hongera Mheshimiwa Waziri lakini hongera pia kwa wana Peramiho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Katibu Mkuu wetu na timu yake nzima kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya kutusaidia kufika hapa. Nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati, Dkt. Mhagama, Makamu wake na Wajumbe. Kamati yetu imefanya kazi kubwa sana, usiku na mchana wamejitoa. Wamefanya kazi hii kwa uzalendo mkubwa, tunawapongeza sana Kamati, ahsanteni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge, wamechangia mengi tulikubaliana na Kamati na tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo mlichangia na kusheheneza mjadala wetu jinsi ambavyo ulikuwa unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee, pamoja na mijadala kuwa mingi na michango mbalimbali. Nasimama nikiwa mwanamke naomba niwapongeze sana Wabunge wanawake wenzangu kwa namna mlivyojadili lakini na Wabunge wanaume namna walivyounga mkono jambo hili. Wote hatubishani, mchango wa wanawake katika Taifa hili ni mkubwa, siyo wa kubezwa ni wa kupigiwa mfano lakini tunaye mwanamke imara na jasiri na mahiri kwelikweli Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye anatuvusha kwenye kufanya mabadiliko ya kidemokrasia katika Taifa letu. Kwa hiyo, nimeona kwa kweli nisiache kuwashukuru wanawake wezangu. Sauti zenu tumezisikia na Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu nzima tunafanyia kazi mambo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasimama tena nikiwa kama mtu mwenye ulemavu katika Bunge lako hili. Kwa hiyo, kipekee niendelee kushukuru na kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa imani yake. Katika kipindi changu cha Bunge ni kipindi kifupi lakini katika umri wangu wa kuishi katika dunia hii pia ni kipindi kifupi. Mheshimiwa Rais, ameniamini kuingia katika historia yakumsaidia kwa karibu Mheshimiwa Waziri wangu, Mama Jenista, ili tulipeleke Taifa letu kwenye kupata sheria ambazo zitaendelea kuimarisha demokrasia kwenye nchi yetu. Ninakushukuru tena na tena Mheshimiwa Waziri wangu kwa namna ambavyo umeendelea kutuongoza na kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme ni muhimu kwa wananchi, Waheshimiwa Wabunge, watanzania na dunia kufahamu kwamba suala la demokrasia ni mchakato endelevu. Siyo suala ambalo litaisha tu hapa tukimaliza, hapana. Ni jambo ambalo linaendelea, kupitia Miswada hii nchi yetu itakuwa inapiga hatua nyingine katika

demokrasia ya vyama vingi nchini, hongera sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa zile *4R*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kimombo sisi tunasema kwamba, *democratization is never an ending process*. Tutaendelea hata kama tutahitimisha lakini bado mijadala inayoendelea kujadili suala hili tutaendelea kupokea maoni kama Serikali. Ndiyo maana hata mataifa makubwa nayo yanaendelea kuboresha demokrasia kila siku siyo hapa kwetu lakini hapa lazima *credibility* hii tuiweke kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuruhusu jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wenzangu Waheshimiwa Wabunge wenzangu walikuwa wanarejelea mambo kadha wa kadha. Wengine wakisema sisi wanasheria wengine sisi watu wa *political science* na mimi na-*declare interest*, mimi mtu wa *political science* na walimu wangu wamo humu ndani kina Dkt. Bashiru, kina Profesa Kitila, Profesa Palamagamba Kabudi, sisi tunasema kwamba kwenye mambo haya ya demokrasia na mambo ya madaraka lazima tuone namna nzuri ya kuyaweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yupo Mwanafalisafa anaitwa Hans Morgenthau, yeye aliandika kitabu kinaitwa *Politics Among Nations: The Struggle for Power and Peace*. Yeye anaamini katika mambo mbalimbali lakini anaamini katika suala la *peace through accommodation*. Kwa nini naisema hii, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ame-*accommodate* mambo mengi na makubwa ambayo Waheshimiwa Wabunge pia waliungana kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameweza ku-*accommodate* masuala yale ya kikosi kazi, kuona namna nchi yetu itaenda kwenye muelekeo ambao ni mzuri. Akaja na *4R*, hili halisemwi na watu wengi lakini nataka nikuhakikishie wenzangu wale wanaofanya mambo ya *emotional intelligence*, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameendelea kutajwa na wanafalsafa kuwa kati ya viongozi duniani

ambao wana *high emotional intelligence*. *Emotional intelligence* ni akili hisia, Mheshimiwa Rais, ameweza kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie ili nimpe muda Mheshimiwa Waziri wangu aweze kuja na hoja na majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nikiwa kama mtu mwenye ulemavu na mwanamke mambo yetu haya mengi yameguswa na yamezungumzwa katika miswada hii. Nataka niwatoe hofu wenzangu watu wenye ulemavu, miswada hii tumezingatia vizuri mambo ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye ule Muswada unaohusu uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Tutaenda kupitia Tume ya Taifa ya Uchaguzi hata kwenye ku-*print ballot papers* tutaweka *inclusion* ya watu wenye ulemavu kwa kutengeneza *accessible format* ya *braille* itakuwepo. Tutaendelea kuhimiza na kushauri vyombo vya habari kuendelea kutoa fursa ya kuweka wakalimani wa lugha za alama; watu wenye ulemavu kushirikishwa ndani ya michakato ya vyama vya siasa tumezingatia na tutakapokuja kutengeneza kanuni tutaendelea kuzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwa nimewapongeza na kuwashukuru watu wengi, nisisahau kumpongeza na kumshukuru Mwenyekiti wetu wa UWT Taifa, Mama Chatanda na Makamu wake kwa namna wanavyoendelea kuibeba ajenda ya wanawake katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa mimi nishukuru nimuachie nafasi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, aweze kutuhitimishia.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsanteni sana kwa kunisikiliza, tunawashukuru sana watanzania kwa maoni, Waheshimiwa Wabunge kwenye Kamati lakini na Bunge lako zima kwa namna ambavyo mmejadili Muswada huu na kutupa maoni na ushauri. Tumepokea na sisi Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama cha

Mapinduzi, chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tutaendelea kuyafanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, aje ahitimishe muswada. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Leo Bunge hili ninapomshukuru Mwenyezi Mungu, ninasikia fahari sana Bunge hili linaungana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuweka historia mpya ya mageuzi makubwa na kama tulivyomsikia kwenye zile *4R*. Mheshimiwa Rais, aliamua kuingiza falsafa ya *reform*, kwa hiyo, leo Bunge lako tukufu linaenda kuungana na Mheshimiwa Rais, kutengeneza mabadiliko makubwa ya mifumo ya demokrasia katika mfumo wa siasa za vyama vingi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kuingia katika historia hii. Jambo hili linaweza kuonekana ni dogo lakini ni jambo kubwa. Toka tumeanza mfumo wa vyama vingi vya kisiasa mwaka 1995 na chaguzi kuanza katika mifumo hiyo. Tume ya Uchaguzi ilipoundwa na kuanza kujiandaa kusimamia uchaguzi mwaka 1993 lakini mnajuwa sheria hizi pia zina-*address* masuala ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaweza tukaangalia miongo hiyo yote iliyopita hapo katikati na leo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amejenga dhamira ya dhati, utashi wa kisiasa na nia thabiti ya kufanya mageuzi haya. Hakika tunastahili kumpongeza na Bunge lako linastahili kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajaribu kupata maneno ya kuanzia lakini ninafikiri mimi ni mkristo na huwa wakati mwingine ninapenda pia kupitia maandiko matakatifu. Kitabu cha Wafalme, kimeeleza wafalme wengi ambao walipata kutawala huko nyuma kwa kuzingatia Biblia lakini nilivutiwa na Mfalme Suleiman, hekima yake na busara yake katika kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfalme Suleiman, siku moja katika utekelezaji wa majukumu yake, alikutana na mtihani mkubwa sana wa kutoa haki. Kurasimisha dhamira ya uhuru na kufanya maamuzi yenye hekima. Wanawake wawili walikwenda mbele yake wanagombania mtoto, mmoja aki-*claim* mwenzake ameiba mtoto wake baada ya yule ambaye alikuwa ni mtoto wa huyo kufariki kwa hiyo akamuegesha kwa mwenzake na mwenzake akisema hapana huyu ni wa kwangu. Kwa hiyo, huyo mtoto aliyekufa siyo wakwangu mimi ni wa huyo. Kwa hiyo, ilikuwa ni kesi kubwa ambayo ilihitaji hekima, maarifa, busara ya hali ya juu kuamuwa mtoto huyo ni wanani.

Mheshimiwa Spika, kipindi hicho hakuna *DNA,* kwa wale Wakristu wenzangu wanakumbuka nini alichokifanya Mfalme Suleiman, aliamua wanawake wale wamkamate yule mtoto na akaagiza uletwe upanga mkali sana. Mtoto yule aweze kukatwa vipande viwili ili kila mmoja apate haki ya kuchukua kipande kimoja na wale wanawake waondoke wakiwa wametendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yule alikuwa mzazi wa mtoto huyo mara moja alishikwa na hisia kali za uzazi. Sasa, ili mtoto wake awe salama aliamua mtoto yule abaki kwa yule mwanamke anayedai mtoto ni wa kwake ilihali hakuwa wa kwake. Ilimradi tu mtoto wake ambaye anajua amempata kwa shida na ana wajibu mkubwa wa kumtunza aendelee kuwa hai na kuwa salama. Hiyo ilikuwa ni hekima ya hali ya juu. Yule mama ambaye alisema mtoto awe salama na apewe mwanamke mwingine; Mfalme Suleiman aliamuru mtoto apewe

kwa huyo mwanamke aliyedhihirisha dhahiri kwamba mtoto huyo ni wa kwake yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka kusema nini? Mwenye dhamana kwa ulinzi wa Taifa letu kwa sasa ni Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mwenye dhamana ya ujenzi wa Uchumi na ustawi wa Watanzania kupitia mifumo ya demokrasia ambayo itasimamia mifumo ya vyama vingi vya kisiasa Tanzania ni Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mwenye dhamana ya kuhakikisha kwamba Taifa hili linakuwa na umoja wa kitaifa, mshikamano, amani na upendo ni Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hekima iliyotumika na Mfalme Sulemani, unaitazama sasa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika R zake nne. Anaonesha ustahimilivu wa hali ya juu kama ustahimilivu aliokuwa nao yule mama wakati kesi yake ikiamuliwa. Mheshimiwa Rais anaonesha hapa kwamba anataka maridhiano, mabadiliko na ujenzi wa Taifa hili jipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme, katika miaka 62 ya Uhuru ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, tumempata Rais tunaye muhitaji leo, kesho na siku zijazo, tunatakiwa kumuunga mkono. Mageuzi yote dunia yanaletwa na viongzoi wakuu. Lakini si suala la mageuzi tu, magezuzi hayo yanaweza kuwa chanya na mageuzi hayo yanaweza kuwa hasi. Leo Mheshimiwa Rais ameamua kutuletea mageuzi chanya kupitia kwenye Miswada hii. Ni fursa nyingine adhimu tumeipata. Mageuzi kama haya yalitaka kufanyika wakati Bunge la Katiba, lakini kwa bahati mbaya umoja wetu wa kitaifa uliondoka na Katiba mpya haikupatikana kwa sababu ya wachache kutokuamini katika mageuzi makubwa.

Mheshimiwa Spika, ninatoa wito kwa Watanzania wote kuungana na sauti za Waheshimiwa Wabunge zilizoinuka kwa siku hizi mbili kuunga mkono Miswada hii. Hii itawezesha kufanikiwa kuleta mageuzi haya makubwa ya mifumo ya kidemokrasia, na hasa katika mfumo wa siasa ya vyama vingi ili kuleta ustawi wa

Taifa, maendeleo ya kiuchumi, maendeleo ya mahusiano ya kidiplomasia, ujenzi wa huduma mbalimbali katika jamii, upunguzaji wa umaskini katika Taifa letu na mambo mengine kadha wa kadha ambayo hayawezi kufanyika vizuri kama demokrasia yetu itayumba yumba katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kukumbuka maneno ya hekima na busara yaliyosemwa na kiongozi wetu Hayati Nelson Mandela, alisema maneno yafuatayo ninaomba ninukuu; "Viongozi wa kweli lazima wawe tayari kujitolea yote katika maisha yao kwa ajili ya maendeleo na uhuru wa watu wao." Mwisho wa kunukuu

Mheshimiwa Spika, haya tunayashuhudia kwa Mheshimiwa Rais pamoja na kwako Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na Serikali nzima. Nimesikiliza mjadala wa Waheshimiwa Wabunge hakika wanatembea katika maneno haya ya busara ya Hayati Nelson Mandela. Wameamua kujitoa kwa ajili ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba ili kupata suluhu ndani ya nchi yetu, na bahati nzuri Rais tuliyenaye jina lake ni Suluhu vile vile. Ni lazima kila Mtanzania awe ni sehemu ya kila mchakato na mageuzi makubwa yanayoendelea katika Taifa hili. Ndiyo maana hapa ninasema pamoja na kuwapongeza viongozi, nimewapongeza Waheshimiwa Wabunge; lakini ninawapongeza viongozi wakuu wa Serikali ya Zanzibar, kuanzia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Makamu wa kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Mawaziri; na leo Waziri pacha mwenzangu, Mheshimiwa Hamza, yupo hapa ndani; na Wajumbe wote wa Baraza la Wakilishi. Hii ni kwa sababu katika jambo hili tumeshirikiana bega kwa bega na wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, ninawashukuru sana kwa kazi hii nzuri iliyotukuka ambayo imetufikisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaungana Mheshimiwa Naibu Waziri, siwezi kumaliza hitimisho hapa mbele leo kama sitamshukuru Mwenyekiti ya UWT Taifa Dada yetu Mary Chatanda na Makamu wake Zainabu Shomari; viongozi hawa ni majasiri. Tangu walipochaguliwa wameendelea kubeba ajenda za wanawake Kitaifa bila kubagua chama, dini, kabila wala jambo lingine lolote. Ninaomba huko waliko wapewe maua yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wanawake na ninawaona hata wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo wanapiga makofi, wanakubaliana na mimi, viongozi hao wamebeba ajenda zetu ambazo zinamkomboa mwanamke bila kujali tofauti zetu za aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, kama niliyosema kwamba leo tunaweka historia na jambo hili ni la kitaifa, ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. Kazi hii haikuwa nyepesi, ilikuwa ni kazi ngumu sana. kupitia maoni na kuyaoanisha na vifungu vyote tulivyovileta kama mapendekezo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikuhakikishie kwamba yapo maeneo mengi ambayo kupitia Miswada hii Serikali imekubaliana na Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria. Yale machache ambayo kwa namna moja ama nyingine tumetofautiana, wakati wa kupitisha vifungu tutapata nafasi ya muktadha mzima wa kuangalia tunafanya ni katika vifungu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelijadili sana lilikuwa ni kuhusu jina la Tume ya Uchaguzi kama ilivyoelezwa kwenye Muswada. Kumekuwa na hoja vingi. Muswada ulitaka kuendelea kuonesha kuwa Tume hii ni Tume huru tangu ilipotamkwa na Ibara ya 74(1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maoni ya wadau yamependekeza kuingiza neno huru kwenye jina la Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali haina tatizo na jambo hilo; na kubwa tulililoliangalia ni kupitia kifungu ama Ibara ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ibara ya 7 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara zote zimeeleza uhuru wa Tume yetu ya Uchaguzi. Ninakubaliana na Waheshimwa Wabunge kuingiza neno huru hakumaanishi kwamba Tume hii haikuwa huru huko nyuma. Tume hii imeshasimamia chaguzi sita; na chaguzi hizo zote ziliweza kuonesha ni namna gani Wabunge wa pande zote; chama tawala na vyama vya upinzani walipata fursa ya kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume huru itapimwa kwa namna ambayo Tume hiyo inapewa fedha za kuendesha uchaguzi, Tume itapimwa kwa majukumu yake yaliyoanishwa ili yatekelezwe kwa msingi wa Kikatiba. Tume itapimwa kwa namna Wajumbe wa Tume wanavyopatikana ili kuifanya Tume iweze kufanya kazi. Pia Tume itapimwa kwa uadilifu wa kazi zinazofanywa na Tume yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote ninayoyasema katika Muswada wa Sheria mpya ya Tume ya Uchaguzi mambo haya yote yamezingatiwa. Mfuko Mkuu wa Serikali utatumika kuendesha uchaguzi. Kifungu cha 9(1) kinaweka utaratibu mpya wa upatikanaji wa wajumbe wa Tume na hapa lazima niseme; Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya ujasiri mkubwa. Wote tunaelewa maana ya *power* (nguvu). Na kwa Mheshimiwa Rais nguvu ni kufanya maamuzi. Ana uwezo wa kusema ndiyo ama Hapana. Hiyo ndiyo power. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kwa kipindi hiki kifupi ameridhia; Katiba imempa majukumu ya uteuzi wa wajumbe lakini amesema utaratibu wa wajumbe kupatikana ufanywe na Kamati ya Usaili. Waheshimiwa Wabunge si jambo jepesi. Ninaomba Mheshimiwa Halima Mdee jambo hili uliunge mkono kwa nguvu yako yote. Kifungu hiki cha 9(1), kinaenda kuweka utaratibu mpya ambao haujawahi kupatikana tangu tumepata uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya *consultation* na Kamati tumekubaliana na tumeleta *proposal* yetu. Sisi kama Serikali tumefikiri tusiache wajumbe wa Tume kupitia kwenye usaili bali tuwe na mfumo mwingine wa kupendekeza Mwenyekiti wa Tume na Makamu Mwenyekiti wa Tume kwa Mheshimiwa Rais ili waweze kuteuliwa. Kamati inataka kuitumia Kamati ya Usaili, na sisi tumekuja na *opinion* ya kutumia viongozi wetu wakuu wa Mhimili wa Mahakama. Wote tumekubaliana Kamati ya Usaili iwasaili wajumbe wa Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako lipo katika sehemu ya kufanya maamuzi. Tutakaa na tutakubaliana hapa kwa mustakabali wa Taifa letu la Tanzania. Kwa hiyo niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kulizungumza jambo hilo, kuitazama Kamati ya Usaili, Kamati kuja na mapendekezo na sisi Serikali kuja na mapendekezo ili tuweze kukutana pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba inamtaka Mheshimiwa Rais kuchukua hatua za kuondoa mjumbe wa Tume, pale ambapo atakuwa labda kwa kuzingatia Katiba. Lakini, kwa kibali cha Bunge lako kutunga sheria kuona nini kifanyike, Serikali imekuja na mapendekezo. Kwamba, kadri itakavyoona inafaa Mheshimiwa Rais pia anaweza kuunda kamati ya uchunguzi ili hatimaye ije kumshauri kabla ya kumuondoa mjumbe wa Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana, eneo hili Waheshimiwa Wabunge walilichangia lakini halikuwa na mgogoro. Wengi walitaka kujua kama tunamlazimisha Mheshimiwa Rais, ina maana tunakiuka Katiba. Tumesema Mheshimiwa Rais, anaweza na halazimishwi. Kitendo cha Serikali kuja na Kifungu hiki cha Nane ni katika muktadha huo huo wa maridhiano pamoja na kuhakikisha kwamba Mheshimiwa Rais, ameridhia, Serikali imeridhia nguvu ile aliyonayo yakufanya maamuzi yeye mwenyewe basi bado kuna vyombo vingine vinaweza vikashiriki na kumshauri. Naomba tumpigie makofi Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo jingine lilikuwa ni kuhusu Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi kuwa Katibu wa Sekretarieti ya Kamati ya Usaili. Tumekuwa na mjadala mkubwa sana hasa kwa kuwasikiliza wadaupamoja na kuisikiliza Kamati yako. Haiwezekani; Kamati ilitushauri; Katibu wa Kamati ya Usaili ambaye ni Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi akafanya jukumu hilo. Kwenye Kifungu kingine cha 18, Mkurugenzi huyu atakuwa pia Katibu kwenye Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeridhiana na Kamati. Hapa sasa badala ya kuweka cheo na sifa ya Mkurugenzi tumeamua kuchukua jina lenye ujumuishi. Kwamba, mtu ambaye ana sifa za uandamizi, mtumishi Mwandamizi Serikalini ana uwezo wa kufanya kazi hiyo vizuri. Tunao watumishi waandamizi ambao wanatekeleza majukumu mazuri tu, kwa mfano Tume ya Mahakama na maeneo mengine; wana uwezo wa kufanya kazi hiyo. Tunachotaka Kamati ya Usaili iweze kutuletea Wajumbe wenye sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hii Kamati ya Usaili kifungu cha 27 cha Muswada kinasema kuwa Tume imepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni; ambazo hata ndani ya Bunge lako zitakuja kusomwa na zitapitiwa na Kamati yako Ndogo ya Sheria – kuona namna gani zoezi zima la usaili litakuwa huru na haki. Kwa hiyo, kwenye hilo hatuna shaka na tunaamini kabisa kwamba jambo hilo litatekelezwa vizuri. Nimesema hapa eneo lingine linaloipa sifa Tume ya Uchaguzi kuonekana inakuwa na uhuru wake wadau wengi walizungumzia eneo la watumishi wa kudumu wa Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria hii kupitia Serikali yetu tumeamua, kama ilivyo Sekretarieti ya Utumishi wa Bunge Tume nayo tumeianzishia Sekretarieti yake ya Utumishi kwenye Tume ya Uchaguzi. Hiyo sasa ni safari ya kuelekea kwenye mageuzi ya jumla. Safari hii kwa sababu ni ya muda mrefu mwendo wowote wa msafiri ataanza hatua kwa hatua; na akishapata nguvu na uwezo wa kukimbia na kufika kule anakotaka kufika. Kwa hiyo, ninaomba

niwaambie wadua kwamba jambo hilo pia tumelichukua na tumelishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda ninaomba niseme tu, majibu mengine yote tutaingiza kwenye maandishi na tutayaleta kwa Waheshimiwa Wabunge, itoshe tu kusema kwa mapendekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, katika kuweka utaratibu wake wa kufanya vikao, kusimamia uchaguzi wa Rais, uchaguzi wa Wabunge, uchaguzi wa Madiwani, kwa Muswada huu ni hatua kubwa sana ya *reform* kwenye demokrasia ya mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania. Kwa hiyo, ndugu zangu Wabunge na wananchi, ninaamini kabisa tutaendelea kuunga mkono jambo hilo na kuendelea kumpongeza Rais na Serikali yake.

Mheshimiwa Spika, nitapitia machache na mengi yatajionesha kwenye Jedwali wakati wa kupitisha vifungu. Nitapitia Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Muswada huu ambao unataraji kutunga hiyo Sheria mpya na hii niseme sheria hii hatukuwa nayo, Muswada huu unaenda kuunganisha Sheria mbili, Sheria Na. 343 iliyokuwa inatumika kwenye uchaguzi wa Rais na Wabunge na Sheria Na. 292 iliyokuwa inatumika kwenye uchaguzi wa Madiwani ikiwa *Local Government*.

Mheshimiwa Spika, Sheria hizi zote mbili zilikuwa zinaongozwa na muktadha wa Ibara ya 74 ambayo inazungumzia uchaguzi kwa ujumla wake na mawanda yake, kilichofanyika kwa Serikali na ninaomba niseme baada ya kupokea maoni ya kutosha kutoka kwenye kikosi kazi kilichofanya tathmini ya masuala ya demokrasia nchini, kikosi kazi ambacho kilijumuishwa na vyama vya siasa, hapa ni lazima ni mpongeze Msajili na Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, lakini nipongeze Baraza la Vyama na hasa vile vyama 19 vyenye usajili wa kudumu, wamefanya kazi kubwa sana kwa mashirikiano ya karibu na Tume yetu ya Uchaguzi kwa pande zote mbili *NEC* na *ZEC* na mnawaona viongozi wetu wenyeviti na watendaji wako hapa.

Mheshimiwa Spika, tunapounganisha mawanda ya sheria hizi mbili yako maeneo mapya mawili ambayo hayo ndiyo tunaweza kusema yalichukua mjadala mkubwa kwenye muktadha wa vifungu vya sheria hii. Jambo la kwanza ni kifungu cha 6(1) ambacho kilikuwa kinaweka mawanda na maudhui ya kuteua wasimamizi wasaidizi watakaoisaidia Tume.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano ya kutosha Serikali imeridhia kifungu hiki kifanyiwe maboresho, na lengo la kufanya maboresho kwenye kifungu hiki ni kuifanya Tume ya Uchaguzi iwe na uwanda mpana wa kuchagua ni nani anaweza kutumika katika usimamizi wa uchaguzi. Jambo hili ni la kihistoria. Tunaposema Tume inaweza kuwatumia watumishi wa umma waandamizi, ukipitia sheria ya utumishi wa umma na miongozo ndani ya Serikali inayoakisi utumishi wa umma, mawanda hayo yanauwezo wa kuwapata watumishi hao wa umma kwa vyeo vyao wenye sifa zitakazoweza kuisaidia Tume ya Uchaguzi kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, tungeomba sana watu wasitoe tafsiri tofauti, tuna Hukumu za Mahakama ambazo ziko *bounded,* Mahakama za Rufaa ambayo ilishatoa maelekezo ya kina wakati huo huko nyuma kuhusu kuwatumia Wakurugenzi. Sasa Sheria hii imeenda kuweka mawanda yakutosha kwa Tume bila kuathiri hukumu zilizoshughulikiwa na Mahakama zetu. Nadhani pia kifungu hicho tumekubaliana na Kamati na tutakutana nacho wakati wa kupitisha vifungu hivyo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ilikuwa ni mgombea wa kiti cha ubunge na udiwani kupita bila kupingwa. Tumeridhia, kwenye kikosi kazi jambo hili lilizungumzwa kwa kipaumbele, tumeridhia na tumeamua kwamba eneo hili nalo lifanyiwe kazi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, tumepokea kilio cha Wabunge wanawake na wanaume kuhusu suala la jinsia na hasa unyanyasaji wa jinsia. Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wabunghe wote waliochangia, mimi kama mwanamke nimewakilishwa na Wabunge

wote wanaume na wanawake. Tutakapofika kwenye vifungu tutashauriana Bunge hili ni nini kifanyike kwa sababu unyanyasaji wa kijinsia hata wanaume nao wananyanyasika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huko tunakokwenda ninaanza kuhofu wanaume watanyanyasika zaidi, kwa hiyo tunatakiwa kutengeneza mfumo wa kudumu utakaosaidia kuondoa unyanyasaji wa kijinsia kwa wanaume na wanawake na kufanya mawanda ya uchaguzi kuwa haki, kutoa fursa na kuhakikisha kwamba makosa yanayotokana na uchaguzi yanayoweza kupelekea unyanyasaji kuendelea yaweze kukomeshwa.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Serikali kazi hiyo pia tulikwishaianza na tungekuwa na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii nadhani leo angepata nafasi ya kueleza. Serikali imekwisha kuamua kuleta sheria ambayo itasimamia masuala hayo yote yanayohusu unyanyasaji wa kijinsia mahali pote. Iwe ni kwenye uchaguzi, iwe ni kwenye ndoa, kila eneo kutakuwa na kifungu chake cha kusimamia jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo imefika mahala pazuri, Wizara ya Maendeleo ya Jamii imeshapeleka Muswada huo kwenye Timu ya Wataalam *(MTC)* na sasa tunasubiri waweze kuisogeza sheria hiyo na Bunge lako tukufu itakapofika muda na tungependa jambo hili lifanyike kabla ya uchaguzi mkuu ili kutengeneza mazingira yawe sawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa, dakika tatu malizia kwa sababu kengele ya pili imeshagonga.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, tutapata fursa ya kushauriana na Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kusema mimi ni mwanamke, mama wa watoto na kwa kweli hasa kwa kuwa Rais ni mwanamke, lazima kwanza tumlinde yeye na wanawake wote lakini na wanaume katika Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo jingine kwenye Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa. Tumesikia Wabunge wengi wakizungumza eneo hilo kama ni eneo muhimu sana la kuangalia kwa jicho la kijinsia. Ninawashukuru wale waliokwisha ipongeza Serikali kwa sababu tumechokoza kwa kuifanya Sheria ya Vyama vya Siasa ianze kutizama mifumo yote kwa jicho la jinsia ndani ya vyama vya siasa, tutakapopata muda wa kufanya mapitio nadhani tunaweza pia kupata nafasi ya kusema vizuri katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Gharama za Uchaguzi inayofanyiwa maboresho inahusu masuala ya kiutawala zaidi, hayo kwa kweli kwetu sisi naona Waheshimiwa Wabunge hawakuyagusa sana.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa nukuu ya Hayati Baba wa Taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema, nitamnukuu; "Afrika inabadilika kwa sababu uongozi wa Afrika unabadilika na kusonga mbele, inaanza kubadilika na kupaswa kuhimiza mambo ya kutosha ya maendeleo katika Bara zima lakini kwa kuzingatia utambuzi zaidi, kuyabainisha zaidi mambo ya msingi, kuyategemeza katika mataifa, kuyaunganisha kwa sauti moja na mwisho wa siku kufanya hayo yote kwa ngazi ya pamoja kwenye Taifa na ngazi zote za chini."

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea sasa yalikuwa ni maono ya Baba wa Taifa, tukitoka kwenye fikra, sasa hayo tunayaona ndani ya Nchi yetu ya Tanzania, Hongera sana Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema Baba wa Taifa alikuja na Falsafa ya Mwenge wa Uhuru katika kusukuma ajenda ya uhuru na maendeleo. Leo Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja na falsafa ya *4R*. Waheshimiwa Wabunge, naomba niwahakikishie tutafika salama na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan atatufikisha salama.

Mheshimiwa Spika, kwa kujali utaratibu wa kikanuni na muda nilionao naomba niseme majibu yote tutayaleta kwa maandishi. Naomba nikushukuru sana, nirudie kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi hii nzito tuliyoifanya lakini kwa pamoja tunaweka historia ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ili taarifa zetu zikae sawa maana hoja zetu zilitajwa tatu hapa, ngoja tupitishe hoja moja moja. Hoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023. Haya toa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja sasa Bunge lako liweze kujadili Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tunaendelea na Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu sasa naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023, uweze kujadiliwa na kupitishwa na Bunge lako tukufu, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono tunaendelea na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws, Amendment Bill, 2023)*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja Muswada wa tatu wa Mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa Nchini wa Mwaka 2023, uweze kujadiliwa na kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na kwa hivyo hoja zetu zote zimeungwa mkono na tutaendelea na utaratibu wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa ujumbe hapa kwamba yupo Mhandisi Robert Kitundu ambaye ni Katibu Mkuu wa KKKT-Tanzania, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na utaratibu wetu, Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Kamati ya Bunge Zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023**

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunaitikia ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge ziweze kuwa sawa sawa.
Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 3 kina marekebisho ya Profesa Kabudi. Mheshimiwa Profesa Kabudi, hayupo. Nani ameyapitia hayo marekebisho ya Mheshimiwa Profesa? Haya wacha tuyatazame hapa mbele kwanza, nani anataka kumsaidia Profesa? Hakuna aliyepitia? Haya ngoja niyapitie hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye kifungu cha 3 ambacho kinahusu tafsiri, marekebisho ya Profesa Kabudi, siyo utaratibu wa kawaida lakini kwa sababu tuko kwenye utungaji wa sheria lazima tutazame pengine kuna jambo ambalo tutaweza kujifunza kutoka hapa.

Mheshimiwa Profesa Kabudi kifungu cha 3 anapendekeza kufuta tafsiri ya neno mtazamaji na kuweka tafsiri mpya kama ifuatavyo; neno mtazamaji limetafsiriwa na Muswada kwamba maana yake ni mtazamaji wa ndani au wa kimataifa aliyesajiliwa na

Tume. Profesa Kabudi anasema lifutwe hilo neno na kuweka tafsiri mpya kama ifuatavyo; mwangalizi, maana yake ni mwangalizi wa ndani au wa kimataifa aliyesajiliwa na Tume. Hayo, ndiyo mapendekezo ya Mheshimiwa Profesa Kabudi.

Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sifa ambazo nchi yetu imeendelea kupata sasa hivi ni kukua kwa Lugha ya Kiswahili na imekuwa ikitoholewa kwa namna moja au nyingine kila siku, kwa hiyo kwa kuwa Profesa Kabudi na timu yetu ya utohoaji tumeliangalia neno hilo, hatuna matatizo nalo. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo. Haya maneno mtazamaji kuna mahali ambapo yanatokeza kwenye muswada huu ambayo tutakuja kurejea kwenye Ibara ya 104(1), (1) ambako huko kuna neno mtazamaji ambako itabidi liwekwe neno mwangalizi maadamu tumekubali kwenye tafsiri, kwa hiyo tutakuwa tumefuta neno "Mtazamaji" pale linapotokea, liwe neno "Mwangalizi" lakini tutalirejea tutakapofika hiki Kifungu. Katibu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia Jedwali la Marekebisho la Serikali, Kamati inakubaliana na Marekebisho ya Serikali, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc*. – KATIBU WA BUNGE:**

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizitajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara ilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 23, Kamati imepitia marekebisho yaliyoletwa na Serikali, yanafanana na yale ambayo Kamati ilikusudia yafanyike. Kwa hiyo, Kamati inaridhia, ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 24
Ibara ya 25

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 28

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yaliyokusudiwa na Kamati yamezingatiwa na Serikali, ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 29 na marekebisho yaliyokusudiwa na Kamati yamezingatiwa na Serikali. Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 30

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yaliyokusudiwa na Kamati yamezingatiwa kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali. Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima*

*pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 31
Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 33(1) kilikusudia kuongeza neno "wa jinsia zote" baada ya neno "wadhamini" kwa malengo kwamba mgombea yeyote anapodhaminiwa kwa nafasi yoyote ya Urais, Ubunge na Udiwani, ahakikishe kwamba anadhaminiwa na watu wa jinsi zote, kwa maana ya wanaume na wanawake. Mapendekezo hayo, Serikali haijazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashawishika kuliomba Bunge lako Tukufu liunge mkono mapendekezo ya Kamati ya kuongeza neno "wa jinsia zote." *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna shida na jinsia zote, lakini tulijaribu kuzungumza na vyama mbalimbali vya siasa ambao wao ndio wamekuwa mara nyingi wakishughulika na jambo hili la udhamini. Kuna baadhi ya vyama walituambia, inapofika wakati wa uchaguzi fitina ndiyo jambo mojawapo, kuwahi, *timing* na vitu vingine ndivyo vinavyoendelea kwenye uwanda wa uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakatushauri Serikalini, sisi hatuna shida, lakini Bunge linaweza kufanya maamuzi endapo itatokea chama fulani kikajaribu kutengeneza muktadha wa jinsi moja isitokee kwenye udhamini huu; na suala la udhamini ni suala ambalo linatakiwa lizingatiwe sana katika kuhakikisha *qualification* ya mgombea. Tunaweza tukawa tumetengeneza muktadha ambao unaweza ukaleta taabu kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunajaribu kukisoma kifungu hiki tukaona kwamba kwa Serikali tunaweza kuendelea nacho kwa kuzingatia mabadiliko ya Kamati, ila tuna kila sababu ya kueleza wale ambao ndio wamekuwa wakishughulika na jambo hili huko uwandani, na inaweza ikatengenezewa mazingira ambayo kidogo yakaleta shida wakati wa harakati za ugombeaji.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati, hapa kwenye haya mabadiliko mlitaka kushughulika na tatizo gani?

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya makusudi makubwa ya kuboresha sheria zetu ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na *inclusion* kwa maana ya dhana jumuishi. Tulikusudia kutoa fursa kwa kila mgombea kudhaminiwa na Watanzania ambao wana jinsi mbili tofautil, lakini siyo idadi. Maana yake katika watu 10 wanaokudhamini, walau awepo mwanaume mmoja au mwanamke mmoja bila kujali idadi. Hayo ndiyo makusudi yetu. Sasa kama hilo lina shida, mimi binafsi siamini kama lina tatizo kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesema iko tayari kupokea mapendekezo ya Kamati katika eneo hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sijui kama mmemsikiliza Waziri, mpaka mwisho. Ametoa kwa mkono mmoja akachukua kwa mkono mwingine. Kwa sasa hivi tunalo tatizo la mgombea wa Urais kwamba amewahi kudhaminiwa na jinsi moja? Kwa sasa hivi ni tatizo? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

**MWENYEKITI:** Kama siyo tatizo, tunatungia sheria kitu gani kama tatizo halipo? Kwa sababu lazima kuwe na tatizo. Yaani kwamba kuna mtu atajitokeza halafu awatafute watu ambao wanamuunga mkono yeye tu halafu wengine awaache. Je, tumeshawahi kuwa na hilo tatizo kwenye jamii yetu? Kama haijawahi, basi hatuna tatizo japokuwa nia ilikuwa ni kuweka mazingira ambayo huko baadaye hata akijitafuta; lakini sasa tusitengeneze sheria ambayo haina kitu inachoenda kukifanyia kazi. Lazima kuwe na tatizo ambalo tunataka kushughulika nalo.

Tukianza kufikiri huko baadaye, ndiyo maana Bunge lipo, linaishi miaka yote. Likitokea, tutashughulika nalo. Kwa hiyo, kwa sasa kwa sababu siyo tatizo na wote mnakiri kwamba kwa sasa siyo tatizo, haya kuna ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa *Engineer* Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo hili limeletwa hasa na yale makundi maalum kwa misingi kwamba siyo tu wanawake au wanaume, kuna masuala pia ya kuwahusisha hawa watu wenye uhitaji maalum, kwa mfano, wenye ulemavu na vitu kama hivyo. Msingi ni kwamba, huyu kiongozi ambaye anadhaminiwa, ombi ni kwamba aweze kuwa na jicho la kujua waliomdhamini ni watu wa makundi ya aina mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, nilikuwa nafikiria labda kwamba, kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri aliyoyazungumza, pengine labda tu tuliondoe neno "zote" badala yake iwe ni kuhusisha, yaani iwe *inclusion*, ihusishe mawanda mbalimbali ya jinsia. Yaani jinsia, tusimalizie "zote" ila iwe "jinsia", kwamba jinsia inaeleweka ni wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu, watu wa kila aina, wote na makundi yote, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keisha, niliona umesimama.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi, hili jambo nililiwaza mimi na kulitafakari kwa kina. Niliona kwamba, ili kuwa kiongozi mzuri ni yule anayetambua uwakilishi wa watu wote katika eneo lake. Kama jambo ni hilo la kufahamu uwakilishi wa watu wote katika eneo lake, kwa mfano kwa Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge, watambue kwamba kuna ofisi za watu wenye ulemavu ambapo katika wale wadhamini mmojawapo akatokea kwamba ni mtu mwenye ulemavu, tayati ina-*sense* kwenye akili yake kwamba, nina hili kundi ninapaswa kulishughulikia na kulifanyia kazi kwa usahihi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo ilikuwa hoja yangu. Naomba nitoe hoja.

**MWENYEKITI:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge, tuna miswada mingi hapa na ninawaona wengi mmesimama. Ehe, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tunakubaliana kwenye ufafanuzi, lakini naomba nitoe uzoefu. Mwaka mmoja nimewahi kutafuta wadhamini wa Mgombea Urais, lakini tulipofika kwenye eneo fulani, mkoa fulani, kwenye ile idadi ambayo tunataka, wanawake, wanaume, na makundi yote tunatamani yamdhamini mgombea wa Urais, lakini inatokea kundi lingine pengine halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe umetuongoza vizuri. Tunasema Mtanzania yeyote mwenye kitambulisho cha kupiga kura, anaweza kumdhamini Mgombea wa Urais. Kwa hiyo, pengine michakato yetu ndani ya vyama iwahamasishe wanachama wake kwamba, wakati wa kudhamini wagombea, jamani jitokezeni ili mkamdhamini huyu mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo tulifika, Mgombea wetu wa Urais tunayemdhamini, waliokuja kumdhamini ilikuwa ni wanawake. Wanawake nawapongeza sana. Ilikuwa ni wanawake wenzangu, lakini pia na wenzake aliosoma nao shule ya msingi. Ilibidi tusubiri mpaka muda kama wa saa moja au saa moja na nusu ili tuweze kujaza ile idadi ya Mgombea wa nafasi ya Urais. Kwa hiyo, haya mambo wote tunakubaliana, lakini lazima tuyaangalie kwenye mawanda yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetuongoza vizuri, nadhani tusimame pale ulipotuongoza na msimamo wetu upande wa Serikali, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ulisimama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama kukumbusha tu kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 13(2) Bunge hili ambalo kwa mujibu wa Ibara ya 63, kazi yake moja ni kutunga sheria, linazuia kutunga sheria yenye kubagua. Sasa haki za kushiriki katika mambo kama uchaguzi zilizo kwenye Ibara ya 21 na 22, haziendi kinyume na kifungu hiki kilivyo. Kifungu kilivyowasilishwa kwenye muswada huu, maana yake ndiyo ambayo ni matakwa ya Katiba, lakini pia, hakitoi fursa ya mtu yeyote aliyepitia mchakato wa kuandikishwa na kuwa na zile sifa za kupiga kura au kudhamini kuweza ku-*fit in.* Mifano dhahiri ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua yapo maeneo ambayo ni ya wachimbaji kwenye migodi, idadi kubwa ni ya jinsi ipi? Tunavyo viziwa vya uvuvi, kwa hiyo, ndiyo maana uliuliza vizuri lile swali lako kwamba tumekutana na changamoto ipi ya watu wanaobaguliwa kiasi cha kuja na mapendekezo hayo ya mabadiliko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mujibu wa Ibara ya 33 kama ilivyowasilishwa, iko kwa mujibu wa Katiba. Vilevile, haioneshi kubagua kundi lolote au kulinyima fursa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya. Mwenye hoja. Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maelekezo yako. Kwa sababu utungaji wa sheria ni mchakato na Bunge hili lipo, wakati ukifika hoja hii inaweza kuwa na mashiko. Kwa sasa nakubaliana na Ibara ya 33. Sasa kwa vile zipo Ibara kadhaa ambazo zinagusa eneo hilo, nikuokolee muda kwamba Ibara ya 33, Ibara ya 34 na marekebisho yaliyoletwa kwa Ibara ya 50 na Ibara ya 62; kwa vile maudhui yake yanafanana basi ziondolewe Mezani kwako, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hivyo vifungu vingine sijavipitia, lakini labda Mwenyekiti wa Kamati atakuwa ameshavipitia kabla ili tujue. Kwa sababu sote nia yetu ni njema, lakini katika hiyo nia njema tusivute kamba nyuma, kwa sababu upo uwezekano kabisa wa watu wa eneo fulani wakawa hawataki. Kama wanavyosema, kuna watu wanakimbia kumdhamini mgombea. Sasa haya tunaongelea uchaguzi wa nchi, lakini hata kwenye vyama kuna watu wanakimbia. Wanawaficha watu wao huko na mambo kama hayo. Sasa tusije tukaleta jambo jipya ambalo kwa sasa hatuna tatizo, tukatengeneza tatizo kwa kifungu hiki. *(Makofi)*

Vifungu vingine sijavipitia kuona muktadha wake unataka nini Mwenyekiti. Ila kwa hapa nadhani twende kwa sura hiyo. Umesema Ibara ya 33. Ibara ya 34; ngoja tuone ulitaka kiingie wapi? Ngoja tuhoji hii 33. Tutaenda taratibu tu. Lazima tutunge sheria ambayo itatusaidia kututoa hapa kutusogeza sehemu nyingine.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

**MWENYEKITI:** Sasa ngoja. Kwa sababu Mwenyekiti, ameamua kunirahisishia muda, hebu nifungulie hayo marekebisho yao yalikuwa yanaingizwa wapi?

Mwenyekiti, hivi vifungu pamoja na kwamba vinaelezea hayo maneno, lakini havifanani. Kwa hiyo, upo uwezekano kwamba kuna mahali haya maneno yanapaswa kuingia. Kwa hiyo, nikupe nafasi uwasilishe halafu tutazame. Kwa mfano, hili la 34(3)(a), mlikuwa mnasema tuweke maneno "jina…

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inahusu uteuzi wa Mgombea wa Kiti cha Urais, pia, itahusu nafasi nyingine za Ubunge na Udiwani kwa vifungu vinavyofuata. Ilikusudiwa ile fomu ya uteuzi, itoe fursa ya kupata taarifa za mgombea kuhusu jinsi yake na hali yake ya ulemavu. Tulidhani hizo ni taarifa muhimu ambazo zitamtambulisha mgombea kwa Afisa Uchaguzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya. Kwa sababu sote ndiyo tuko kwenye kujifunza, kuna mengine ya kujifunza na mengine ndiyo tunaenda hivyo. Hizi sifa tukiziongeza ama haya maneno tukiyaongeza sisi tunavyofikiri kama Bunge, zinamsaidia mgombea kwa kueleza kwamba huyu ni mwanamke, huyu ni mwanaume, huyu ni mtu mwenye ulemavu ama zinampunguzia chochote alichopaswa kukipata? Sisi tunavyoona, zinamsaidia ama zinampunguzia? Ndiyo tujadili hapa. Kama tunaona zinamsaidia tuziweke, kama tunaona zinampa uhasi, sijui uhasi! Siyo uasi, uhasi; yaani kwa maana ya lile neno hasi. Yaani zinampa hasi. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki Serikali haikuwa na tatizo kwa marekebisho yaliyoletwa na Kamati. Kwa sababu tuliona, kwa mgombea Urais fomu zake zitakapoonyesha kama yeye ni mtu mwenye ulemavu ama ni wa jinsi ya KE ama wa jinsi ya ME, kwenye mifumo ya uchaguzi na hasa kwenye ngazi hiyo ya juu, tunafahamu kuna maandalizi ya walinzi binafsi na maandalizi ya

wahudumu watakaomsaidia mgombea. Sasa kama tutakuwa tumeweka hizo jinsi za kuonesha zilivyo, kwenye nafasi ya Urais unaona kabisa uhitaji wake ambao ni mkubwa ili mgombea huyu asaidiwe kwa kuzingatia hali aliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaweza tukaitafsiri hata kwa wagombea Ubunge kama Mgombea Ubunge, ni mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa anahitaji msaada wa ziada zaidi. Lakini hata kwenye ugombea Udiwani. Kwa hiyo, kwa Serikali tuliona vifungu hivi vingeweza kutusaidia kufanya *management* ya wagombea wakati ule wa uchaguzi na hatukuwa na shida nayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ukiwa bado umesimama kuna hayo marekebisho yanayopendekezwa kwenye (a), kuna hayo marekebisho yanapendekezwa kwenye (d), majina na anuani za wadhamini nayo yaingie haya maneno ya jinsi, hali ya ulemavu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki sasa ndicho alichokisema Mwenyekiti kwa eneo hilo hakutokuwa na muktadha wa kuingiza lakini kwenye kile cha kwanza kutakuwa na muktadha wa kuyaingiza.

**MWENYEKITI:** Kazi tunayo, *AG* hebu tupitie wote hapo. Fomu za uteuzi zitawasilishwa zikiwa na maelezo yafuatayo; Jina na anuani ya Mgombea kwa sasa, Jina na anuani ya Mgombea ambaye atakuwa ni Mgombea mwenza, tamko la Mgombea na mambo kama hayo. Halafu mapendekezo ya Kamati kuongeza maneno Jinsi na hali. Kwa hiyo fomu za uteuzi zitawasilishwa zikiwa na maelezo yafuatayo; Jina, Jinsi, Hali ya Ulemavu ya Mgombea na Anuani ya Mgombea. Halafu tunaenda kwenye (d); Majina na Anuani za Wadhamini ambao sasa mwanzo yalikuwa yaongezwe kati ya neno Majina na Jinsi, Hali ya Ulemavu na Anuani za Wadhamini, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu yangekuwa kwamba muswada kama ulivyo uko sahihi. Kwa sababu mambo mengine yanakuwa *technique* yakiwa na *Intraparty nomination stages*.

**MWENYEKITI:** Sasa hapo nilikuwa nataka ushauri wa kitaalam, maana tusijekuwa tumeweka hapa kinaonekana kitu kinaelea. Kwa maana hapa ni jina na anuani na huku ni majina na anuani, kwa nini tunataka sehemu moja na sehemu nyingine tunataka tusiweke? Haya nataka kuamini hapa mbele kwamba kwa sababu Serikali imepitia yale marekebisho na hiki kifungu Kamati ilipata nafasi ya kujadili wameleta hapa mapendekezo yao.

Kifungu cha 34(3)(a) jina kwa muktadha aliyousema Mheshimiwa Waziri, kwamba tukiweka hapa itawasaidia kupanga mahitaji ya wale wagombea. Na hapa mbele majina na anuani za wadhamini pabaki hivyo maana yake kifungu hiki cha 34 yatachukuliwa mapendekezo ya sehemu ya kwanza pekee ya mapendekezo ya Kamati, halafu sehemu ya pili tutakuwa tunayaondoa, tumeelewana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 34 pamoja na marekebisho ya Kamati kwenye kifungu kidogo cha 3(a), kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41

Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 50, kina marekebisho ya Kamati. Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kifungu hiki cha 50, maudhui yake yanafanana na kifungu cha 34 kwa sehemu ya (a), kwa hiyo na nyinyi Serikali kama imeridhia kwa sehemu hiyo ya (a), pia itaridhia kwa sehemu hii ya 50(a), kwa maana kuwatambua hawa Wagombea kama wana hali za Wagombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, (b) ilikuwa inahusu wadhamini nadhani kwa maana ya wadhamini tumeshatolea maamuzi ninaamini basi itabaki sehemu hiyo ya (a), ahsante.

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 50 pamoja na marekebisho ya Kamati ambayo yako kwenye kifungu kidogo cha 3, fasili ya (a), kinaafikiwa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja marekebisho yake)*

Ibara ya 51

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 51 Mheshimiwa Ng'wasi Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kifungu cha 51 kinataka wakati wakurudisha fomu ya uteuzi wa Mbunge, Mgombea aweke dhamana kwa Msimamizi wa Uchaguzi kwa kiasi cha fedha kitakachoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba kifungu hiki kinaweza kikawa kina athari ya kuleta *discrimination* ambayo ni kinyume na *sub article* 13(2) ya Katiba ambayo inasema "Taasisi yoyote au mamlaka yoyote isitunge sheria ambayo inaweza ikawa na asili ya kiubaguzi" kifungu hiki kinataka mtu akiwa anagombea Ubunge akirudisha fomu yake ya uteuzi arudishe na fedha. Fedha hizi ziweze kutaifishwa na Serikali pale ambapo hatofikisha kura kwa wingi wa 1/10 ya kura zote zilizopigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashawishika kusema kifungu hiki kinaweza kuwa kinyume na Ibara ya 21 ya Katiba ambayo inasema "Kila mtu ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa ikiwa amekidhi vigezo vya Katiba". Pia inaweza kuwa kifungu hiki kipo kinyume na Ibara ya 67 ambayo inatoa vigezo vya mtu kuchaguliwa kuwa Mbunge, ambayo imetoa kigezo cha umri, utaifa na chama. Sasa tukiongeza tena kigezo cha kuweka fedha naamini tunaweza kuwa tunaenda kinyume na vifungu hivi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaribu kuangalia kifungu hiki kimekuwepo kwenye Sheria ya Uchaguzi muda wote toka Tume ilipoanza kazi ya kusimamia uchaguzi, kwenye sheria yetu ya uchaguzi wakati wa kugombea na nadhani Waheshimiwa tunafahamu kwamba kila Mgombea amepitia kifungu hiki. Ukiacha masuala ya haki za binadamu kama yalivyoelezwa na nadhani Mheshimiwa *AG*, anaweza akanisaidia lakini maudhui ya jumla ya

kifungu hiki ilikuwa kwa kweli kupima *seriousness* ya kila Mgombe pale anapokusudia kuchukua fomu na kwenda kugombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri wa fedha hizi kwa mujibu wa sheria zinatakiwa pale Mgombea anapokuwa ameshinda arudishiwe kwa sababu zinawekwa kama dhamana. Tunachelea kukiondoa kifungu hiki unaweza ukafungua uwanda wa mtu tu kuamua na kwenda na wakati mwingine hakuna ile nia thabiti na vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tulikuwa nacho katika Sheria za Uchaguzi zote zilizopita kwa hiyo sisi kama Serikali, kwa kweli tulikuwa tunafikiri kila Mgombea ana dhamana ya kuweka *commitment* ya *seriousness* yake katika kuamua kwenda kugombea kuliko kukiacha wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote tu tunaweza tukakuta utitiri wa watu wanakwenda wanachukua fomu lakini ile *seriousness* haipo. Kwa hiyo, kwa tafsiri ya sheria tulizonazo na sheria nyingine pia zimeweka vifungu vya dhamana sasa hatuoni kama sheria hii ikiweka kifungu cha dhamana pekee yake ndiyo kinakiuka misingi ya Kikatiba ya Haki za Binadamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, umeleta hoja ya Kikatiba umetaja kifungu gani na kifungu gani?

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetaja Ibara ya 13(2), Ibara ya 21 na Ibara ya 67.

**MWENYEKITI:** Haya, Serikali imeshatoa maelezo unasemaje juu ya maelezo hayo?

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nachelea pia na mimi kusema kwamba tukiacha kifungu hiki ambacho ndiyo kilikuwepo. Lakini maadamu tuko katika utungaji mpya wa sheria sio

mbaya kukiangalia upya, maudhui yake yanaendana sambamba na kifungu cha 63. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari sheria hii inataka mtu akiwa anakuja kugombea, akichukua fomu ya uteuzi wakati anairudisha, arudishe fomu ikiwa na wadhamini. Maana yake mimi nadhani hii ni *seriousness* tosha na idadi ya wadhamini imekwishawekwa kwenye sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna makundi maalum tunaweza tukayatenga kijamii tukiweka vigezo hivi vya kifedha, kuna watu ambao wanataka kutumia haki zao za kuomba kuchaguliwa lakini kwenda kuchagua. Tukiweka kigezo cha fedha kuna makundi maalum hasa ya vijana ambayo tunaweza tukayatenga kwenye mchakato huu, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono. Akishatoa hoja huwa unasimama, sio mnaanza kuota taratibu kama uyoga hivi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha wa kifungu kilivyo hakikiuki moja wapo ya ibara za Katiba, ambazo mleta hoja anaziweka. Kwa sababu kimelenga kuupa mchakato wa kiuchaguzi ambao una muda wake maalum usije kuingiliwa na watu ambao hawana nia thabiti na ndiyo mantiki ya kifungu kidogo cha pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya dhamana ni sharti jingine kama lile la mtu kuwa na wadhamini au takwa la dhamana hata ingefika wakati wa kufungulia shauri. Hawezi akasema tu kwamba kwa sababu ni haki yangu kushiriki kwenye mambo ya *governance* ya nchi sitalipa ada za Kimahakama. Kwa hiyo, ningependa kutofautisha na hoja ambayo Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, amewasilisha mambo ya kiutaratibu yanaeleweka wala hayaendi kukiuka.

**MWENYEKITI:** Sawa, kwanza hoja ya vifungu vingi vimekuwepo ambavyo vinafanyiwa marekebisho. Lakini hii hoja ya dhamana kila Mgombea kwa sasa si lazima awe amepitishwa huko na chama chake, ndiyo Katiba inavyosema? *(Makofi)*

**WAJUMBE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sasa sina uhakika kama hiki kigezo kimoja tu ndicho kinampima huyu lakini changamoto ninayoiona kwa upande wa kifungu cha 35 ambacho tumeshapitisha kinahusu pia dhamana kwa mgombea wa Urais, sasa hapa ni cha Mbunge, na kule tumeshapita.

Sasa tunataka dhamana awe nayo Rais, pekee halafu hawa wengine wawe hawana ama? Kwa sababu kama tumepitisha 35 na hii sheria inahusu Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, ndiyo maana Mwenyekiti alisema mwanzo kama ni maboresho tunafanya kwa wote hatufanyi kwa mmoja halafu kwa wengine tukafanya tofauti. Samahani kuna mtu anazungumza simsikii sijui anaongea nini? Yuko wapi anayezungumza?

Mheshimiwa Sophia, unasemaje?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kamani, yeye ameliona kwa hiyo kwenye suala la Rais, labda kuna mtu aliona haina haja kuwa Rais anastahili kuwa na hizo dhamana; lakini Mheshimiwa Kamani, amezungumzia kwa *level* ya Ubunge, sasa ninaomba tupate nafasi au apatiwe nafasi tuweze kujadili tuone tunafanyaje, tunaweza tukaipitisha pia lakini lazima tutoe maoni.

**MWENYEKITI:** Kutoa maoni sasa ndiyo tumejiwekea utaratibu, hamkusimama kuunga mkono hoja. Mmesimama hapo watu wawili akiwa na yeye amesimama ndiyo wakaanza wengine taratibu, nadhani tulishaelezana kanuni zinasemaje Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, kuhusu hoja hamkuunga mkono kwa hiyo, siwezi kurudia sio utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maana ya kuvunjwa Katiba ama kumnyima mtu haki, haki inatolewa na wajibu kwa hiyo haki inaenda na wajibu.

Sasa hii ni sehemu ya wajibu anayopewa huyu mtafuta hii haki ya kupigiwa kura. Kwa hivyo, hili la kwamba pengine linamzuia, linaleta ubaguzi ama namna fulani hivi kwa namna alivyolieleza Mheshimiwa Kamani, hapana hamna Kifungu cha Katiba kinachovunjwa kwa sheria kutungwa kwa sura hii. Ndiyo maana tumesema na hayo mengine kwa sababu ukisema apitie kwenye chama pia itakuwa ni kuvunjwa kwa sababu kuna mtu hana chama kwa hiyo, mazingira lazima yapimwe kwa sura hiyo.

Kwa hiyo, unawekewa haya masharti ili kulifanya hili zoezi lisiende ndivyo sivyo kwa hiyo nilikuwa naipitia hapa Katiba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ng'wasi, usiwe na wasiwasi kifungu hiki kitakuwa hakijavunja Katiba, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 51 kinaafikiwa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 57

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 57 Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia marekebisho yaliyoletwa na Serikali yanakidhi matarajio na matakwa ya Kamati, ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 58
Ibara ya 59

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 60

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 60, Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Katika kifungu hiki kinaonyesha masharti ya mtu ambaye hataruhusiwa kugombea kwa upande wa Madiwani, hatoruhusiwa kugombea ikiwa atakuwa ana makosa yafuatayo. Sasa mimi nataka kuongeza kifungu cha 60(1)(g) kuwa kama mtu huyo atakuwa ametiwa hatiani kwa kosa la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia ndani ya kipindi cha miaka mitano kabla ya uchaguzi basi mtu huyo asiruhusiwe kugombea nafasi ya Udiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitaridhika na majibu ya Serikali ningependa kutoa hoja ili Wabunge wenzangu waweze kutoa hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 60 hili ni eneo la uendeshaji wa uchaguzi na inatakiwa vifungu hivi vifanane katika maeneo yote. Sasa tukikiweka kwenye eneo hili pekee yake na huku tulikotoka hatujakiweka kifungu hiki na tunaongozwa pia na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninafikiri tutafute namna nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema tunadhani, tunafikiri tuje sasa na Sheria kwa maelezo ya Serikali niliyoyapata ndani ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto ambayo itaweza kuyatengeneza makosa yote yanayohusu unyanyasaji wa kijinsia katika sekta hizo mbalimbali. Ili kuweka adhabu na kuweza kuyashughulikia kwa muktadha unaotakiwa bila kuathiriwa na sheria nyingine kama *penal codes* na sheria nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kadiri tunavyoendelea, kwa mfano nimesema hapa Ibara ya 27 ya Tume ya Uchaguzi imepewa dhamana ya kuhakikisha kwamba inakuwa na kanuni zitakazoshughulika na kosa lolote ambalo ama ndani ya Sheria ya Uchaguzi halimo lakini linatakiwa kufanyiwa kazi kwa muda wa papo kwa papo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Katiba sababu za mtu kutokuruhusiwa kugombea zimeelezwa na sababu hiyo haipo katika zile sifa za mgombea kwenye Katiba. Kwa kweli tunafikiria sana ni namna gani tutapata muktadha unaoweza kutusaidia ku-*address* jambo hili la jinsia kwa kuzingatia kutokuharibu Katiba lakini kutoa haki ya unyanyasaji wa kijinsia na makosa hayo; kama kosa la

kutokuruhusu mtu kugombea, lakini vilevile kushughulika na makosa ya unyanyasaji wa jinsia papo kwa papo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umesema kuna vifungu tumevipitisha, nikawa najaribu kuangalia huku nyuma, ni vipi? Kuna kifungu kinafanana na 60?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosa sifa nadhani tupo kwenye sura ya tano ya uchaguzi wa Madiwani; kukosa sifa ya kugombea, na huko nyuma nafikiri tumemaliza kifungu kinachohusu uchaguzi wa Rais, Sura ya Nne uchaguzi wa Wabunge sifa za kugombea Wabunge zimetajwa katika…

**MWENYEKITI:** Nadhani zimetajwa kwenye Katiba, humu ipo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ipo kwenye Katiba, huku hamna, hakuna huku, hatujaweka huku sawa. Waheshimiwa Wabunge sifa za wagombea Udiwani zinawekwa kwenye hii Sheria kwa sababu kwenye Katiba hazipo huku zipo za Rais na Mbunge kwa hivyo hata makatazo yaliyopo huku kwenye Katiba yanamhusu Mbunge na Rais. Hoja inakuja hivi, yale ambayo wamekatazwa kule Rais na Mbunge kosa la namna hii lipo, la kuwanyima wale sifa? Lipo ama halipo? halipo, sawa. Je, itakuwa ni haki na halali kuwawekea wao huku ilhali hawa wagombea wengine hawana? Tunatunga sheria hapa tusijetukaweka mambo Madiwani tukawa tumewakaba.

Hoja hii ni ya msingi sana kwa kweli. Mtu ambaye ameshitakiwa kwa kosa kama hili kwa kweli hastahili kuwa kiongozi. Lakini hoja ni kwamba tunaiwekaje kwa sura hiyo hapa? Kumzuia huyu mgombea

Udiwani pekee wakati mgombea Urais hajawekewa, mgombea Ubunge hajawekewa, tunamwekeaje Diwani peke yake?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kukusaidia; ukiacha hilo kosa ambalo nimelisema mimi yapo makosa mengi ambayo yamewekwa kwenye Ibara ya 60 humu kwa Madiwani ambayo pia hayapo kwa Wabunge. Kwa hiyo nadhani najaribu kukufungua uone kwamba hapa kuna sifa tofauti kabisa ambazo tunaweza zika-*justify,* hoja yangu, kwamba tunaweza pia tukaongeza ikawa ni moja kati ya sababu maalumu kama ambayo nimejenga hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Mojawapo ni ipi ambayo haipo kabisa kwa Madiwani na Rais na Wabunge ili tuanzie hapo kwenye mfano ambayo tumeiweka hapa kwenye 60 halafu huku wengine hawa hawajawekewa tumeweka hapa ili na hii tuiongeze maana kama tumeshaanza kuongeza tuongeze tu kabisa.

Jamani, angalieni wote hayo marekebisho siyo lazima aangalie Mheshimiwa Salome pekeyake mwenye hoja tuangalie wote tunatunga Sheria hapa kwa Pamoja. Ni ipi kati ya (a) mpaka (j); hakuna au ipo?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda upo *limited* lakini labda tuangalie hiyo Ibara ya 60 (1) (g), iwapo ni sehemu ya au ana ubia katika shirika au ni meneja wa kampuni ambayo ni sehemu ya mkataba wowote unaoendana na mamlaka na kuendelea. Sidhani kama hiyo ipo kwenye Katiba kwa Wabunge japo sijaangalia Katiba, lakini nadhani hiyo inaweza ikawa mojawapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome ipo kwenye (f) kwenye Katiba yetu Ibara ya 67(f) hapa imeongezewa tu maneno lakini ipo kwenye Katiba. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema hoja ni ya msingi kabisa kwamba mtu amfanya kosa na hapa inasema ametiwa hatiani maana yake siyo kwamba kasingiziwa au kafanyaje hoja ni yamsingi.

Katika mizania ya utungaji sheria huwezi kusema Diwani awekewe masharti mazito zaidi kuliko yale aliyowekewa Mbunge ama yale aliyowekewa Rais kwa sababu hawa wote ni viongozi ambao wanachaguliwa kwa nafasi ya uwakilishi. Sijui kama nimeelewaka, haya.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo

**MWENYEKITI:** Nani anayeomba Mwongozo.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Sophia.

**MWENYEKITI:** Sasa Mwongozo inabidi nivae Joho nirejee pale juu labda…

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba ushauri.

**MWENYEKITI:** Ndivyo utaratibu ulivyo, inabidi niahirishe hapa ije Siwa nipandishe pale juu nikasikilize. Bunge la Kamati lilikuwa linavunjaje Kanuni. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeongea vizuri sana kwamba tunatunga sheria, na haya mambo ya kiesheria pia yanahitaji watu walioenda shule nafikiri nyie mmekaa sana mmesoma sheria. Kama kweli tunakiri kosa la unyanyasaji wa kijinsia ni baya na ni makosa ambayo yanafanyika

sana kwenye chaguzi na tumepitiwa kama Waheshimiwa Wabunge kwa pamoja maana yake umetupa nafasi ya kusoma kwa haraka haraka wengi tumeshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanyaje sasa kama hili swala ni baya na tunafikiri kama kuna haja ya kulipekeka kule kwa Mheshimiwa Rais na kulipeleka kwa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mwisho wa siku tunarudi pale pale mambo yamekuwa magumu katika hali ya unyanyasaji tunaomba utusaidie. Nilisema habari ya mwongozo nilitaka kusema Kiti chako kitusaidie tunasaidiaje Watanzania katika hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa pamoja na mambo mengine ni kazi yangu hapa kuhakikisha Sheria zinatungwa kwa hiyo mizania. Kwa hiyo kwa mizania hiyo tutakuwa tunawaweka Madiwani mazingira tofauti na hawa wagombea wengine. Japokuwa kama kama nilivyosema hoja ni nzito, lakini kwa sababu haianzii kule ambapo makosa yote yameanzia hatuwezi kuanzisha hapa jambo jipya.

Kwa hivyo, tutafute tu namna na Serikali imesikia huko mbele katika yale mambo kwa sababu nyie mmeshasikia hoja ya Katiba mpya jamani si bado ipo kwenye kuendelea. Kwa hiyo itakapoanzia huko itaenda kwenye haya yote ili Bunge likatunga Sheria ambayo tutaanza kwenda kwenye tafsiri Mahakamani kabla ya uchaguzi alafu mambo yakawa yanaonekana kwamba hatukufanya kazi yetu vile inavyopaswa.

Kwa sababu sasa hapa tunakuwa tumewachagua wao peke yao wakati wote na viongozi wa kuchaguliwa. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Salome Makamba alikuwa ameshapewa nafasi ya kuzungumza kwa mara ya pili na kwa hivyo tunaendelea, ndio utaratibu wenyewe. Meheshimiwa Salome anasikitika lakini ni hoja ya kikatiba hata nikiitoa kwenu kuamua nitakuwa kidogo na mimi mwenyewe sijui nataka muamue nini?

Mkiamua halafu tukawa Katiba hatujaitendea haki tutakuwa hatuendi sawa. Kwa hiyo Mheshimiwa Salome amesema Mheshimiwa Mwakagenda sisi wote ni Wanasheria tunatofautiana tu zile ngazi. Kwa hiyo ile tafsiri mimi naweza kuwa nimesoma zaidi kuliko kuliko Mheshimiwa Salome Makamba. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi Mheshimiwa, hoja yako imeeleweka. (Makofi)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 61

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 62

**MWENYEKITI:** Ibara ya 62 ina marekebisho ya Kamati. Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 62(2)(a) maudhui au masharti ambayo yanapendekezwa na Kamati yanafanana na yale yaliyopo kwenye Ibara ya 50(a)(34). Kwa hiyo naamini Serikali ilishakubaliana na eneo hilo, *unless* kama wanawezakutuambia Kamati tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na sehemu (b) pia yalishafanyiwa maamuzi na Kiti chako na Waheshimiwa Wabunge waliridhia, naomba niondoe eneo hiyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Ibara ya 62 pamoja na marekebisho ya Kamati kwenye kifungu kidogo (2) (a) kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 63

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani Ibara ya 63.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mahudhui ya kifungu cha 63 yanaendana sambamba na yale mahudhui ya kifungu cha 51 na tayari Kiti chako kimekwishatoa Mwongozo kwa hiyo naomba marekebisho hayo yaondoke katika meza yako.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71
Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74
Ibara ya 75
Ibara ya 76
Ibara ya 77
Ibara ya 78

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 79

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 80
Ibara ya 81
Ibara ya 82
Ibara ya 83
Ibara ya 84
Ibara ya 85
Ibara ya 86

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 87

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 88

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 89
Ibara ya 90
Ibara ya 91
Ibara ya 92
Ibara ya 93
Ibara ya 94
Ibara ya 95
Ibara ya 96
Ibara ya 97
Ibara ya 98
Ibara ya 99

Ibara ya 100
Ibara ya 101

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 102

**MWENYEKITI:** Ibara ya 102, marekebisho ya Kamati. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inajiridhisha kwamba marekebisho yaliyoletwa na Serikali yanamakusudio sawa na yale ambayo yameletwa na Kamati kwa hiyo tunaridhika na yaliyoletwa na Serikali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 103

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 104

**MWENYEKITI:** Marekebisho ya Mheshimiwa Profesa Kabudi.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maadam yamepita katika Ibara ya 3 napendekeza neno mtazamaji katika aya hiyo ibadilishwe na iwe mwangalizi kama ambavyo tumekubali katika tafsiri ya neno kuondoa neno mtazamaji nakuwa mwangalizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mapendekezo hayo Serikali nadhani tulishakubali kule.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishakubaliana Kiswahili kinazidi kukua na kama endapo jina litatakiwa kutoholewa vinginevyo kwa kuwa kinakua tutarudi tena kwenye Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 105
Ibara ya 106
Ibara ya 107
Ibara ya 108
Ibara ya 109
Ibara ya 110
Ibara ya 111

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 112

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 102, marekebisho ya Kamati; Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ambayo Kamati imependekeza yaongezwe kwenye kifungu cha 112 yanahusu mgombea wa nafasi ya Ubunge, kwa maana ya viti maalumu inahusu uteuzi wa wagombea wa viti maalumu kwa nafasi ya Ubunge lakini masharti ya kifungu kinachofuata cha 113 kama unaweza kunifatilia yanahusu masharti ya Udiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekubaliana na mpendekezo ya Kamati ya kifungu cha 113 yanayohusu Udiwani lakini haijakubaliana na kifungu cha 112 yanayohusiana na Ubunge. Nikirejea maelekezo yako kwa vile hizi nafasi zote zinafanana kwa utaratibu nadhani labda Serikali ilipitiwa tu kwa kifungu hicho cha 112; kinahusu kuongeza Ibara (3) ambacho kinasema bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2); Tume inaweza kutoa Mwongozo kwa vyama vya siasakuhusu utaratibu utakaotumika na vyama vya siasa kuchagua wagombea wanawake wa viti maalumu. Kwa vile kifungu cha 113 kimeridhiwa na Serikali ninaamini hiki pia Serikali ikaridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Serikali imeleta kifungu kipya badala ya kuridhia yale mabadiliko ambayo hayo ya 112 na 113 Serikali imependekeza kifungu kipya cha 114 ambacho ndicho kinachoeleza hayo maneno uliyoyasema hapa. Kifungu kidogo cha 114 fasili ya kwanza inasema Tume baada ya kushauriana na msajili wa vyama vya siasa inaweza kutoa Mwongozo kwa vyama vya siasa kuhusu utaratibu wa kuchagua wagombea wanawake viti maalumu. Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndicho ninachomaanisha kwamba masharti haya yanatakiwa yawe kwa nafasi zote mbili, kwa nafasi ya Ubunge na kwa nafasi ya Udiwani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Kwa hiyo 112 wameiwekea kifungu kipya inabidi kwa Madiwani Serikali ndiyo ilikuwa haijaleta, imeleta mabadiliko kwa Wabunge kwa Madiwani ndiyo ilikuwa haijaletwa. Hivi, yale ya Kamati yapo kwa wote wawili. Haya sawa ngoja tumalizane na hii 112; kwa hiyo Mwenyekiti ukifungua hapo marekebisho ya Serikali waliyoyaleta sijui kama upo nayo hapo ukiyapitia yanajibu ile hoja si ndiyo, kwa upande wa Wabunge kwanza tumalize alafu tutafuata Madiwani.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 112 haihusu Wabunge, inahusu Madiwani wa Viti Maalum ila Ibara ya 112 ndiyo inahusu Wabunge wa Viti Maalum.

**MWENYEKITI:** Ndiyo nasema hivi, Serikali kuhusu kifungu 112 kile mlichokuwa mmependekeza Kamati, badala ya kubadili Kifungu wameleta Kifungu kipya kwa ajili ya 112 ili hicho Kifungu kipya kizungumzie hoja hiyo unayoieleza Mwenyekiti.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na wewe lakini uandishi bora wa sheria ungezingatia *marginal notes* ambazo zimeeleza kabisa kifungu Namba 112 uteuzi wa Wabunge Wanawake wa Viti Maalum. Kwa hiyo, hiyo nyongeza ambayo Serikali imeileta ingewekwa chini ya Ibara ya 112; lakini Ibara ya 13 *(marginal notes)* zinaeleza kuhusu uteuzi wa Madiwani Wanawake Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nyongeza ya kifungu hicho ingekuwa kwenye nyongeza ya 113 ili uandishi uwe bora na unaoeleweka vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Nafikiri Mheshimiwa Waziri naona umesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipokuwa inaangalia mapendekezo ya Kamati na kufikiria namna ya kukiandika kifungu hiki vizuri, muktadha wa vifungu vyote hivi viwili unatakiwa kufanana. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba kama utaridhia, wakati tunaendelea na vifungu vingine Serikali iweze kuleta muktadha huu unaofanana kwa kifungu hicho pia cha Waheshimiwa Wabunge.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa kuna namna mbili za kufanya. Namna moja ni ya kuchukua hichi kifungu 114, Mheshimiwa Mwenyekiti tuende pamoja. Ni ya kuchukua hichi kifungu kipya 114 kiendelee kubaki pale bila kwenda kule kwa Wabunge wala kwa Madiwani,

kisimame peke yake halafu kiseme Wabunge wa Viti Maalum na Madiwani wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kutakuwa kujirejea wala kuleta kifungu kipya ambacho kina maneno hayo hayo, kinafanana kila kitu isipokuwa neno Viti Maalum. Sasa hapa baada ya kuwa hilo tunaenda nalo kwa sura hiyo, ngoja tutakapokifikia hiki Kifungu kipya ndiyo tutaweza kuelewana vizuri. Mwenyekiti hii 112 nafikiri marekebisho ya Kamati tunaweza kuyaondoa kwa sababu 114 itaenda kujibu hoja ya Wabunge na Madiwani.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tunakubaliana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Ibara ya 112

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 113

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 113 nadhani Mwenyekiti kwa sababu umeshaeleza hoja ambayo ipo hapa na inafanana na kifungu kilichopita kama nimeelewa vizuri, si ndiyo Mwenyekiti?

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo tuendelee.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tuendelee. Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 114

**MWENYEKITI:** Hapa mimi sasa ndiyo nina swali na uzuri wake vile vifungu viwili vimeshapita. Nataka kuuliza swali kwenye hichi Kifungu kipya kilicholetwa na Serikali. Mwongozo wa kuchagua wagombea wanawake Viti Maalum. Tume baada ya kushauriana na Msajili wa Vyama vya Siasa inaweza kutoa mwongozo kwa vyama vya siasa kuhusu utaratibu wa kuchagua wagombea wanawake Viti Maalum.

Kifungu kidogo cha pili, endapo chama cha siasa kitakiuka mwongozo utakaotolewa chini ya kifungu kidogo cha kwanza, Tume inaweza kurudisha kwa chama husika orodha ya majina au baadhi ya majina katika orodha ya yaliyowasilishwa kwa ajili ya wagombea wanawake Viti Maalum. Sasa hapa itakuwa na Madiwani pamoja na Wabunge.

Swali langu, vyama vya siasa kwa sababu ndivyo vinavyopewa hizi nafasi kulingana na kura walizozipata kipindi cha uchaguzi, sasa mwanzo ilikuwa Uchaguzi Mkuu sasa ni uchaguzi. Kwa hiyo, mimi swali langu naomba mnisaidie Serikali Mheshimiwa *AG* na Mheshimiwa Waziri. Hivi hili siyo kwamba vyama sasa vinaingiliwa kwenye kufanya maamuzi nani aende nani asiende?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upo sahihi na hasa baada ya kufanya marekebisho kwa vifungu hivi vingine viwili, kifungu hiki lazima kiwe *redundant*, hakitakuwa tena na mkutadha.

**MWENYEKITI:** Hapa hatujafanya marekebisho; kifungu cha 112 hakuna marekebisho ya Kamati na nimeshahoji. Kifungu namba 113 hakuna marekebisho ya Kamati na nimeshahoji. Ninachohoji sasa hivi ni hichi kifungu Kipya ambacho Serikali imeleta kwa ajili ya kukubali hoja ya Kamati, ndiyo hoja yangu ipo hapo.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kifungu hiki kinajibu hoja ya Kamati kwa sababu Kamati ilipendekeza kwamba, kutengenezwe utaratibu, huo utaratibu utengenezwe na Tume wakishirikiana na

Msajili wa Vyama vya Siasa ili kuvitengenezea utaratibu vyama vya siasa namna ya kuleta Wabunge wa Viti Maalum.

Ndiyo swali langu, vile Vyama vya Siasa vyenye kura zake, vikitengenezewa utaratibu na Tume kwa kushirikiana na Msajili wa Vyama vya Siasa siyo kuingilia uhuru wa vile vyama vya siasa kuleta watu, kwamba nimeamua mimi hawa ndiyo wanawake ninaotaka kulingana na taratibu zangu ndani ya chama changu na katiba ya chama changu ambacho tumeshirika uchaguzi kwa kufuata sheria? Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna madhara ya kuachana na kifungu kipya. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni za Kudumu za Bunge Kanuni ya 34(6) tutaendelea mpaka tumalize hii kazi iliyo mbele yetu hapa kwa sababu tunakaribia kuhoji. Sasa Mheshimiwa *AG* hapo ndiyo umenichanganya kidogo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuelewa. Uandishi wa Sheria siyo kitu chepesi. Wakati tulipokuwa tunashughulikia kifungu kilicholetwa na marekebisho ya Kamati, uliona muktadha wa kifungu kile cha kwanza ni kuitaka Tume itengeneze mwongozo kule kwa vyama vya siasa. Sasa wakati Serikali inaangalia kifungu hiki ikaona kuna umuhimu siyo Tume tu, kwa sababu vyama vya siasa vinasimamiwa na Msajili wa Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wetu ndani sasa ya Serikali, kabla hoja hiyo haijachukua picha ya mwongozo kwa Tume pale tulipoongeza mwongozo wa Tume kwa kushauriana na Msajili wa Vyama vya Siasa. Tunaomba tu uridhie tulete kifungu cha kukifanya kifungu hiki kiwe *redundant*. Hakina kazi tena hapa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa kifungu cha 112 na 113 nimeshavihoji ili tuelekee kwenye hiki kipya, sasa maswali

yangu hapa ninayouliza ninaona Serikali imesema inaahirisha hicho kifungu.

**MBUNGE FULANI:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

**MWENYEKITI:** Eeh! Sawa lakini sasa kwa sababu hoja ya Kamati ambayo ilikuwa imeletwa hapa mbele ndiyo iliwafanya Serikali ilete hiki kifungu, kwa hiyo mimi nilitaka kujiridhisha kama huku siyo kuingilia uhuru wa vyama vya siasa? Kwa sababu zile kura wanaandikiwa vyama walete, sasa hawa wanaenda kutengeneza utaratibu katiba ya chama, mpaka mtu anaenda kujiunga na hicho chama ameshasoma katiba, kapitia taratibu zao ndiyo ameenda kujiunga na hicho chama, sasa sisi tunataka tena tuingie kwenye kile chama wakati tumewawekea misingi tayari? Mtu ameenda kujiunga kwa kupenda?

Haya, naona kidogo kuna sauti za akina mama humu ndani zinazoashiria kwamba kuna jambo, nimewaona moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. Haya tuanzie hapa, tutazunguka namna hii. Mheshimiwa Salome Makamba dakika moja.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba uridhie kwamba hiki kifungu kisitoke kwa sababu sisi tulikubali kuondoa 112 na 113 tukiwa na matumaini kwamba mambo yetu yatakuwa *solved* kwenye 114. Lakini nikuondoe wasiwasi kwamba, kwa kifungu hiki mwongozo ambao unaongelewa hapa wa namna ya upatikanaji yaani ni kwamba hatujafika kwenye mwongozo natamani ungekuwepo humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo huo ni namna ambavyo mchakato unatakiwa ufanyike kwa kuzingatia mambo ya *gender*, kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali, tofauti na sasa hivi kwa mfano CCM, wana Wabunge wa Vyuo Vikuu sijui, Wabunge wa *NGO*, huku kwetu CHADEMA tunachagua Wabunge wa Mkoa, Wabunge wa Vijana yaani lazima tuwe na mwongozo ambao upo *balanced,* ambao ukionekana unakuwa na sura ya kitaifa ya

namna ambavyo Wabunge wa Viti Maalum wanapaswa kupatikana ili kuondoa upendeleo, rushwa na mazingira mengine.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo mantiki ambayo tunatamani Tume ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Msajili wa Vyama vya Siasa watupatie tuwe na *standard form* ambayo mimi nikisema naenda kugombea CHADEMA leo…

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa kwa sababu nilikuwa nimetoa dakika moja. Mimi nataka kuelewa kwa sababu kila chama kimeenda kwa msajili, kimesajili Katiba yake, kimesajili taratibu zake. Sisi tunataka Msajili na Tume ije hadi kule kwenye chama kutuamulia mambo? Mheshimiwa Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala siyo kwamba wataenda kuingilia vyama, tunafahamu kwamba Msajili wa Vyama ndiye baba anayesimama katikati kuhakikisha vyama vyote vinafanya sawa sawa na Katiba zao. Kwa hiyo, sisi tulikuwa tunafikiria, Mheshimiwa Salome amesema hapa, sisi kama wanawake tunadhani, tukiwa tuna *unform* moja ya kupata Viti Maalum vya wanawake tutapunguza malalamiko na uonevu ambao tunafikiri wanawake wa miaka ijayo wasije kuyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tunapozungumzia *formula* moja wakatengeneza na labda tu niongezee kipengele hapo, isiwe Msajili wa Vyama wawekwe na viongozi wa vyama pia waambiwe kwamba utaratibu wetu wa kupata Viti Maalum ni huu hapa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, humu ndani vyama vikubwa vilivyomo na uwakilishi wa Wabunge wa Viti Maalum ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo na Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi, Wabunge wanawake wanaoenda kugombea Majimboni ukishindwa huji humu ndani. Wabunge wa upande wa CHADEMA, Viti Maalum ukienda kugombea Jimbo na

jina lako linakuwepo kwenye orodha. Ni taratibu ambazo kila chama kimejiwekea namna ya kuleta watu humu ndani.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Subiri kwanza kwa sababu ukimpa taarifa Mwenyekiti unatafuta majanga Mheshimiwa. Sawa inawezekana utaratibu wa kwenye chama chako upo tofauti lakini huo ndiyo uhalisia. Wabunge mnaogombea Majimbo upande wa CHADEMA orodha yenu upande wa Viti Maalum mnakuwepo na ninyi.

**MBUNGE FULANI:** Hapana.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, mnagombea mara mbili?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Eeh! Ninyi mnagombea mara mbili, CCM hawaruhusiwi, sasa hayo mnataka yakaamuliwe wapi zaidi ya ndani ya vyama vyenu? Yaani mnataka haya ya kwamba anayegombea Viti Maalum agombee pia Jimbo yakaamuliwe wapi? Kwenye vyama vyenu au yakaamuliwe na Msajili na Tume? Haya anayefuata, aliyekuwa amesimama tu. Haya Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa nami nisisitize kwamba tuliridhia kuondoa yale mapendekezo ya Kamati kwenye 112 na 113 kwa sababu Serikali ilikuwa imeleta mapendekezo kwenye 114 ambayo ulituambia yanaweza yakabeba yote mawili; lakini nikirejea kwenye Ibara ya 81 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, inasema kwamba bila kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi yaweza kuweka masharti yanayofafanua utaratibu utakaotumiwa na vyama vya siasa kwa ajili ya kuchagua na kupendekeza majina ya Wabunge wa aina ilitojajwa katika Ibara ya 66(1)(b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea hapo utaona kuwa inaongelewa kwa Viti Maalum. Kwa hiyo hiki tunachojaribu kukiongelea hapa ni kwamba kwa kuwa tunatunga hii sheria basi Tume itekeleze jukumu lake la Kikatiba ambalo imepewa kwenye Katiba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ipo pale pale. Tume ya Uchaguzi yaweza kuweka masharti yanayofafanua utaratibu, sasa hivi Tume ya Uchaguzi imeweka masharti au hayapo?

**WABUNGE FULANI:** Hayapo!

**MWENYEKITI:** Mmefikaje humu ndani Wabunge wa Viti Maalum? Kama Tume haijaweka mmefikaje humu ndani na humu mmo Wabunge wa Viti Maalum? Mheshimiwa Neema malizia hoja yako.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa hoja kubwa na msingi wa hii hoja ni kwamba, inasema utaratibu unaofanana. Tunachojaribu kufanya ni kwamba kuwe na utaratibu unaofanana wa namna ya kuwapata hawa wawakilishi wa Viti Maalum, lengo zima ni kuona namna ya…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema hebu ngoja kidogo, unaofanana? Hivi vyama vinafanana?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana. Imeandikwa hivi, kuweka masharti yanayofafanua utaratibu utakaotumiwa na vyama vya siasa. Kwa hiyo tunachojaribu kusema kwa hivi sasa, hicho kitu hakijafanyika ndiyo dhumuni la kuleta hili pendekezo.

**MWENYEKITI:** Swali langu mmefikaje hapa ndani kama huu utaratibu haupo?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na sisi tunaweza tukauliza Serikali ilifikaje kukubali kwa upande wa Madiwani wa Viti Maalum na kuisahau kwa upande wa Wabunge wa Viti Maalum kwa kurejea ile 113 ndiyo ilikuwa imeongezwa.

**MWENYEKITI:** Zote mbili zimeshahojiwa, Waheshimiwa Wabunge anayefuata, ukiacha Mwenyekiti, wale waliokuwa wamesimama. Mheshimiwa Hokororo halafu Mheshimiwa Manyanya. Wengine hamkuwa mmesimama.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini niungane na wachangiaji wengine kujibu swali lako kwamba vyama vinaingiliwa? Jibu ni hapana kwa kufuata muktadha wa Ibara ya 81. Kifungu cha 114 kilichopendekezwa kinasema Tume inaweza kwa hiyo mimi sioni madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefafanua vizuri kwamba vyama hivi viwili ambavyo vina Wabunge pengine kule wana ule utaratibu na huku wana huu utaratibu; lakini tukumbuke wakati mwingine hao Wabunge wa Viti Maalum kwa utaratibu huu ambao sasa hivi vyama unavitumia, utaratibu wa ndani ya chama changu ni murua kabisa, mathubuti kabisa. Tunaukubali kwa asilimia mia moja. Lakini hii pengine kwa msingi wa Ibara ya 81 itaepusha sasa, kwenye *point* "A" kuwa na Wabunge wa Viti Maalum sita ambao pengine wanavyopatikana ndiyo hiyo kutoka kwenye makabati na nini na nini na sifa nyingine ambazo zinaondoa heshima ya Wabunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo ndiyo maana pengine inaonekana kuitwa Wabunge wa Viti Maalum, pamoja na kwamba tumepatikana kwa mujibu wa Katiba lakini hilo jina linadogoisha kwa sababu ya vyama vingine upatikanaji wao Tume haisimamii kwa mchakato kama unavyofanyika ndani ya Chama cha Mapinduzi.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo na wewe unatamani vyama vifanane. Mheshimiwa Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kimsingi kwanza nadhani kwa mara ya kwanza Waheshimiwa Wabunge hasa wanawake tunajitahidi sana kwenda sambamba na Miswada hii. Ili kujaribu kuangalia changamoto zote zinazotukabili kundi hili la wanawake na tukawa tunatafuta wapi tunapita. Lengo la sheria zinazotungwa ni kurekebisha mapungufu ambayo yalikuwa yanaonekana katika maisha ambayo tayari tumeshaya-*experience* na tumeyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumeona kwamba kwa sababu Tume inayo hiyo nafasi ya kufanya hivyo na hapa tunalozungumzia ni la mtu huyu mwanamke atakayekuwa kwenye kundi la Viti Maalum ni vema hizi changamoto huko kwenye Chama tukisema tunawaachia ni sawa, lakini kuna suala la msingi la haki za binadamu, suala la msingi la haki za huyu mwanamke au jinsia kwa ujumla wake. Kwa msingi huo tunaona kwamba ukiwepo utaratibu mzuri ambao ni kwa Vyama vyote, CCM hatuna shida kubwa, lakini CHADEMA na vingine vilivyopo, mmesema vipo 19 mpaka sasa hivi vyenye usajili wa kudumu, ni vema kuwepo msingi ambao unaleta maridhiano, unaleta, kurekebisha na kujenga upya. Ndiyo lengo letu hapa, tumeona matatizo tunataka kurekebisha ili tujenge upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni kama kuna changamoto kwa sababu watakaokuwa wanatengeneza hivi vifungu Tume itashirikisha makundi kupata kanuni ambayo itatusaidia kuingiza hayo makundi vizuri.

**MWENYEKITI:** Haya, sawa, hoja imeeleweka. Mnaoendelea muangalie kifungu kidogo cha (2); "Tume inaweza kurudisha kwa chama husika orodha ya majina." Yaani Tume ikakatae Wabunge waliopelekwa na chama ambacho kimetafuta kura.

Haya, anayefuata Mheshimiwa Keisha.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarudi kwenye msingi ule ule wa kwamba, tunatunga sheria ambayo haikinzani na Katiba. Kama walivyosema wenzangu, Katiba hii inaruhusu vyama vya siasa vipendekeze na kutoa utaratibu wa kuchagua. Sasa vyama vya siasa vimetekeleza jambo moja, lakini jambo la kuchagua bado halijakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Katiba inaruhusu, nadhani ni vizuri sisi kama Wabunge tukatengeneza sheria sasa. Hii inaenda kusaidia wanawake au Wabunge wa Viti Maalum kuonekana kwamba sio Wabunge wapo wapo tu, ni Wabunge wenye heshima, wamegombea kwa utaratibu mzuri ambao umetengenezwa na sheria hii ambayo tunakwenda kuitengeneza leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo machache nashukuru.

**MWENYEKITI:** Haya, wa mwisho, Mheshimiwa Patrobas Katambi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hili jambo ndiyo maana upande wa Serikali tumesema tunaondoa kwa sababu tunazo sababu za kwamba hii ni *substantive law* ambayo imeshaeleza zile *original rights* na *obligations.* Kwa upande wa *procedural Laws* ambazo ndizo zinatoa kama *servants,* zinaenda kusaidia katika chama chenyewe kuweka utaratibu ambao unatakiwa sasa kuuleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudi kwenye sheria ya msingi, inaeleza kwamba kama ataleta nje ya utaratibu na mambo yakawa yamekiuka haki za binadamu na hisia zote ambazo ni *genuine* za Waheshimiwa Wabunge, maana yake bado pia sheria nyingine ambazo ni *principle* zitatumika kuhakikisha kwamba Tume inaamua kulingana na usahihi uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusichanganye kuhusiana na *substantive laws* ambazo zinaeleza kuhusu *original rights* na *obligation* zilizopo pamoja na hizi ambazo ni *procedural* ambazo ni *servants,* siyo *master of justice*, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Huyo alikuwa wa mwisho kuzungumza.

Mwenyekiti naona umesimama na kuna mtu yuko nyuma yako, sijui kama alitaka kuongea kwa niaba yako ama vipi. Naona ni Mjumbe wa Kamati huyo, alitaka kuongea kwa niaba yako ama vipi?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana. Nataka kujazia nyama kidogo kabla Mwenyekiti hajaongea. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massare, endelea.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa sababu uandishi unaonekana unaleta tafsiri ambayo siyo; na kwa sababu tulipokuwa tumehoji 112 na tumeshatoka kule, hatuwezi kurudi kwa mujibu wa kanuni zetu, ninashauri uandishi utofautiane na maelezo yaliyopo kwenye uandishi wa sasa. Kwa sababu, kuweka utaratibu unaofanana, Tume haiwezi kuelekeza vyama vya siasa, kwa sababu vyama vya siasa vina mlengo tofauti, na malengo tofauti ya kuja katika Bunge hili. Pia kila Chama kina Katiba yake ya wazi, na anayejiunga na chama kama ulivyosema wewe, anakuwa amekiri na kusoma Katiba ya kile Chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunashauri kwamba, bila kuathiri masharti ya kifungu hiki kidogo cha (2), Tume inaweza kuvitaka vyama vya siasa kuweka utaratibu wa wazi wa kupata Wabunge wa Viti Maalum bila kuonesha kwamba utaratibu utakuwaje, ni kama ulivyotoa mfano, Wabunge wa Viti Maalum wa chama cha upinzani ambao wako hapa, wao hugombea kwanza

kwenye majimbo, lakini Mbunge wa CCM akishaenda kwenye jimbo, maana yake ameshajiondoa kwenye Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu wa Chama changu; Chama Cha Mapinduzi, ni utaratibu wa wazi na unapita kwenye mchakato ambao ni mzuri. Kwa hiyo, vyama vingine kutokana na taratibu zao na milengo yao, ni vigumu sana kuviwekea sheria. Kwa hiyo, tuone namna ya uandishi ambao utatusaidia na kututoa hapa baada ya kutoka 112 na 113, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, imeeleweka. Kwa hiyo, kifungu hiki kinakuja ili kwenda kushughulika na matatizo kwenye chama fulani, na siyo kwamba kuna tatizo la kupatikana kwa Wabunge wa Viti Maalum ama Madiwani wa Viti Maalumu. Linakuja kwa ajili ya kushughulika na tatizo ambalo liko kwenye chama fulani au vyama fulani, lakini siyo tatizo la jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, atakuwa wa mwisho kwenye hoja hii ili tuweze kusonga mbele.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Kamati ilishauriana kwa kina sana na Serikali, nami niliamini Serikali tulielewana, lakini nimeshangaa kuona Serikali wanataka kuondoa kifungu ambacho wamekileta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, madhumuni ya Kamati ni kuwa na utaratibu wa wazi na siyo utaratibu unaofanana. Natolea mfano Chama Cha Mapinduzi kwamba utaratibu wa kupata Viti Maalum ni huu. Kwa hiyo, Tume na Msajili wa Vyama vya Siasa ajue utaratibu wa Chama Cha Mapinduzi ni huu. Pale ambapo mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi ambaye aligombea nafasi hiyo akaikosa kwa sababu utaratibu haukufuatwa, awe na fursa ya kulalamika kwa chombo kinachosimamia hizo taratibu. Kadhalika kwa vyama vingine na hii haikulenga chama chochote.

Ililenga vyama vyote vya siasa viweke utaratibu wa wazi na siyo unaofanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, malengo hapa ni uwazi *(transparency)* ili mwanachama yeyote aweze kuzisimamia haki zake pale ambapo zitakuwa zimekiukwa na chama chake. Hii ni haki ya asili ya mwanachama yeyote wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vyombo viwili kwa maana ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Tume ya Uchaguzi, wana wajibu wa kulinda haki za wanachama kwa vyama vya siasa. Hiyo ndiyo ilikuwa mantiki na ninaamini Serikali itakuwa imetuelewa kwenye dhana hiyo na inaweza kuweka kwa lugha ambayo itajibu hoja ya Kamati kwa maana ya hoja ya uwazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu kilichopo hapa mbele nimekisoma na kuwasomea tena. Mapendekezo haya niliyonayo hapa mbele hayaendi kusema vyama vilete, yanasema Tume na Msajili wa Vyama vya Siasa watengeneze mwongozo wavipelekee vyama, ndicho kilichopo hapa.

Kingine kinasema hivi, huo mwongozo watakaoutengeneza, ukiwa umekiukwa, wao wana uwezo wa kurejesha majina kwenye chama husika ili chama sasa sijui kikarudie uchaguzi wa hao hao wa Viti Maalum ama kikafanye nini?

Hoja ni kwamba, vyama vya siasa vipo kwa mujibu wa Katiba. Tume yetu ya Taifa ya Uchaguzi ipo kwa mujibu wa Katiba, Msajili wa Vyama vya Siasa yupo kwa mujibu wa Katiba. Sasa, ninyi mnataka kazi ya vyama vyenu akaanze kuifanya Tume? Haya, hapa tumepelekwa kwenye Ibara ya 81 kwamba; tena imeeleza vizuri; "Tume ya Uchaguzi, (kwa sababu yenyewe inahusika na uchaguzi) yaweza kuweka masharti yanayofafanua utaratibu utakaotumiwa na vyama vya siasa kwa ajili ya kuchagua na kupendekeza majina." Ndiyo maana mko humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge, kama ziko changamoto kwenye vyama vyetu, tusubiri Sheria ya Vyama vya Siasa pia tutaipitia hapa. Ndiyo utaratibu, tusubiri Sheria ya Vyama vya siasa tutaipitia hapa. Nasema hivi kwa sababu, ukivipokonya vyama vya siasa mamlaka ya kushughulika na wanachama wao, wewe unataka akashughulikiwe nje? Sasa vyama vya siasa, humu si tumesema mtu hawezi kuwa Diwani, Mbunge wala Rais bila kuwa na chama cha siasa? Sasa lazima chama cha siasa kiwe na nguvu za kufanya kazi zake na kushughulika na watu wake. Si ndiyo jamani! *(Makofi)*

Kwa hiyo, hiki kifungu kilichopo hapa kwenye hii ibara yetu ya 81, wala hakizungumzii hiki kilichopo humu. Kwa hiyo, tuendelee na hiki. Pia, tutakapohitaji ifafanuzi wa hiki ambacho hakifanyiki, tutafute namna nyingine, lakini siyo kwa namna kifungu hiki kilivyoandikwa hapa. Vyama vya siasa vitafute kura na vishughulike na kura zake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati na Kamati ya Bunge, kwa sababu sheria zote za marekebisho huwa zinakuja kwenu, hili mtakuwa mnaliangalia kwa karibu ili Katiba yetu kifungu cha 81 kifanyiwe kazi vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Kifungu cha 114 cha Serikali hakipo. *(Makofi)*

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

Ibara ya 114

**MWENYEKITI:** Siyo kifungu cha 114 iliyokuwa imetajwa tajwa hapa. Ile haipo, tunarudi kwenye kifungu cha 114 humu kwenye muswada. Kifungu 114 kina marekebisho ya Serikali. Ngoja niyatazame haya.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 115

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 116
Ibara ya 117
Ibara ya 118
Ibara ya 119
Ibara ya 120
Ibara ya 121

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 122
Ibara ya 123

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 124

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Lugangira, kifungu cha 124.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 124 kinaleta makosa mengineyo, nami hapa napendekeza iongezwe ibara nyingine ambayo iwe ya kwanza ambayo itaangazia matumizi hasi ya akili mnemba *(artificial intelligence)* kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu madhara ya matumizi ya akili mnemba *(artificial intelligence)* kwa lengo la kupotosha umma kwa nia ovu kwenye mchakato wa uchaguzi ni jambo kubwa ambalo linaitikisa dunia. Vitendo hivi vimeshathibitishwa katika maeneo mengi, na hata huku kwetu

Barani Afrika tuliona mwezi wa Kumi mwaka 2023 kwa Rais wa Zambia kwamba ilirekodiwa *video* ambayo ilisema kwamba hatagombea tena ilhali *video* ile ilikuwa imetengenezwa kwa *artificial intelligence.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, hata Mwenyekiti wa *African Union,* waliweza ku-*gush email* yake, barua ambayo ilionekana imesainiwa naye ikaenda kwa wakuu wa nchi za *EU* kwa lengo la kuomba ufadhili wa fedha katika mchakato wa uchaguzi jambo ambalo lilikuwa siyo kweli, ilikuwa imetengenezwa na *artificial intelligence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua changamoto hii, mabunge mengi duniani hivi sasa yameanza kuangalia eneo hili la athari za akili mnemba *(artificial intelligence)* kwenye uchaguzi. Pia hata Bunge la Dunia *(IPU)* ambalo wewe ni Rais wake, nalo limetambua eneo hili kama changamoto na tayari wako kwenye mchakato wa kuandaa azimio ambalo litaangazia madhara ya *artificial intelligence* kwenye demokrasia, haki pamoja na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya azimio hilo la *IPU* kupita, itasababisha nchi kadhaa kufanya marekebisho. Kwa sababu hapa tunafanya marekebisho ya sheria na ninatambua kwamba ipo Sheria ya Mitandao, lakini kama ambavyo ipo Sheria ya Rushwa na sheria nyingine, lakini kwa umahususi wa suala la uchaguzi, suala hili limeletwa kwenye Sheria ya Uchaguzi, basi nami naomba kupendekeza eneo hili. Nisiporidhika na majibu ya Serikali nitatoa hoja na nitaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naona anataka kusimama au vipi? Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naielewa hoja ya Mheshimiwa Neema Lugangira katika jambo hili. Pamekuwa na

mjadala na ni mjadala wa dunia sasa namna ambavyo akili bandia zitakavyoathiri uchaguzi. Hata hivyo, Serikali iko kwenye mchakato wa kufanya mapitio ya Sera ya TEHAMA hapa nchini na tuko hatua za mwisho ambapo sera itatuongoza kwenye kupitia ama kutunga sheria ambazo zitalichambua jambo hili kwa mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu jambo la akili bandia siyo suala la uchaguzi peke yake, linaathiri maeneo mengi, *lina-cut across,* nilikuwa napendekeza kwamba mapendekezo anayoyaleta tusiyaingize hapa, ila tui-*address* hoja yake wakati tutakapokamilisha mapitio ya Sera ya TEHAMA pamoja na sheria ambayo italiangalia jambo hili kwa ujumla wake. Kwa hiyo, tulichukue kama ni *concern,* liwe *addressed* kwenye sheria ambayo italishughulikia jambo hili kwa ujumla wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa Mheshimiwa Waziri Nape na ninamshukuru kwa kuungana nami. Hata hivyo, napenda kupata ufafanuzi; je, tunakwenda kwenye uchaguzi mwaka 2025, litakapojitokeza kwamba kuna watu wametumia akili mnemba *(artificial intelligence)* kupotosha, kuchafua na kuharibu uchaguzi, nini kitakachofanyika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naona unataka kusimama. Sasa, sijui ni yupi? Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo Sheria na Kanuni ya Adhabu kama *Penal Code* na Sheria ya Makosa ya Mtandao. Hivyo, hakutakuwa na *gap* kwamba endapo mtu akitenda kosa kukawa hakuna sheria ya kumwadhibu. Hivyo, tunayo nafasi ya kutumia hizi sheria nyingine, kama Makosa ya Jinai, Kanuni ya Adhabu, Sheria ya Makosa ya Mtandao, kumchukulia mtu huyu hatua wakati michakato mingine inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wazo la Mheshimiwa Neema ni jema sana, lakini kwa kuwa kuna hiyo kubwa inakuja kama alivyosema Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya masuala haya, tunawea tukatumia *penal code,* tunaweza tukatumia Sheria ya Makosa ya Mtandao na sheria nyingine ambazo tunazo kudhibiti suala hili la kutumia mitandao kuchafuana, na kadhalika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, umeshasimama mara mbili tayari.

Waheshimiwa Wabunge, ni kweli, hili ni eneo jipya linalohusu akili mnemba na mjadala unaendelea ili kujua namna sheria za kila nchi zinavyoweza kubadilishwa ili kuangalia namna ya kushughulika na hili tatizo.

Sasa kwa hapa nchini kwamba tutaanza kushughulika nalo kwenye hoja ya uchaguzi wakati ile kwa mawanda yake mapana, kwa sababu siyo lazima iwe ni hoja ya uchaguzi, yaani ni kosa kubwa kabisa, siyo hoja tu ya uchaguzi pekee. Uchaguzi ni sehemu ndogo tu ya namna unavyoweza kupata athari. Sasa kama nchi hatujaweza kufika mahali ambapo tumeshafanya huo utafiti wa kutosha na kuweza kuweka muktadha wetu tunataka kushughulika vipi na hili tatizo. Itakuwa ngumu kidogo kulianzisha kosa kwenye hii sheria inayohusu uchaguzi.

Kwa hiyo, nafikiri kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, tuendelee kufuatilia kwa karibu na kama alivyosema Mheshimiwa Neema na huko kwingine hayo maazimio tutakavyokuwa tumeshajadiliana kwa kirefu, tutaziletea Serikali ili zione namna ya kuzibadilisha sheria zake ama kuzirekebisha ama nyingine kutunga sheria mpya kabisa ili kuweza kushughulika na matatizo kama haya.

Mheshimiwa Neema, sura ni hiyo ya hiki kifungu chako. Vile vile, katika ule uandishi wa sheria, pia ingekuwa ngumu kidogo, kwa sababu kuna maeneo pia ingetakiwa tubadilishe. Kwa mfano,

unasema “Uchaguzi; kwa lengo la kupotosha mchakato mzima wa uchaguzi ikiwemo udhalilishaji, uongo na kadhalika.” Sasa hii “nakadhalika” Mahakama itashindwa kujua ulikuwa unazungumzia nini hapo? Kwa hiyo, mengine tu ni ya kiuandishi, lakini hoja ya msingi ni kwamba hoja yako imeeleweka. Yapo makosa mengi ya sura hii, lakini kwa kuwa uchaguzi ni sehemu tu, lazima tuwe tumeanzisha hili kama kosa hapa nchini halafu ndiyo linaenda kwenye mambo mengine pia.

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri hilo limeeleweka. Sasa tunaendelea. Tuko wapi?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 125
Ibara ya 126
Ibara ya 127
Ibara ya 128
Ibara ya 129
Ibara ya 130
Ibara ya 131

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 132

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 133
Ibara ya 134

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya 134 kuna kifungu kipya cha 135 kinapendekezwa na Kamati na Mheshimiwa Zainabu Katimba.

Ibara Mpya ya 135

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nimetizama Jedwali la Marekebisho la Kamati wamependekeza na wenyewe kuanzishwa kwa kifungu hichi kipya 135 ambacho kitafafanua makosa ya ukatili wa kijinsia katika muktadha wa uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti ya kifungu hichi na mapendekezo yangu ni eneo lile ambalo Kamati wenyewe wamependekeza isomeke kwamba "mtu yeyote atatenda kitendo cha unyanyasaji au ukatili wa kijinsia kwa mgombea". Sasa katika kifungu hichi hawajafafanua kwamba ukatili wa kijinsia ni kitu gani na ukingalia kwa mfano hamna sheria mahususi ya makosa ya ukatili wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu ambacho nimekipendekeza kimefafanua kuelezea kwamba ukatili wa kijinsia katika muktadha wa uchaguzi ni kitu gani. Ukiangalia kwenye Sheria hii kuna makosa ya rushwa ambayo yamefanyiwa rejea na wakafanya rejea kwenye Sheria Mahususi ya Rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye Sheria Mahususi ya Rushwa imefafanua kwamba rushwa ni kitu gani lakini kwa sababu kwa wakati huu hatuna Sheria Mahususi ya Ukatili wa Kijinsia, kwa hiyo makosa ya ukatili wa kijinsia hayafahamiki. Kwa hiyo, ndio maana nimefafanua hapa kwenye hichi kifungu muktadha unaendana tofauti ni kwamba nimefafanua kwamba ukatili wa kijinsia ni kitu gani kwenye hichi kifungu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya sasa hebu ngoja nielewe maana hii sehemu ina mapendekezo matatu, kutoka kwako Mheshimiwa Zainab Katimba umeanza kwa kueleza kuhusu mabadiliko ya Kamati. Kwa hivyo ulivyokuwa unataja Kamati nikafikiri unasema umekubaliana na ya Kamati lakini sasa kwa maelezo uliyoyatoa ni kwamba wewe ungetemani hiki kifungu kilichopo kwanza halafu hata hicho cha Kamati viondoke kiwekwe hiki cha kwako? *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mnayo nadhani haya Majedwali ya Marekebisho, sasa kwa sababu yote yanahusu kifungu kimoja sioni kama ni busara kushughulika na kimoja kimoja kukiondoa tuviangalie vyote vitatu kwa wakati mmoja halafu itatusaidia namna ya kwenda.

Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sasa sijawahi ku-*move Schedule of Amendment* ambayo iko juu ya *Schedule of Amendment* hapo utaniongoza nifanyeje, lakini naungana na Mawazo ya Kamati na naungana na mawazo ya Mheshimiwa Zainab Katimba kwa maana ya *margin note* inayohusiana na makosa yanayohusiana na ukatili wa kijinsia. Sasa kwenye *content* ya uandishi, hilo ndio nimeomba utuongoze na sehemu ambayo nataka kuboresha kwenye mapendekezo ya Kamati ni ngazi za utoaji wa adhabu kwenye makosa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imeenda moja kwa moja kwamba ukikutwa na hatia uende mahakamani na utafungwa na adhabu zimetajwa pale na nilikuwa natamani kabla hujapelekwa mahakamani kwa sababu kitakuwa ni kipindi cha uchaguzi wakati tupo kwenye mchakato wa uchaguzi, ukitenda kosa hilo upelekwe kwenye Kamati ya Maadili ya Uchaguzi, namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati ya Maadili ya Uchaguzi kama umepelekwa kwa mara ya kwanza upewe onyo kali na baada ya onyo kali ukirudia tena kosa hilo basi ufungiwe kuwa mgombea yaani uenguliwe kwenye kinyang'anyiro cha kugombea nafasi hiyo ambayo ulikuwa unagombea. *Then* ukishatoka hapo sasa adhabu za Kamati kama ambavyo zimependekezwa kwenye marekebisho haya ziweze kuchukuliwa kuendelea mbele, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Kamati ni kuhakikisha kwamba tunaondoa au tunatambua kosa la ukatili na unyanyasaji wa kijinsia wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Kamati imependekeza *formulation* ya kifungu hicho cha 135 baada ya kifungu cha 134 lakini nimewasikiliza wadau wawili hapa wamechangia nilidhani kifungu kama kilivyopendekezwa na Kamati ya Utawala Katiba na Sheria kilivyoandikwa kinaweza kumwachia fursa Jaji au Hakimu ku-*determine* aina hiyo ya kosa kama ni kosa la unyanyasaji wa kijinsia au ukatili wa kijinsia kwa tafsiri ambayo mahakama itaona inafaa kwa kuzingatia utamaduni wa mahala na wakati husika kwa sababu tunaamini tafsiri ya neno moja moja inaweza kubadilika kutegemea na mazingira na tamaduni za mahali husika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninachofurahi ni kwamba wote tunakubalina hapa pana tatizo na liko tatizo kubwa la msingi ambalo tunatakiwa kulishughulikia ili kupata suluhu na nilisema toka mwanzo ukatili wa kijinsia ni pande zote mbili. Sisi tumependekeza

ifuatavyo, na tumependekeza hivi labda nitoe maelekeza kidogo tunataka tuwe na kifungu cha adhabu lakini tumependekeza..

**MWENYEKITI:** Hapa mbele sina mlichopendekeza

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo kimeletwa.

**MWENYEKITI:** Sina, ngoja nikipate kwanza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya.

**MWENYEKITI:** Haya ni mapendekezo mapya siyo haya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio na tuli-*submit* leo.

**MWENYEKITI:** Hamja-*submit* sisi hapa hatuna marekebisho ya Serikali kwenye kifungu hiki, Mheshimiwa Waziri

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, enhe! Huu uandishi wa Sheria Bungeni ni shughuli kweli kweli lakini tutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipotazama maoni ya Mheshimiwa Zainab na ya Kamati sisi tuliona twende hivi bila kuathiri masharti ya Sheria ya Kanuni za Adhabu *(Penal Code)* ambayo imetaja makosa hayo yote mtu ambaye wakati wa shughuli za uchaguzi atatenda kitendo cha unyanyasaji au ukatili wa kijinsia kwa mgombea anatenda kosa na akitiwa hatiani kwa mujibu wa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ambazo zenyewe zinasaidia kosa linahukumiwa papo kwa papo. Sasa hofu yetu uilikuwa tukiacha pembeni hizi kanuni za uchaguzi

tukapata zile *due procedures* za mlolongo wa Mahakama mambo haya tutachelewa kwa hiyo tukaamua twende navyo vyote viwili ili tuweze kuwa tunafanya maamuzi ya harakaharaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumesema kwa kuwa anatenda kosa akitiwa hatiani kwa mujibu wa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika Kanuni za Maadili na wakati huo anaendelea pia kwenye yale mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Eenheee! Mapendekezo yaa..., kwanza nianze na haya, Mheshimiwa Salome Makamba umependekeza huyu mtu mara ya pili aenguliwe siyo?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio.

**MWENYEKITI:** Sasa kwa sababu hii siyo hiki kifungu kule kwenye zile Kanuni za Maadili siko nazo hapa mbele kwa hiyo sijazipitia. Kuna mahali ambapo wameeleza anaweza kuanguliwa vipi yule wa uchaguzi? Kuna mahali? Maana hapa nikianza kutafuta, kuna mahali anaweza kuanguliwa mgombe na ile Kamati?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hatua za awali ni zile za kumsimamisha na unapomsimamisha kwa hiyo kunakuwa na fursa ya kufuatilia ile milolongo mingine ambayo inaweza kumuondoa. Shida ya kumuondoa Mheshimiwa mgombea inatawaliwa pia na Katiba.

**MWENYEKITI:** Ndio maana nataka kujua humu kwenye haya maadili anaweza kuondolewa na ile Kamati, hawezi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Hapana anaweza kusimamishwa.

**MWENYEKITI:** Basi naanza kupunguza hapa, kwa hiyo marekebisho yako Mheshimiwa Salome Makamba kwa sababu sifa za nani anaweza kugombea zipo kwenye Katiba hatuwezi kuja kuziweka huku kwa sura ambayo inamuondoa mtu kwenye ile haki yake ya kugombea kwa hiyo hili linaondoka. Enhee!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba tafadhali, umetoka kutuongoza hapa kwenye suala la hoja ya Mheshimiwa Ng'wasi kila haki ina wajibu umetuongoza vizuri na *of course* kile kifungu ambacho Mheshimiwa Ng'wasi alikuwa ana ki-*move* kilikuwa kwa upande mmoja mwingine ni mtazamo kwa upande mmoja mwingine pia kinavunja Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuzingatia matakwa ya haki na wajibu suala la unyanyasaji wa kijinsia lazima mtu awajibike na kwa sababu huyu mtu inakuwa ni haki yake kuendelea kugombea kumbuka anamnyima haki mtu mwingine ambaye amemdhalilisha kijinsia amemfanyia ukatili wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *with due respect* nashauri busara ituongoze kwenye jambo hili ndio maana nimesema apewe haki kwa kupewa onyo kali ambalo umetusaidia nilitaka nijue kwenye hizo kanuni hilo onyo kali ipo kwa ngazi ya kwanza na ngazi ya pili aenguliwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome twende vizuri, kama hoja itakuwa ni hiyo maana yake lazima uende kule Mahakamani ili wakamtengue huyu mtu kama kashinda uchaguzi. Ukisema ile Kamati imuondolee haki yake ya kugombea sasa hii mbona itakuwa… kwanza watu watachomolewa wengi mapema tunarudi kule kule tena.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *that be the case* yaani ukisema unaiondoa *amendment* yangu yote kwa sababu ya kifungu kimoja hii nimetoa…

**MWENYEKITI:** Naiondoa ya kwako kwa sababu hii ndio sehemu pekee iliyokuwa tofauti kwa sababu tunajaribu kuangalia yale ya Kamati ya kwako na ya Mheshimiwa Zainab.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana siyo hiyo sehemu pekee.

**MWENYEKITI:** Haya cha tofauti kingine cha kwako?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, cha tofauti ni kwamba alichokileta Mwenyekiti wa Kamati yeye baada ya kukutwa na hatia *due process* ya mahakamani ina-*take place* mimi ukikutwa na hatia…

**MWENYEKITI:** Ile hatia anakuwa amemkuta nayo nani?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani labda nataka nisome kile alichoandika, Mwenyekiti wa Kamati anavyopendekeza, 135 Mwenyekiti wa Kamati anasema; "mtu ambaye atatenda kitendo chochote cha unyanyasaji au ukatili wa kijinsia kwa mgombea atatenda kosa la ukatili wa kijinsia katika uchaguzi na iwapo atatiwa hatiani anatumikia kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au faini" na kuendelea kwa *interest* ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba mtu huyo anapokuwa ametenda kosa yule ambaye anadhani ametendewa kosa anapaswa kwenda kushtaki Mahakamani sasa mimi kwa kuona kwamba *process* ya Mahakama inachukua muda na pengine inaweza kumuathiri tu huyu mgombea nikasema kwa nini jambo hili lisisikilizwe kwanza kwenye Kamati ya Uchaguzi?

**MWENYEKITI:** Haya twende kwenye ya kwako Mheshimiwa sehemu ya mwisho; "Atatiwa hatiani na Kamati ya Maadili ya Uchaguzi atapewa onyo kali na akirudia atakosa sifa za kuwa

mgombea wa nafasi hiyo." Wewe unamkosesha sifa kwa sheria mtu ambaye amepewa sifa na Katiba?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio nikasema *with due respect* kama nimetoa *option* mbili ya kwanza apewe onyo kali ya pili akose sifa kama suala la kukosa sifa tunakubaliana na mimi nitakubaliana na ushauri wako kwamba linaenda kinyume na katiba libaki hilo la onyo kali lakini tusiliondoe yaani *process* ya Kamati ya Maadili ya Uchaguzi iwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipitisha hichi kifungu bila kuchukua kifungu changu maana yake yule aliyefanyiwa ukatili wa kijinsia akitendewa kosa lile hawezi kwenda kwenye kamati ya maadili inampasa aende Mahakamani moja kwa moja *process* ambayo itamchukua muda mrefu.

**MWENYEKITI:** Umevisoma vya wenzio vifungu au umesoma chako peke yako? Umevisoma vya wenzio maana naona…

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kifungu ambacho tunachokifanyia *amendment* hapa cha Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Utawala.

**MWENYEKITI:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge kwanza hatuwezi kuanzisha yaani hatuwezi kuondoa haki ambayo mtu amepewa kikatiba na hizi sheria, hiyo ni pale mwanzo kabisa. Halafu sehemu ya pili ambayo kuna anapendekeza Mheshimiwa Salome ukiyasoma sasa hayo yote kwa pamoja yeye anataka hili kosa pale kwenye hii Kamati ya Maadili ya Uchaguzi ndiyo ambayo imtie hatiani yule mwenye kosa badala ya Mahakama.

Kwa hiyo, kwa maana ya kwamba itarahisisha maana atatiwa hatiani wakati kipindi kilekile cha uchaguzi kama ni onyo anapewa anapewa kipindi hichohicho siyo lazima watu waende Mahakamani. Lakini sasa sina hakika sana kama wale watu wanao uwezo wa kutoa haki kwa sura hiyo.

Mheshimiwa Naibu Waziri naona unataka kunisaidia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nikushukuru uko sahihi sana. Kwa haki ambayo imetolewa kwa mujibu wa katiba. Kwenye katiba na nimuongoze vizuri Mheshimiwa Wakili Msomi Salome Ibara ya 107 inasema "mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa ni mahakama".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haki ile ambayo itakuwa imetolewa kikatiba ni ngumu kwa sababu tunachotaka kufanya hapa tunashindwa kutofautisha tunatunga Sheria ya Uchaguzi ni tofauti na sheria ambazo tunataka kuzifanya sasa Sheria ya Uchaguzi ile Kamati ya Maadili tunataka kuibadilisha kuwa kama ni mahakama au *quasi-judicial board* haiwezi kuwa *tribunal* kwa msingi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uko sahihi kwenye eneo hilo kwamba mamlaka zile nyingine kuna *trial* na *procedures* zitaendelea katika utaratibu wa kawaida wa *due process of the law*, ahsante

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, aanh! Mwanasheria mkuu wa Serikali

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshindwa kumfuatilia na kumuelewa Mheshimiwa Salome kwa sababu Bunge lako na hatua hii halitungi hizi Kanuni za Maadili na anayoyaomba hayamo humu na kuja kuwa na hizi *code of ethics* maana yake kwa mujibu wa sheria ni mchakato shirikishi wa Vyama vyenyewe kukubaliana maadili pamoja na kusaini. Kwa hiyo, hoja yake inakosa mashiko kwa msingi huo, huwezi uka-*suggest* kosa la mtu kuenguliwa sifa kupitia kanuni ambazo kwa sasa hazijatamka kama kosa na ambazo hazijapitia ule mchakato wa ushirikishi

**MWENYEKITI:** Haya. Kwanza tuende kwenye hoja ya msingi. Serikali inakubali hoja ya kwamba kwa sababu huu Muswada au kuwa na kifungu kinachohusu kosa hili. Kwa hiyo, tunakubaliana kwamba kosa hili liwekwe, Si ndio? Haya kama tunakubaliana kosa hili liwekwe twende kwenye marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati.

Marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati; "mtu ambaye atatenda kitendo chochote cha unyanyasaji au ukatili wa kijinsia kwa mgombea atatenda kosa la ukatili wa kijinsia katika uchaguzi na iwapo atatiwa hatiani atatumikia kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano."

Haya marekebisho yaliyoletwa na Mheshimiwa Zainab Katimba yenyewe yameeleza kwa kweli kila kosa linalofikirika kwa sasa. Kila kosa linalofikirika kwa sasa, yale ambayo yatafikiriwa kesho na nini itakuwa kidogo mtihani. Lakini hapa mwisho kinazungumzia pia kifungo kisichopungua miaka miwili, huku wamesema miezi sita na huku kisichozidi miaka mitano, na Kamati inasema kisichozidi miaka miwili; faini isiyopungua milioni nne, Kamati inasema milioni mbili na isiyozidi milioni 20 au vyote, isiyozidi milioni tano au vyote kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge ni kweli wakati mwingine usipoweka maana yule mtazamaji ama anayelitazama hilo jambo anaweza asielewe sana. Lakini ukiweka kwa kirefu namna hii jambo lolote ambalo umeliacha maana yake halimo. Kwa hiyo, ni afadhali kuweka kile ambacho kiko kwa ujumla ili lolote hata litakaloibuka hapo baadaye na lenyewe litaingia humo. Kwa hivyo, kwa muda tulionao hapa, nilikuwa najaribu kupitia hapa, imeeleza kuhusu matusi yaani mambo mengi kwa kweli, kejeli na mambo kama hayo. Kwa sababu tukiamua kusema maana ya haya makosa ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia ni yapi? Nadhani inawezekana haya yasitosheleze ile orodha yakawepo zaidi ya hayo. Kwa sura

hiyo bora tuweke kifungu cha jumla ili yoyote yanayojitokeza yaingie hapo. *(Makofi)*

Sasa, kwa muktadha huo nafikiri kifungu kilicholetwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwa kifungu kipya kinakuwa na uzito zaidi. Changamoto tu tutakayoipata ni kwamba kosa hili linaanzishwa kama kosa la uchaguzi lakini linataka uende Mahakamani. Maana yake ni kwamba hizi kanuni zetu za maadili baada ya kupitisha sheria hizi sijajua zitaenda kuandikwa kwa sura gani ili kutokuwafanya hawa wote wakimbilie Mahakamani badala ya kuiruhusu hii Kamati ya Maadili kufanya kazi kwa ngazi ile. Kwa sababu ndiyo inamaanisha hivyo, tukishaweka hiki kifungu hapa maana yake wewe ukiona umetendewa ndivyo sivyo uende ukashtaki na inabidi huku uendelee na kampeni na kule uwe unaenda kupeleka ushahidi, sijui kama naeleweka? *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima tushirikiane hapa tuone namna ya kuliweka hili jambo hapa kwa sababu kwa kweli wote hatutaki unyanyasaji na ukatili wa kijinsia. Lakini tukiliweka hapa linamaanisha mimi na hayo makosa mengine yaliyowekwa humu pia yanamaanisha nini? Tushirikiane jamani, wale Wanasheria humu ndani, ili tusije tukamfanya huyu mtu sasa akawa yuko *busy* Mahakamani anapoteza muda wake wa kampeni huyo ambaye hajafanya kosa, wakati ile ya Kamati inakufanya ushughulike palepale Kamati ya Maadili, labda Mwenyekiti tusaidie.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Kamati ilikuwa ku-*establish* hilo kosa na adhabu. Nimesikiliza maelezo ya Serikali kwenye eneo hilo, kimsingi wamekubaliana na Kamati kwa maana ya hoja hii ya ku-*establish* hilo kosa na adhabu lakini pia wameeleza namna bora ya kushughulikia, kwa maana ya adhabu. Mimi naomba turidhie kwamba marekebisho yaliyoletwa na Serikali yanaweza kuboreshwa kidogo kwa kuakisi yale yalioletwa na Kamati ili tuweze kuvuka hatua hiyo, kwa sababu madhumuni tutakuwa tumeyakidhi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Sasa lile la Serikali liko wapi? Haya, ya Serikali inasema bila kuathiri masharti ya sheria za mtu ambaye wakati wa shughuli za uchaguzi anatenda kitendo cha unyanyasaji wa ukatili wa kijinsia kwa mgombea anatenda kosa, na akitiwa hatiani kwa mujibu wa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika Kanuni za Maadili ya Uchaguzi. Kwa hiyo siyo Mahakamani tena? Haya, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza tunakiri kwamba mapendekezo yaliyokuja hayakuja kwa *schedule* iliyowasilishwa rasmi Bungeni. Ilikuwa ni wakati wa kujadiliana na Kamati kwenye Jedwali lao kuhusiana na kifungu hiki; kwa hiyo tunakubaliana nao. Lakini marekebisho haya hoja ya Mheshimiwa Waziri inalenga sasa kuondoa lile ombwe. Kwa kusomwa bila kuathiri masharti ya Sheria za Kanuni za Adhabu maana yake katika mchakato huu wa uchaguzi jambo lililokwisha kulalamikiwa, kwa sababu lazima lichunguzwe, yawezekana kukawa na mambo zaidi, na si lazima yampe nafuu huyu, kama atakuwa ni mhalifu anaangukia zaidi hata ya hiki kilichokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, endapo itakuwa kwa muktadha wa haya yaliyo kwa taratibu za uchaguzi bado kwa ku-*subject* kwenye kanuni za adhabu faida yake ni kuwawezesha sasa vile vyombo vingine. Kama ni Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali chini ya kifungu cha 18 kutoa miongozo au kanuni ambazo hata zinaweza zikatoa *time frame* ya namna ya mashauri hayo kushughulikiwa ndani ya kipindi kile cha uchaguzi bila kuathiri; na kama ni mamlaka zingine hivyo hivyo. Kwa sababu itabidi kufuata sheria zingine na taratibu zilizopo bila kuathiri kinachokusudiwa hapa, kwa maana ni kuwezesha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali hili kosa kwa sasa hivi lipo kwenye hii Sheria ya Kanuni za Adhabu ama halipo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuanzia kifungu cha 130 na hasa 138 ya *Penal Code* kuna mawanda mapana sana ya unyanyasaji. Sasa inapokuja sasa ni lipi, maana yake ndipo inakuja sasa thamani ya haya kuwianishwa na kule.

**MWENYEKITI:** Aah, ngoja, ngoja twende vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kule sheria ipo na imekaa sawa, haina shida, shida inayoletwa hapa ni ile inayohusu uchaguzi tu basi. Kwa nini; kwa sababu hii sheria hatutaki itengeneze kosa la jinai lingine, kwa sababu kosa la jinai liko tayari kule. Hapa kosa linalotengenezwa ni la kosa ambalo pengine sijui, yaani ni kosa pengine linafanana na hili lakini linahusiana na uchaguzi pekee na linataka kushughulikiwa kama kosa la uchaguzi. Ukishalipeleka tena kwenye jinai tunaanza uka-*prove beyond reasonable doubt* sijui ukatafutee, aah! Sasa tutakuwa tena tunarudi pale pale. Kama tunataka kusema hivi basi sheria ipo tayari sasa tunatunga sheria juu ya sheria. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, …

**MWENYEKITI:** Kifungu chenu ndicho kinachotupeleka kule, kinatupeleka kule kufanya nini wakati yale makosa kule yapo tayari. Kimesema…

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu…

**MWENYEKITI:** … bila kuathiri masharti yale, maana yake yote unayoyasema hapa usiathiri kule ama mimi ndiye sielewi bila kuathiri maana yake nini. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali naona ulisimama tena. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *criminalization* na *decriminalization* ni kazi ya Bunge hili kwenye

kutunga sheria na jinai yoyote na ngazi zake na mamlaka ya kuzishughulikia huwa hazibagui kwa sababu ni uhalifu unooshughulikiwa. Sasa ni uhalifu *economic, drug, trafficking* hapo sasa…

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sasa tunakwenda…

**MWENYEKITI:** …ngoja twende vizuri, hii hii ambayo ni jinai tayari ipo kule. Hii jinai kwa namna ilivyochangiwa humu ndani inatakiwa iletwe kwenye uchaguzi ili ushughulike nalo kama la uchaguzi siyo la jinai kama ile nyingine. Kwa sababu kama ni jinai kama ile nyingine hiyo ipo tayari na bado nafikiri hoja ilikuwa ni kwamba ile jinai ipo na bado watu wanapata athari. Kwa hiyo, wanataka hili lizungumzie uchaguzi na lishughulikiwa kwa muktadha wa uchaguzi liishe pale mengine maisha yaendelee. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala sasa la dhana, makosa ya jinsia yalio kwenye *Penal Code* adhabu zake zinakwenda mpaka miaka *minimum* 30 mpaka *life*. Hebu fikirieni Waheshimiwa katika mchakato wa uchaguzi mgombea unabakwa, tulichukulie hilo, na angalieni adhabu iliyo hapa, jamii itamuacha yule mtu? Ndiyo maana ninasema tukubali ku-*brand* kosa la uchaguzi liwe kwenye *framework* ya *penal law* na *procedural law* ambazo Bunge hili limeshatunga ili iwe rahisi hata Mamlaka zingine kuwekea kanuni na kuhakikisha ndani ya miezi sita labda kipindi cha siku 30 litekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nitakupa mfano…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*, muda wetu unakimbia nakuwa kama nakukatisha, ukitupeleka huko tayari sheria ipo. Kwa nini Wabunge bado wanalalamika? Wanataka kosa hili lisiende, umesema hapa suala la dhana, ukasema sijui kitu gani lisiende

kwenye zile *standards* za kosa la kawaida la udhalilishaji. Likienda kwa mtindo ule hakuna mtu hapa kura zake zitaongezeka kwa kusubiria kesi kule mpaka iishe Mahakamani. Mtu anataka kosa lake lishughulikiwe kama la uchaguzi. *(Makofi)*

*Okay,* umeongelea kuhusu kubakwa, sasa kubakwa pengine ni *extreme* sana na mifano iliyotolewa humu ndani nafikiri kubakwa ni suala lingine lakini wanazungumzia mambo ya jukwaani, ndiyo maana huyu mwingine ameamua kuwa *very prescriptive;* na tulikuwa tunajaribu kusema tuweke la jumla. Humu anasema ataongea maneno, atachora, atafanya ishara, atafanya kitendo kinachoashiria matusi, fedheha, dhihaka na mambo kama hayo. Yaani yale tukisema sasa tunataka kwenda na haya ya kubaka tuyaweke huku wakashughulikie ile Kamati, ile Kamati kweli itaweza hayo mambo? Ndiyo maana tukasema tuchukue lile lengo la kuweka haya makosa kwa jumla ili yanapopelekwa Kamati ndiyo inapima, ile Kamati ya Maadili, kama hili ni kosa ama vipi halafu adhabu atoe. Tukilishalifanya gumu sana, kubwa sana kama yale mengine hatutafika mahali ambapo Bunge lilikuwa linajadili kifungu hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Patrobass.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, udhalilishaji, unyanyasaji au matendo yoyote yale ya ukatili wa kijinsia ni ngumu kujua litafanyika kwa utaratibu gani au litakuwa na uzito wa kiwango gani. Bado tutarudi kwenye ku-*contradict* sheria kwenye *standard of proof*. Kwa sababu hatuwezi kuwa na *criminal offenses* halafu tukaenda kuiamua *on balance of probabilities,* haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani zaidi hapo *the standard of proof* itakuwa *beyond reasonable doubt*. Sasa…

**MWENYEKITI:** Nisaidie, kesi ya Mheshimiwa Mwakagenda nadhani uliisikia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio.

**MWENYEKITI:** Mgombea amesimama jukwaani anaendelea na kampeni zake, halafu ule upande mwingine wanasema hivi jamani msimchague yule ana ziwa moja. Hiyo hapo hiyo ukiipeleka kwenye *penal code* inakujaje mwanasheria mwenzangu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mazingira kama bado tunarudi pia kwenye Kanuni za Maadili ambayo yapo…

**MWENYEKITI:** Ndio maana tunasemaje… yako tayari humu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio kwenye maadili.

**MWENYEKITI:** Hebu nitajie Mheshimiwa Waziri ni kona gani nisome.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa Kanuni hizi za Maadili unatokana na sheria mama *(parent law)* ya uchaguzi. Na utaratibu wake kila kabla ya uchaguzi vyama vya siasa vyote wanakaa pamoja na kuangalia muktadha wa mazingira ya uchaguzi na kuweka kanuni ambazo zitasaidia kuweka mwongozo, kama ni kusimamisha, kama nikufanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukisoma hizi kanuni utagundua vipo vipengele vimewekwa *in general,* lakini vina-*address* makosa hayo ya unyanyasaji wa jinsia na makosa ….

**MWENYEKITI:** Nipeleke kwenye kimojawapo Mheshimiwa ili tupite hapo. Nipeleke kwenye kimojawapo. Pitia tu taratibu Mheshimiwa.

Mheshimiwa Patrobass nakuruhusu usimame kwa hapa ili mtafute hicho kifungu *faster*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kifungu cha 2(2)(2), ukurasa wa tisa…

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa tisa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vya siasa na wagombea hawatapaswa kufanya yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, (a) naiacha; (b), kutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji na vitisho na lugha ya uchochezi, uvunjifu wa amani na kuashiria ubaguzi wa kijinsia, ulemavu, rangi au maumbile kama alivyosema Mheshimiwa Sophia kwenye mikutano ama kwenye shughuli zozote za kampeni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya. Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kama tulivyosema hakikuwepo lakini sasa tunataka kukiweka ili Wabunge na Madiwani na wote kwa kweli wanaogombea wasipate huo udhalili.

Haya, Waheshimiwa kanuni zetu zinasema hivyo na Mheshimiwa Patrobass Katambi ulikuwa unasema hatuwezi kutunga sheria ambayo inafanyaje? Umetumia maneno gani? Nataka kutumia ya kwako.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwenye kosa lolote linalokuwa la jinai *standard of proof* haiwezi kuwa *on balance of probability.*

**MWENYEKITI:** Huku hatuanzishi jinai, kwa hiyo umeshaeleweka, nilitaka hicho nielewe hoja yako. Huku hatuanzishi jinai tunataka liwe ni kosa la uchaguzi. Aah, tunaanzisha kosa la uchaguzi, kama ambavyo huku kuna rushwa. Huku si tumetaja rushwa jamani, hivi rushwa imetajwa wapi humu? Ngoja, makosa mengineyo ya uchaguzi, adhabu ya hongo, takrima, adhabu ya kujifanya mtu mwingine, sijui halafu makosa mengine yako wapi? *(Makofi)*

Kwa hiyo makosa mengi tu rushwa humu imo ambayo imetajwa kwa muktadha ule kule ama ni kosa la uchaguzi**.** Ushawishi mbaya kwa Wajumbe, Maafisa wa Tume, adhabu kwa watu wenye hatia ya vitendo vya rushwa na vitendo haramu. Haya yamewekwa kwa muktadha gani humu jamani? tusaidiane, ndio tunatunga sheria hapa.

Sasa nimeipata, Mwenyekiti wa Kamati hebu twende kwenye kifungu 132 na Serikali, kifungu 132 ambacho kilishapita. Hapa inasema adhabu kwa watu wenye hatia ya vitendo vya rushwa na vitendo haramu imeeleza hapa najaribu kupiga kura, namshawishi halafu anasema anatenda kosa la kitendo cha rushwa na akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Waheshimiwa Wabunge tuko pamoja hapo? Eenhe, tutafute mahali ambapo humu tunataka kufanya sisi wenyewe, maana tusije tukawa tumekishikia bango kifungu kimoja tu halafu mengine. Haya, hatia ya kujifanya watu wengine, kuingilia mikutano halali. Haya mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya kutazama haya maadili ya uchaguzi ikiwa kifungu kilichopendekezwa na Kamati, ikiwa kifungu hicho kikiingia humu ni kwa namna gani kitakuwa kina *contradict* hii. Hicho kifungu kinachohusu ukatili wa kijinsia kikiingizwa humu

kwenye sheria hii inayohusu mambo ya uchaguzi na kikaandikwa kwa sura ile ambayo wameleta Kamati kitakuwa kina-*contradict* hii kwa namna ipi?

Mnanijibu wawili, sasa sijui nimsikilize nani kwanza? Mheshimiwa Naibu Waziri halafu Waziri halafu *AG*.

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hiki kimetungwa mwishoni kinarejea kwenye Kanuni hiyo, kwa hiyo hai-*contradict*, kinatupeleka kwenye rejea kama jinsi ambavyo ilivyokuwa hiki….

**MWENYEKITI**: Shida ya kifungu cha Serikali kinatupeleka kwenye *penal code*.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimesema kanuni.

**MWENYEKITI:** Soma hapo mwanzo, soma hapo mwazo, kinasemaje?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuathiri masharti ya Sheria ya Kanuni na Adhabu…

**MWENYEKITI:** *Penal Code?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes*, bila kuathiri.

**MWENYEKITI:** Kama kinatupeleka kule sasa tunatunga cha nini, kwa sababu kule viko tayari hivi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulisema tunatunga kosa ambalo litakuwa ni la kiuchaguzi na Waheshimiwa Wabunge wakapiga makofi hapa.

**MWENYEKITI:** Lakini sasa *standards* si ni zile kule?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukubaliane.

**MWENYEKITI:** Aah *God!* Mheshimiwa Waziri amejishika kichwa, Mheshimiwa *AG*. *(Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rahisi sana tungetumia *phraseology* iliyotumika kwenye 132 lakini msimamo ambao nafikiri na hoja hata ambazo Mheshimiwa Katambi amekuwa akitumia ni maneno yaliyo kwenye jedwali la Kamati. Ingelikuwa Kingereza ukishasema atatenda kosa maana yake hapa ni *offense* na akitiwa hatiani maana yake *up on conviction.*

**MWENYEKITI:** Sisi hatutaki iwe *offense,* ukishaifanya *offense, offenses* zipo *already.* Ukiifanya *offense* huku kwenye uchaguzi sasa ni ya kazi gani? Yaani hicho kifungu si kitakuwa *superfluous?*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya Mwenyekiti halafu Mheshimiwa Wakili Swalle.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha wa maelezo ambayo umeyatoa hivi karibuni, Ibara ya 132 ya Muswada unaopendekezwa, Ibara ndogo ya (2)(a) na (b) zinaeleza kuhusu makosa lakini ukisoma (b) inaeleza kwanza ina-*establish* kosa na ina-*establish* adhabu sawa na mapendekezo ambayo Kamati imeyaleta mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema; "Mtu ambaye (a) anapiga kura au anamshawishi mtu mwingine na kadhalika kuhusu kupiga kura." Halafu inakuja, "(b) kwa madhumuni ya kujipatia karatasi ya kura huku akijua anatoa kadi batili ya kupiga kura anatenda kosa la kitendo haramu na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi 200,000 au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi 10, 12 au vyote kwa pamoja." Mantiki yake ni nini? Kama ulivyosema haturudi tena kwenye *penal code,* tuna-*establish* kosa la kiuchaguzi na adhabu zinazoendana na masuala hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Wakili Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nadhani Mwenyekiti wa Kamati ametuongoza vizuri, mimi nilikuwa nadhani yale maneno *without prejudice* ina maana kwamba hayo ambayo yanafanyika huko kwenye *penal law* yataendelea huko, lakini hapa kwa muktadha wa sheria hii tunashughulika na kosa la kiuchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hata kama sina hayo mapendekezo hapa vizuri ya Serikali, sisi tu-*establish* kosa la kiuchaguzi kwenye Sheria hii lakini tukitambua tunapofanya hivyo hatuathiri mambo mengine ya makosa ya jinai ambayo yapo kwenye sheria zingine, ndiyo jambo ambalo liko hapa kwenye sheria hii.

**MWENYEKITI:** Utungaji wa sheria Kiswahili ni mgumu sana, bila kuathiri ni nini Mwanasheria, Kiingereza chake ni nini? *Notwithstanding* au *without prejudice?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *without prejudice to other.*

**MWENYEKITI:** Ahaa, ambayo tafsiri yake?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaweza kuwa bila kuathiri masharti mengine.

**MWENYEKITI:** Maana yake yale masharti yapo na lazima yafuatwe, nadhani watu tunachanganya hapa. Siyo kwamba uyatupe yale ndiyo useme unasonga namna hii hapana. Maana yake yale yapo na usiyaathiri, bila kuathiri masharti yale unaenda. Si ndiyo jamani? Humu ndani uzuri hamna Jaji aliyewahi kugombea ili atusaidie tafsiri nzuri.

Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti hapo ulipotupeleka hili kosa halipo kwenye *Penal Code,* hili kosa hili lililoanzishwa hapa ni jipya kabisa nafikiri. Hili la mtu anapiga kura anamshawishi mtu mwingine nadhani kwenye *penal code* halipo ama lipo?

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika.

**MWENYEKITI:** Halipo, sijawahi kulisoma kule. Haya Waheshimiwa ngoja tukubaliane hivi, swali langu ni moja tu halafu tuvuke hapa. Kifungu hiki kikiwekwa hapa, kwa namna ambayo hakitupeleki kwenye *penal code* kinazungumzia uchaguzi tu, halafu na hizi kanuni bado zikazungumzia hiki kitu kilichoko hapa, yaani kwa maana ya kwamba Kamati ya Maadili bado ina nguvu ya kushughulika nalo hili tuliloliweka hapa, athari inakuwa wapi? Yaani athari ya kisheria inakuwa wapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya kisheria umelifanya kosa kuwa la uchaguzi na limekuwa katika mfumo huu ambao tunausema, shida inakuja kwenye kanuni baadaye. Unapofanya *decision* ambayo itaenda kuathiri haki ya mtu ya kikatiba ya kugombea na akaondolewa labda au akapewa adhabu ambayo…

**MWENYEKITI:** Hayo ya kuondolewa unayaongeza wewe, tuende kwenye kifungu kilivyoandikwa hapa ili tutunge hapa tuondoke.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye kifungu.

**MWENYEKITI:** Ehee!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo athari itakuja kwenye *decision* ambayo itakuja kuwekwa kama itaenda ita-*contradict* na *decisions* na mamlaka ambazo zimewekwa. Kwa mfano, kama unasema unatoa *conviction* au adhabu, maana yake lazima huyo mwamuzi kwenye mamlaka awe na hayo mamlaka ambayo yapo kisheria hayawezi kuja kupingwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ninachokiona pia tusipoweka vizuri…

**MWENYEKITI:** Jamani ngoja, Mheshimiwa hebu shika hii, Mheshimiwa Zainab nimekuona. Hebu fungua na huo ukurasa wa tisa mpe huyu Kanuni. Ehe twende taratibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kusema kwamba…

**MWENYEKITI:** Ngoja shika hiyo Kanuni kwanza ukurasa wa tisa. Twende hapa tuliposema; "Kwa kutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji, vitisho au lugha inayochochea." Haya yote kule kwenye *penal code* si yapo? Mbona yamwewekwa huku? Maana yake ni nini, wale Wajumbe wa Kamati ya Maadili wanao uwezo wa kushughulikia haya kama makosa ya uchaguzi kipindi cha uchaguzi. Kama hivyo ndivyo na hapa wote tumesema inaendelea, uvunjifu wa amani kuashiria ubaguzi wa kijinsia maana yake wanayo. Ulemavu, rangi, maumbile sijui kwenye mikutano kwenye shughuli zote za kampeni.

Wabunge wanachokitaka kiwekwe kifungu sasa kinachohusu udhalilishaji wa kijinsia unaohusika na uchaguzi, yale ya *criminal* mtu aendelee kule na *criminal* zake! Kina athari gani? Mimi sioni kina athari. Sasa tusonge mbele. Kaa Mheshimiwa, kaa hapo ngoja nitoe mwongozo tumalize hapa tusonge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kifungu kilichopendekezwa na Kamati sehemu hii ya mwisho ambayo wameweka adhabu, naangalia vizuri hapa cha Serikali na cha Kamati najaribu kuona kipi kitatupeleka sehemu ambayo michango ya Waheshimiwa Wabunge ilitaka twende. Nafikiri sawa hiki cha Serikali tukiondoa maneno; "bila kuathiri masharti ya Sheria ya Kanuni za Adhabu" tunaondoa ile *Penal Code* ikae kule na yale makosa iendelee na shughuli zake. *(Makofi)*

Tunakuja hapa kwenye; "Mtu ambaye wakati wa shughuli za uchaguzi anatenda kitendo cha unyanyasaji au ukatili wa kijinsia kwa mgombea anatenda kosa na akitiwa hatiani kwa mujibu wa kanuni za maadili ya uchaguzi atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika Kanuni za Maadili ya Uchaguzi." *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii tutakuwa sehemu ya maelezo yaliyotolewa kutoka kwenye upande wa Kamati yamo na haya yameweka kwa ujumla kwa hiyo makosa yote aliyokuwa ameainisha Mheshimiwa Zainab haya wote tukae nayo. Tume ile haya na uzuri Serikali mnayo yale mapendekezo ya Mheshimiwa Zainab. Ile *prescription* aliyoitoa ni muhimu ikaongezwe huku kwa sababu huku ndiyo mmeandika na maneno kejeli na nini, sasa yaingie yale humu kwenye Kanuni ili kuweza kuwa imechukua mambo yote yaliyokuwa yanalalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, humu kwenye Sheria tunaweka cha jumla ambacho hakiathiri Kamati ya Maadili kufanya kazi yake, lakini Kamati ya Maadili inaposhughulikia ukatili wa kijinsia itakuwa imepata nguvu zaidi kutoka kwenye kifungu hiki kinachohusu kesi za uchaguzi. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Karibu.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina lengo la kukupotezea muda lakini kwa vile Kanuni unazo hapo na wakati mimi nachambua sikuzipitia hizo Kanuni na umeona namna ambavyo hili tatizo ni kubwa. Sisi hatujui ukubwa wa adhabu zilizoko kwenye Kanuni na mimi kwa sababu nimeshiriki uchaguzi na ninajua chache utafungiwa mikutano miwili, mikutano mitatu mtu kanidhalilisha imeniathiri. Sasa isije ikawa tu mtu anafungiwa mikutano miwili halafu zege linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani tupate mwanga wa ukubwa wa adhabu ambayo itakuwa inatolewa kwa mtu ambaye amekutwa na hatia ya kosa la udhalilishaji wa kijinsia angalau, kabla hatujapitisha hicho kifungu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa uzuri wake hii huku haiondoi kama unataka kwenda njia ile kule nyingine. Hii itashughulika tu na ule muktadha wa uchaguzi. Kwa hiyo kumzuia asifanye kampeni ni adhabu kubwa kabisa kwa mtu anayegombea maana yake kuna maeneo hatofanya mikutano, hatoweza kuwafikia wapiga kura. Kama atazuiwa mpaka siku ya kura pia jema, akizuiwa wiki tatu wewe unafanya kampeni peke yako yeye si watu wote unaweza ukawaambia amejitoa hayupo na wewe unatumia sababu hizo hizo lakini kule kwingine hakukuondoi wewe kwenda kufuata haki yako. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nadhani hapa tutoke kwa sura hiyo. *(Makofi)*

Haya kwa hivyo, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Zainab Katimba tutachukua marekebisho ya Serikali tutaondoa ile sehemu ya kwanza inayohusu masharti ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu ili ibaki kwenye wale wale walioko kule wakati wa uchaguzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumependekeza kwa Serikali kwa sababu hizi Kanuni hatuzitengenezi sisi humu ndani. Tumependekeza wakachukue maneno yale; katika maneno yale yanayokosekana humu yale ambayo ameyaletea marekebisho Mheshimiwa Zainab yakaingie humu ili wakati wanayatazama na yenyewe yawemo. *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kifungu Kipya cha 135 kinachohusu kuanzishwa kwa kosa la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika uchaguzi hii Sura Namba 16 hapa tutaondoa kwa sababu inahusu kule kwingine. Kwa hiyo kosa litakuwa linaitwa hivyo Waheshimiwa Wabunge, "Unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika uchaguzi." Kwa hiyo, tumeingiza hilo kosa humu kwenye hii Sheria. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana Waheshimiwa. *(Makofi/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsanteni sana. Sasa ili tuweze kwenda kwa mtiririko mzuri, hiki kifungu kipya tumeshahoji kimeshaingia lakini tutaendelea kuita zile namba zilizoko kwenye Muswada halafu tutabadilisha namba baadaye. Haya kifungu 135 kilichopo sasa tunaendelea, Katibu.

Ibara ya 135

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 136

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 136 kinahusika na nyaraka zinazohusiana na uchaguzi, kwa maana ya matangazo mbalimbali ambayo wanayatumia, mabango na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imependekeza na hiki kifungu kilikwepo kwenye Sheria inayofutwa kilipendekeza kwamba unapokuwa na bango wakati wa uchaguzi unataka kwenda kulibandika mahali, lazima liwe na muhuri na anuani ya mpigachapa au mchapishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeangalia mazingira yetu ya Kitanzania na tumeangalia na hatari ambayo mgombea mwenzio anaweza kuchapisha mabango ya aina hiyo hiyo na akayabandika yakiwa hayana sifa hizo na ukaonekana wewe ndiye uliyebandika. Tulipojaribu kuangalia upande wa Serikali ni namna gani wanaweza kudhibiti mgombea ambaye anapingana na mimi akachukua mabango akayatengeneza bila kufuata hizo sifa akayabandika

halafu akaja kunikatia rufaa kwamba nimevunja hiyo kanuni ya uchaguzi nitakuwa nimetenda kosa ambalo linanipa adhabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maadam hatuwezi kusimamia vitu kama hivyo tulidhani huu siyo wakati mzuri wa kuweka vitu kama hivyo. Tukafikiria hawa Madiwani huko vijijini wataenda kuchapisha wapi machapisho au mabango ambayo yatatumika na yatakwa na sifa kama hizo. Kwa hiyo tuliona kiuhalisia kifungu hiki hakitekelezeki, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Serikali Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni njema na tulipeleka kifungu hiki tuligundua kwamba tulipata matatizo sana kwenye chaguzi zilizopita. Yale mabango ambayo yalikuwa hayajawekewa hivyo vielelezo ambavyo tunavisema hapa kwa mujibu wa Sheria ilionekana kabisa kwamba kuna wakati mwingine wagombea ama tunaita washabiki tunawaita nini sijui wale, wapambe eh? Wapambe wa wagombea wakati mwingine walikuwa na uwezo wa kutengeneza mabango ambayo yana kashfa dhidi ya wagombea wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu hujui chanzo cha bango hilo ni nani na wapi, kwa hiyo ilikuwa ni ngumu sana kuchukua hatua kwenye Kamati za Maadili na kuweza kudhibiti mambo hayo. Kama mabango hayo yataonesha *originality* yake, wapi yalikotengenezwa ni rahisi sana ku-*prove* kama kweli lilitoka kule ama halikutoka kuliko kama litakuwa liko *plain* kabisa na halina kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa wale ambao tulikuwa kwenye uchaguzi mwaka 2015, 2020 Vyama vya Siasa vilitakiwa baadaye baada ya tatizo hili kujitokeza, wadhamini wote katika vyama vya siasa wayadhamini mabango yote ambayo yalikuwa

yanatumika kwenye uchaguzi ili kwenda sambamba na tatizo hilo ambalo lilikuwa limejitokeza. Kwa hiyo, kulikuwa na *mischief* hapo ambayo tunafikiri sasa hivi ni lazima tutafute dawa ambayo itaweza kutusaidia.

**MWENYEKITI:** Najaribu kuwaza kama, hii si ni mbinu ya uchaguzi au? Siyo mbinu ya uchaguzi? Haya, Kamati inapendekeza imeleta jedwali la marekebisho inataka kifungu hiki kifutwe kwa sababu upo uwezekano mgombea mwenzako akachapisha jambo ambalo siyo wewe umefanya akafanya yeye lakini kwa upande huo huo ukiisikiliza Serikali nayo inaona wewe mwenyewe unaweza ukamfanyia mwenzio hila, kama hivi ninavyosema ni mbinu za kiuchaguzi. Kwa hiyo anataka kuzuia huyu mwenye hiyo mbinu ili asimfanyie mwenzake lakini sasa sijui kama hili eneo tunaweza kuliwekea haya mazingira maana wote tumepitia jamani kwenye uchaguzi kwa hiyo sijajua yaani uwezekano. Kwa sababu pia hao wafuasi wanaweza kuwa wamekusaidia wewe kutengeneza mabango yako lakini pia wanaweza kutengeneza na ya yule ya mtu mwingine, kwa hiyo lina sura zote. Hivi hili haiwezi ile Kamati yetu ya Maadili ikaenda kuwasikiliza hawa wagombea wakajitetee huko? Eti si waende wakajitetee kule hapa tuondoe kifungu hiki? *(Makofi)*

Nani kasimama, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kulikuwa na mabango tena huko? *(Kicheko)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Serikali lakini pia nakubaliana na Kamati *I mean,* kwamba ni bora hiki kifungu kiondolewe. Tumeangalia tu upande wa mabango lakini tunafahamu fika kuna wakati maana yake inategemea na kiongozi gani wa juu, kuna wakati unaenda kuchapisha hata hayo mabango inategemea uko upande gani. Wanaweza wakakataa hata kuyachapisha, wanaweza wakakataa hata kukupatia gari lako ukabandika mabango kwenda kuyafanyia *branding.* Kwa hiyo nakubaliana kabisa na Kamati kufuta hiki kipengele ili kuweka uhuru na usawa katika kampeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu tunapogombea tunapeleka yale mabango kwa Wakurugenzi lakini mwisho wa siku Wakurugenzi wanaweza kukusaidia kwamba limepitishwa lakini mwisho wa siku adui yako kama inavyosema Kamati akaifanya kwa sababu yeye anachotaka ni kukuharibia. Kwa hiyo, mimi naunga mkono maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Patrobass.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama lilivyoelezwa vizuri na Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, lengo kubwa hapa ni kile ambacho kinaenda kubandikwa *public* kijulikane kwamba kimetoka kwa mgombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna wajibu ambao ilikuwa inahitajika ukitengeneza bango lako uende kwa msimamizi wa uchaguzi wakaliangalie kuanzia lilivyowekwa, picha yake, maelezo yake yaliyopo pale kama hayaendani na hayakinzani na Kanuni za Maadili zilizopo za maadili. Baada ya hapo, unapata ile *proof* ya kwenda kubandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lolote linalobandikwa nje ya yale yaliyothibitishwa na Mamlaka ya Uchaguzi, maana yake ni batili. Kwa hiyo, hakutakuwa na hoja tena kwamba 'amenibandikia bango.' Hiyo ilikuwa inaondoa changamoto hiyo. Kuna vyama vingine ambavyo vilifanya vizuri zaidi hasa chama pendwa, chenyewe kilikuwa kina utaratibu wake wa kupitia mabango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama Cha Mapinduzi kilikuwa kinaangalia mabango ambayo yamethibitishwa na yanaenda kule. Kwa hiyo, hata likitengenezwa lingine na mtu ambaye ana nia ovu, basi itaonekana moja kwa moja kwamba hili halija-*originate* kutoka kwa mgombea ambaye ameruhusiwa, ndiyo *essence* ya hiki kifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Eeeh! Leo mitihani iko mingi hapa mbele. Mheshimiwa Yahaya.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Naona Bunge la jioni litatukuta humu ndani, lakini hamna neno.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Kamati ni kuondoa haya ambayo yanatokea. Ukweli kwa nchi hii bado haijafikia wachapaji kuwa na nembo zao. Wachapaji wengi, kwa mfano tumchukulie mtu kama Diwani yuko Kijijini kule Kalambo anampata wapi mtu wa kuchapa akaweke nembo ili apeleke kwa Mkurugenzi atambuliwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hapa sheria inasema wachapaji waweke alama zao chini kwenye lile bango ambalo linataka kubandikwa. Kwa hiyo, hoja tumeona nchi hii bado hatujafika huko, ndiyo maana Kamati inaishauri Serikali na Bunge lako Tukufu kwamba iondolewe hii ili baadaye tutakapofika kwa wachapaji wenye nguvu na uwezo wa kutengeneza na kuweka, basi tunaweza tukafikia huko, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hapa tulitaka kukiwa *mischief* gani? Ngoja nimwulize ambaye hagombei. Yaani kuna *mischief* gani kwenye uchaguzi ambayo tulitaka kui-*address* hapa? Mpaka imebidi nichanganye na Kiingereza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyoelewa, ilikuwa ni kuondoa tu kuruhusu kundi fulani kuhujumu taratibu za uchaguzi za chama kingine kwa mabango ambayo hayajaratibiwa vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tunazungumzia demokrasia, siyo! Hatuoni kuna namna mchapaji fulani anaweza akakataa kuchapa mabango ya chama fulani akigundua kwamba atajulikana! *AG* huo uwezakano upo au haupo?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Aah, nazungumza na ambaye hagombei, ninyi si mna *interest!* Kwenye hoja hii, hata mimi sigombei.

Mheshimiwa *AG,* uwezekano huo wa mtu kukataa kwa sababu atakuwa ananasibishwa na mabango ya mtu wa chama fulani, upo au haupo? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezekano upo, lakini kwa mifumo iliyopo, anaweza kushughulikiwa ipasavyo.

**MWENYEKITI:** Sasa unamshtaki wapi na amekataa biashara? Wewe umeelewa swali la msingi? Jibu wewe pamoja na kuwa unagombea. Je, upo uwezekano wa mimi mwenye kibanda changu nikakuuliza, wewe chama gani? Unataka niweke jina langu hapo! Aah, sitaki. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni-*practice,* kwa sababu anapofanya kazi hiyo wakati huo kwanza ame-*register* hiyo biashara. Kama amei-*register* biashara, anapoenda kufanya kazi hata kama ni ya ushindani, ana uhuru na haki ya kuweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto yake, haya mabango yanavyochapishwa kiholela ni vile wakati mwingine yanaenda kugusa haki ya msingi ya mgombea. Ndiyo maana tunasema kwamba lazima kwanza yatambulike yalikotoka na pili, Mamlaka ya

Uchaguzi itambue kwamba mgombea huyu ana mabango haya na ambayo ndiyo yataenda *public* katika kubandikwa. Tofauti na hapo, itakuwa ni *chaos*, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niliuliza hapa ile nimetumia neno "*mischief*", Kiswahili linaitwa nini? Yaani kwamba kuna changamoto ambayo tunataka kushughulika nayo, mpaka sasa hivi nawasikiliza bado sijaiona hiyo changamoto ambayo tunataka kuiondoa kwa kifungu hiki. Changamoto iliyopo ni nini yaani?

Serikali, changamoto yetu ni nini? Kamati inataka kifungu kifutwe, changamoto yetu ni nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakueleza, ni *practice* ambayo imekuwepo, hakuna asiyejua, wakati mwingine mnakuwa na mabango ya mgombea wenu na wakati mwingine mgombea wenu hata wa Kiti cha Urais mmeyatengeneza vizuri, mmeweka ujumbe wa kampeni vizuri, lakini katika kipindi hicho hicho cha kampeni anatokea mtu mwingine ana-*copy* lile bango lenu hivyo hivyo, anabadilisha ujumbe, na wakati mwingine anaweza kuweka hata maneno ambayo hayana maadili kwa namna moja ama nyingine na kuliweka lile bango mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, msipokuwa na *mechanism* ya kuliona bango hilo kwa wakati, hamjui aliyetengeneza ni nani, wapi?

**MWENYEKITI:** Sawa. Je, upo uwezekano wa *forgery*? Yaani kwa mfano mimi Jenista *and Company* ndiyo imepewa labda *tender* ya kuchapa mabango yangu, si ndiyo! Mtu akaamua naye kujitengenezea. Maana uchaguzi si ni vita jamani! Akatengeneza mahali, pale pakaandikwa Jenista *and Company* wakati siyo wewe. Uwezekano huo upo au haupo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sheria itapitishwa, mtu ambaye atakuwa *reliable* kwa kazi hiyo, ina maana kwamba, na tunasema hapa, mtu akishafikia hatua ya kuweza kufanya hiyo kazi ya uchapishaji wa mabango na nini, ana uwezo wakuwa na *seal* yake, ana uwezo wa kuwa na muhuri na saini yoyote ambayo ita-*protect* hiyo bidhaa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna mtu atatengeneza bango ambalo ni *fake,* ni rahisi tu kujua kwamba hili siyo lenyewe; na kwa kutumia sheria na taratibu tulizonazo, kuna uwezekano tu wa kutambua kwamba bango…

**MWENYEKITI:** Naam! Kama ambavyo tuweza kutambua hiyo kwamba ni *fake,* hata hii nyingine tunaweza kutambua pia kwamba ni *fake*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, *we have to make progress*. Kuna marekebisho hapa ya Serikali na ya Kamati, naanza na marekebisho ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, wanaoafiki mapendekezo ya Kamati ya kufuta kifungu hiki waseme ndiyo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda, kifungu kinafutwa. Tunaendelea.

Ibara ya 137

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 137 Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yangu kwenye kifungu hiki ni kuhusiana na kosa lile la

ukatili wa kijinsia likithibitika kuwa mgombea alitumia ukatili wa kijinsia katika uchaguzi, basi iwe ni hoja mojawapo ya kupinga matokeo ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kile kifungu cha ukatili wa kijinsia tumesema kwamba tunapeleka haya makosa, tumefanyia marekebisho hapa na tukapitisha tukasema tunapeleka haya makosa kwenye Kamati ya Maadili na huko kuna adhabu zake, kwa hiyo, nadhani kinaweza kikatafsirika hivyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Zainab Katimba alikuwa anapendekeza kufuta kifungu cha Serikali na kuweka cha kwake. Sasa kwa hoja ile ambayo tumetoka nayo kule mwanzo, anakubaliana kwamba haya marekebisho yake yaendane na ile hoja ambayo tumeipeleka kwa Serikali kwa sababu sisi hatutungi hizi kanuni, wakatazame namna ambavyo wataoanisha sasa haya mapendekezo yake na lile pendekezo la kuongeza yale makosa humu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 138
Ibara ya 139
Ibara ya 140
Ibara ya 141

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 142

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 143

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 144

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 145
Ibara ya 146

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 147

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 147, Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha ule ule ambao nilitumia kutoa kifungu cha 137(2) ambacho kinazungumzia kupinga matokeo ya uchaguzi kwa kutumia kosa lile la ukatili wa kijinsia ambalo adhabu zake zimewekwa kwenye Kanuni ya Maadili ya Uchaguzi, sasa kifungu hiki pia napendekeza katika Uchaguzi wa Madiwani, kwa sababu kile kifungu cha mwanzo kilikuwa ni kwenye Matokeo ya Uchaguzi ya Wabunge, kwa hiyo, kwa muktadha ule ule naona tutumie tafsiri tuliyoitumia katika kutafsiri kosa la ukatili wa kijinsia.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Inatoka wapi?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko huku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Swalle.

**TAARIFA**

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Zainab Katimba, japokuwa tumeshapita kwenye kifungu cha 137, lakini ninavyofahamu kwa uzoefu ambao nimefanya kwenye baadhi ya kesi za uchaguzi, unapokwenda kupinga matokeo Mahakamani, kati ya swali unaulizwa, kama hayo makosa ulipaswa kwenda kwenye Kamati ya Maadili, utaulizwa; je, umewahi kutoa taarifa kwenye Kamati ya Maadili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba mchakato wa kwenda kwenye Kamati ya Maadili na adhabu zake haizuii kosa hili tena baadaye kuwa sehemu ya kupinga matokeo Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sawa. Hicho kifungu alichokuwa anataka kukifuta mwanzo, nadhani hapo kwenye Serikali Mheshimiwa Swalle, kwenye huu Muswada namna ulivyo kwa sasa, kifungu cha 137 fasili ya (2) inasema: "Uchaguzi wa Mbunge utatangazwa kuwa batili", yametajwa hapo kwamba "wakati wa kampeni za uchaguzi maelezo yaliyotolewa na mgombea au kwa niaba yake na kwa ufahamu wake na ridhaa au idhini yake kwa nia ya kutumia hoja za ukabila rangi, udini, tofauti au kuhusu kati ya mgombea iwapo ni wa jinsi moja kwa nia ya kutumia tofauti hizo."

Sasa yeye alitaka liongezeke hilo la "ukatili wa kijinsia." Yaani liwepo hapa. Kwa hiyo, ndiyo maana kwa sababu hiki cha 137 ameondoa, imekuja huku mbele. Kwa nini aliondoa kwenye 137? Kwa sababu kwa ujumla wake lile kosa la ukatili wa kijinsia ambalo litakuwa linahusu uchaguzi, ni kwamba hapa tumelianzisha kwa ujumla, lakini yale maelezo marefu yatapelekwa kwenye Kanuni za Maadili.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, na ndiyo maana nimesimama kumpa taarifa Mheshimiwa Zainab Katimba kwamba kupeleka haya makosa kwenye Kamati ya Maadili hakuzuii kosa hilo baadaye kuwa sababu ya kupinga uchaguzi. Kwa hiyo, hakuwa na sababu ya kuondoa kosa hili hapa, linapaswa kubaki. Ndiyo hoja yangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya sasa ameondoa kule kwa Wabunge. Kwa hiyo, ndiyo tuko kwa Madiwani sasa hivi na kwa sababu kwa utaratibu wetu tukishahoji kifungu, Bunge limeshafanya maamuzi, na ili turejee huko inabidi tuje kwa mabadiliko ya vifungu tena. Yaani siyo hapa tulipokaa, yaani inabidi tuje na *amendments* pengine watapoleta mabadiliko ya sheria mbalimbali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu zoezi la utungaji sheria ni endelevu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu ndio huwa unaleta haya mabadiliko ya sheria mbalimbali nafikiri ni muhimu kweli kwenda kulitazama kwa sababu ilivyoondolewa ile hoja ya mwanzo tukafikiri pengine inapaswa kwenda kwa sura hiyo na Mheshimiwa Zainab alipoondoa kwenye 137 nami nikaafiki kwa kupitia hiyo hoja aliyokuwa ameitoa.

Kwa hiyo, nafikiri ni muhimu haya mambo mawili yatazamwe kama yatahitaji kurekebishwa, basi yarekebishwe ili mtu asipate faida kwa ule udhalilishaji akawa tu alizuiwa kufanya kampeni, halafu baadaye tukakuta ameshinda wakati alitiwa hatiani. Sasa kama alishinda, ndiyo Mbunge yule mwingine aende Mahakamani sasa akatumie hiyo kwamba huyu nilimpeleka Maadili, alipewa adhabu, lakini ile adhabu bado ameshinda uchaguzi. Kwa hiyo, sasa ndiyo nimekuja kupinga ili asiwe Mbunge au asiwe Diwani kwa muktadha huo.

Kwa hiyo, kwa sasa katika utungaji wa sheria, nadhani kama tumeondoa kwa Wabunge, tunaondoa na kwa Madiwani, lakini ni muhimu Serikali ilichukue jambo hili ili kama tutahitaji kuja nalo baadaye sasa lije kweli lianzishe haya makosa ili mtu asifaidi, yaani

asikae humu Bungeni wakati kafanya udhalilishaji huko nje au kafanya ukatili wa kijinsia na bado akashinda uchaguzi. Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 148
Ibara ya 149
Ibara ya 150
Ibara ya 151
Ibara ya 152
Ibara ya 153
Ibara ya 154
Ibara ya 155
Ibara ya 156
Ibara ya 157
Ibara ya 158
Ibara ya 159
Ibara ya 160
Ibara ya 161
Ibara ya 162
Ibara ya 163
Ibara ya 164
Ibara ya 165
Ibara ya 166
Ibara ya 167

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 168

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 168, Mheshimiwa Profesa Kabudi.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeze tuongeze maneno katika aya ya (b) ya kifungu hiki cha 168 ili ilingane na aya (a) na aya ya (c) ya kuweka ukomo wa matumizi ya fomu hizi ambazo ziko chini ya sheria ya mwaka 1985 na ya mwaka 1979 ili kuondoa mwanya wa mtu kusema kwamba fomu hizo zinaendelea.

Kwa hiyo, moja, zote zilingane na ziweke ukomo wa matumizi ya hiyo fomu wakati sheria hii mpya itakapotoa fomu nyingine zitakazotumika ili kuwe na consistence na uniformity kati ya (a), (b) na (c). Tukiangalia (a) imeweka ukomo na ukiangalia (c) imeweka ukomo, lakini ukiangalia (b) kwenye fomu zilizotolewa na sheria ya mwaka 1985 na 1979, haikuwekwa ukomo. Sasa ili pasitoe loophole au mwanya wa ubishi huko mbele ya safari, ionekane kwamba na zenyewe zina ukomo. Ndiyo sababu ya kupendekeza nyongeza hiyo ambayo inafanana na (c) na (b).

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna tatizo na eneo hilo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. NENELWA MWIHAMBI *ndc* - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani…

**MWENYEKITI:** Ngoja Katibu, hebu twende 112. Endelea na ulichokuwa unasema.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa hoja, taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa mujibu wa Kanuni ya 102(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imeupitia Muswada wa Sheria ibara kwa ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023 kama ulivyorekebishwa au kubadilishwa katika Kamati ya Bunge zima sasa ukubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. sasa nitawahoji kama ulivyo utaratibu wetu.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa lengo la kuweka masharti ya kusimamia Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kufuta Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya Mwaka 1979 pamoja na mambo mengine yanayohusina nayo**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu na kwa upande wetu kama Bunge tumeshamaliza kazi ya kutunga Sheria ya Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023.

Kama ilivyo ada baada ya kumaliza sisi tutampelekea Mheshimiwa Rais ambaye na yeye atafanya kwa sehemu yake kupitia vifungu vyetu vya Katiba vinavyomtaka yeye aweke saini ili Sheria iwe imekamilika.

Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya. Kamati ahsanteni sana kwa kazi nzuri lakini pia Serikali tunawashukuru kwa ushirikiano.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:** Kamati ya Bunge Zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuketi. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Kamati yako ijielekeze kwenye Muswada wa Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023. Ukurasa wa tatu, jina refu la Muswada lina marekebisho ya Serikali na Kamati.

**Muswada wa Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023**

Jina Refu la Muswada

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeangalia marekebisho yaliyopendekezwa na Serikali yanafanana na yale yaliyokusudiwa na Kamati kwa hiyo, tunayaondoa ya kwetu, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Jina refu pamoja na marekebisho ya Serikali Waheshimiwa Wabunge linaafikiwa?

*(Jina Refu la Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kichwa cha Sehemu ya Pili ya Muswada

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kulingana na yale marekebisho yaliyokubaliwa huku mwanzo hii sehemu inayosema kuanzishwa muundo na majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuongeza neno huru hapo, marekebisho hayo yanaafikiwa?

*(Kichwa cha Pili cha Muswada kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

**MWENYEKITI:** Ngoja, kifungu cha 5 Serikali imerekebisha nini hapa?

Waheshimiwa Wabunge, hii Ibara ya 5 inahusu muundo wa Tume na Serikali imeleta marekebisho. Marekebisho ya Serikali yanasema Mwenyekiti…sijui wote tuko hapo? lakini kifungu kidogo cha Pili, Rais atateua wajumbe wa Tume kama ifuatavyo:-

(a) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume kwa kuzingatia masharti ya Katiba kutoka miongoni mwa majina yanayopendekezwa na Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya mashauriano na Jaji Mkuu wa Zanzibar.

Serikali, hapa kidogo kuna tofauti gani kati ya Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano na Jaji wa Zanzibar kupendekeza hayo majina na ile Kamati ya Usaili kupendekeza majina? Badala ya hawa watu wawili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia muswada ulivyo kwa sababu hawa watu wawili pia ni wenyeviti wa…mmoja ni mwenyekiti wa Kamati ya Usaili na mwingine ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Usaili. Kwa hiyo, hawa watu wawili tofauti siyo kubwa na ninaweza kusema haipo kwa sababu wao ni sehemu ya ile Kamati ya Usaili.

**MWENYEKITI:** Ipo kwa sababu hawa ni watu wawili, yaani ni kama vile, mimi nionavyo, wanasheria na nyinyi tusaidiane tunatunga sheria hapa. Kama tunasema Mheshimiwa Rais ameridhia kuwe na mchakato wa kuwapata hawa mwenyekiti na makamu mwenyekiti halafu huo mchakato ukawa ni watu wawili sasa tumechukua mamlaka ya Rais ya kazi gani?

Ile tume, samahani siyo tume ile kamati ya usaili mwenyekiti ni Jaji Mkuu, makamu mwenyekiti ni Jaji Mkuu wa Zanzibar, mjumbe mwingine mwanasheria mkuu wa Serikali, mjumbe mwingine nani?

Nadhani ni Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu kitu kama hicho.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mjumbe huyo mmoja ukiacha wale wawili, mwenyekiti na makamu, Mwenyekiti wa Haki za

Binadamu lakini mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Anamteua yeye mwenyewe?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Kwa nini isifanye kazi Tume badala ya hao watu wawili. Kwa sababu tutarudi palepale kwenye nini. Yaani tunataka zoezi hili kwa sasa hivi kwa sababu mchakato hauko wazi, haijulikani, sasa inataka kujulikana halafu tunataka tumpe mamlaka hayo Jaji Mkuu peke yake halafu mamlaka hayo apewe Jaji Mkuu wa Zanzibar?

Hapana, waamuliane yaani siyo watu wawili wafanye hii kazi. Ifanye ile kamati ya usaili impelekee Rais isipokuwa hawa mwenyekiti na makamu wasiingie kwenye kufanyiwa usaili lakini kamati ya usaili ndiyo ipeleke majina badala ya watu wawili. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna shida kabisa na mapendekezo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuendelea na ushauri wa Kamati kwamba Kamati ya Usaili itakuwa na majukumu mawili. Jukumu la kwanza ni kupendekeza majina ya atakayekuwa mwenyekiti na makamu mwenyekiti. Jukumu la pili ni kuendesha usaili kwa wale wajumbe wanaotambulika na Ibara ya 64 ya Katiba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naam, naam.

Waheshimiwa wajumbe inaonekana haya mambo yalikuwa njiani bado yalikuwa hayajafika hapa mezani. Sasa hivi nimeletewa, Katibu amenipatia sijajua amepokea saa ngapi, ni kwa sababu mazingira ya utengenezaji wa hii Sheria kidogo imekuwa tofauti na yale masharti tuliyonayo ya zile Sheria nyingine kwa hiyo inaendelea kutungwa tukiwa hapa hapa ndani.

Sasa nimeletewa hapa maandishi ambayo yanakaa vizuri zaidi kwenye kifungu hiki. Yanasema hivi, nitawasomea ili nitakapowahoji mjue kifungu tunachokipitisha kitasomeka kwa namna gani.

Kwa kufuta aya (f) ya jedwali la marekebisho na kuiandika upya kama ifuatavyo:-

Katika Ibara ya 5(a) inasema kwa kuongeza mara baada ya Ibara ndogo ya 1 ibara ndogo ifuatayo, Ibara ndogo ya 2 sasa itakavyokuwa, Rais atateua wajumbe wa Tume kama ifuatavyo:-

(a) Mwenyekiti na makamu mwenyekiti wa Tume kutoka miongoni mwa majina yatakayopendekezwa na Kamati ya Usaili kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 74 fasili ya kwanza (a) na (b) na Ibara ndogo ya (2) ya Katiba na Kanuni zitakazotengenezwa chini ya Sheria hii. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Kamati ya Usaili itapendekeza majina ya mwenyekiti na makamu mwenyekiti kwa Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hiki ndiyo mlichohojiwa Waheshimiwa Wabunge. Haya, kifungu cha 5 na marekebisho haya niliyoyasoma hapa ya Serikali kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeyatazama marekebisho yaliyoletwa na Serikali yanafanana na yale ambayo tulikusudia kwa hiyo tunakubaliana na marekebisho yaliyoletwa na Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Serikali inapendekeza kufuta kifungu cha 10.

Ibara ya 10

**MWENYEKITI:** Mapendekezo ya Serikali kufuta kifungu cha kumi ambacho kilikuwa kinahusu uteuzi wa mwenyekiti na makamu

mwenyekiti na wajumbe wa Tume, pendekezo hilo la Serikali la kufuta kifungu hiki linaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya 11

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 11 tunayo marekebisho ya Serikali, uko hapo Mheshimiwa Waziri? Tuko pamoja Mheshimiwa Waziri?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12

**MWENYEKITI:** Ngoja, baada ya kuwahoji kifungu cha 11 Waheshimiwa Wabunge, marekebisho yaliyoletwa na Serikali ni marekebisho ambayo kwa kweli inabidi tuwapongeze maana saa nyingine huwa yanapita huku tunakuwa hatujui wamesemaje maana ya kwao huwa tunasema tu na ya Serikali.

Mheshimiwa Katambi ananiangalia kama asome yeye haya marekebisho. *(Makofi/Kicheko)*

Marekebisho haya yanasema hivi, kwa kuongeza aya ifuatayo baada ya aya (b) kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Serikali za vijiji, mitaa na vitongoji Tanzania Bara kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa katika Sheria itakayotungwa na Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Sheria hii itatungwa nyingine tena lakini wamefanya jambo la kheri sana kwa sababu wadau walilisema sana jambo hili. Sasa nimeona niseme hapa kwamba Serikali jamani ni sikivu sana. Mazingira haya ndiyo unaweza kusema Bunge liipigie makofi Serikali. *(Makofi)*

Haya ahsanteni sana kwa hiyo, majukumu ya Tume jamani limeongezeka na hilo, tunawashukuru sana.

Katibu tunaendelea.

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 16 pamoja na Marekebisho ya Serikali. Waheshimiwa Wabunge, kwenye hiki kifungu, Serikali inasema kufuta neno "posho" popote lilipo na badala yake kuweka "mshahara." Hapa tunazungumzia Wajumbe wa Tume. Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Tume, Serikali, hawa Wajumbe wa Tume wataacha kazi huko walikokuwa wakishateuliwa? Wanaacha kazi? Kwa sababu posho maana yake watu wana kazi zao nyingine wanafanya zile na za Tume. Je, hawa wanaacha kazi? Mheshimiwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawaachi kazi na ndiyo maana hawawezi kulipwa mishahara kwa hiyo watalipwa posho. Kwa sababu taarifa zao za utumishi zitahamishwa kutoka kwenye Tume ya Utumishi wa Mahakama. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 16 kwa namna kilivyo, kinasema Wajumbe wa Tume watalipwa posho na stahili nyingine kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo itakayotolewa na mamlaka husika. Kifungu kidogo cha Pili kinasema Wajumbe wa Tume watalipwa kiinua mgongo baada ya kumaliza

muda wa ujumbe wao. Serikali imeleta marekebisho inasema kufuta neno "posho" popote lilipo na katika Ibara hiyo na badala yake kuweka neno "mishahara."

Haya, sasa sijajua, Wajumbe wa Kamati naona mmesimama. Mheshimiwa Yahaya, halafu Mheshimiwa Khadija Taya.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala, ilionekana Wajumbe kulipwa posho halikuwa na shida lakini kipengele kinachofuata kwamba watalipwa kiinua mgongo. Anayestahili kulipwa kiinua mgongo ni yule anayelipwa mshahara. Lazima itengenezwe *mechanism* ya kwamba, wale aidha waombe likizo bila malipo wanapoteuliwa na Tume au namna gani. Kwa sababu huwezi kumlipa mshahara mtu ambaye ana ajira nyingine ya Serikali katika Serikali hiyohiyo. Ndiyo hoja iliyokuwepo hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija Taya.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kusema hivyohivyo. Hiyo hoja ilikuja kwa sababu ya kiinua mgongo; na sisi wote tunafahamu kiinua mgongo hakiwezi kupatikana bila mshahara. Ndiyo maana tuka-*propose* kwamba, kama mmetaka kuwalipa posho, muwalipe kiinua mgongo bora mtengeneze huo mfumo wa kuwalipa mshahara waache shughuli nyingine wanazofanya kwa kipindi hicho wawe wanafanya hiyo kazi tu. Ahsante.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Sijajua Taarifa inatajwa wapi. Anhaa, Mheshimiwa Francis Mtinga.

**TAARIFA**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba, Waheshimiwa Madiwani

wanalipwa posho na wanalipwa kiinua mgongo. Kwa hiyo ile kauli ya kusema kiinua mgongo hakiwezi kulipwa bila mshahara, nadhani itakuwa ina shida. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya jamani ndiyo maana unajua hivi vishkwambi vyetu tumepewa kwa ajili ya kazi; maana si kila kitu mnachoona Spika huku mbele, tunatunga Asheria hizi wote.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Inatokea wapi Taarifa na ni nani anapewa? Mheshimiwa Professa Kabudi.

**TAARIFA**

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani shida ni lugha kwa sababu kwa Kiswahili *gratuity* ni kiinua mgongo na *pension* ni kiinua mgongo. Nadhani tunakokwenda Ofisi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tutengeneze Istilahi ili kuondoa neno moja kutumika katika muktadha mbalimbali. Ingekuwa kwa Kiingereza tungesema *they will be paid gratuity*, lakini *gratuity* Kiswahili ni kiinua mgongo, *pension* Kiswahili ni kiinua mgongo kwa hiyo tunakuwa na shida ya upungufu wa Istilahi za kutosha kutofautisha ukilinganisha na Kiingereza. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge, hawa Wajumbe wa Tume kwa kweli kusema watalipwa Mshahara na Serikali maana yake kwanza walipwe kila mwezi halafu hawawezi kulipwa mishahara miwili, sheria zetu haziruhusu. Sasa, *anyway*, uzuri wake kifungu kilichoko hapa kwenye hii "bila marekebisho ya Serikali" nadhani kina mantiki zaidi kuliko haya marekebisho yaliyoletwa hapa. Kwa leo itabidi mtumie sana Busara ya Spika kwa sababu wengine hivi vifungu mnakuwa hamjaviona kwa karibu kwa hiyo leo tutumie Busara ya Kiti.

Busara ya Kiti inasema hivi, tutaenda na Muswada ulivyo kwenye kifungu cha 16. Walipwe posho na hicho kinachoitwa kiinua mgongo kwa jina lolote, ndiyo hichohicho. *(Makofi)*

Halafu, kiinua mgongo jamani si ni kuinua tu mgongo, yani wala si lazima kipangiwe kinapitia njia gani, njia yeyote. Hapa napo pakirejewa kuandikwa posho kwa huko baadaye ila kwa sasa kifungu Kibaki namna kilivyo, walipwe posho na si Mshahara kwa sababu utaashiria waache kazi huko wanakotoka. Kifungu cha 16, hakina marekebisho yeyote.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yeyote)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kichwa cha Sehemu ya Tatu

**MWENYEKITI:** Kichwa cha sehemu kinabadilishwa kwa sababu ya lile neno "Huru" linaloingia hapo kwenye neno "Tume" baada ya neno "Tume". Kwa hiyo tunaafiki?

*(Kichwa cha Sehemu ya Tatu ya Muswada kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

**MWENYEKITI:** Ibara ya 23 wanafuta hiki kilichopo na kuleta kipya. Serikali, mbona haya marekebisho yanafanana na Muswada ulivyo? Yaani marekebisho mliyoleta hayana tofauti na Muswada ulivyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na hicho ndicho nilichokuwa nafanya kuwasiliana na Mwandishi wa Serikali. Nasema hiki Kifungu hakina marekebisho kinatakiwa Kibaki kama kilivyo kama tulivyokiandika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapa mbele itabidi niletewe nanii. Haya, kifungu cha 23 hakina marekebisho yeyote, kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo ya Serikali, napendekeza kubadili mpangilio wa vifungu katika muswada huu.

**MWENYEKITI:** Haya.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapendekeza kubadili mpangilio ya vifungu vya Muswada huu baada ya marekebisho tuliyoyafanya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mabadiliko ya Mpangilio wa Vifungu unaafikiwa?

*(Mabadiliko ya mpangilio wa Ibara yaliyopendekezwa na Serikali yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake kwa Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa Hoja, Taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, leo siyo mchezo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na kwa mujibu wa Kanuni ya 102(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya

Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na Marekebisho yaliyofanyika. Naomba sasa kutoa Hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023 kama ulivyorekebishwa au kubadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe na Bunge. Naomba kutoa Hoja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa nitawahoji hoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki, kwa hivyo Muswada huu umepitishwa na Bunge.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Kwa lengo la kubainisha Muundo, Majukumu, Utaratibu wa Upatikanaji wa Wajumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Sifa za Mkurugenzi wa Uchaguzi, kuweka Utaratibu wa Uendeshaji wa Vikao vya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa Mara ya Tatu na hiyo inahitimisha safari yetu ya kutengeneza Sheria hii inayohusu Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2023 na hivyo baada ya kuwahoji Waheshimiwa Wabunge na kusoma

kwa mara ya tatu maana yake sisi kama Bunge tumemaliza mchakato wetu wa kutunga Sheria. Kama matakwa ya Katiba yalivyo, tutampelekea Mheshimiwa Rais ili naye aweze kutia Saini yake halafu iwe Sheria ambayo inaweza sasa kuanza utekelezaji wake.

*(Muswada wa Sheria kwa ajili ya kubainisha muundo, majukumu, utaratibu wa upatikanaji wa Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na sifa za Mkurugenzi wa Uchaguzi, kuweka utaratibu wa uendeshaji wa vikao vya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kuweka masuala mengine yanayohusiana nayo – Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws [Amendment] Bill, 2023)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejiridhisha na marekebisho yaliyoletwa na Serikali kwamba yanajibu hoja ya Kamati kwa namna ya kutosheleza, ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko ya Serikali)*

Ibara Mpya ya 12

*(Ibara Mpya ya 12 iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ninaomba kwenye kifungu cha 13(d) ambapo

panasomeka; "*The Parties financial and property management rules*" baada ya maneno hayo ndipo Marekebisho yangu yaingie.

**MWENYEKITI:** Ndiyo jenga Hoja ili tujue yapite ama yasipite.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo mengine yote kuanzia (a) mpaka (h) yanataka vyama kuwajibika katika maeneo mbalimbali. Katika eneo hili pamoja na wajibu wa kutoa taarifa za fedha, nilidhani ni jambo la msingi iwapo tutakuwa na *mechanism* ya kuzuia *illicit financial flows* kwenye vyama ili kuepuka kujikuta tunakuwa na vyama ambavyo vinakuwa *financed* na makundi ambayo yanaweza kuhatarisha usalama wa nchi.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna shida na Kifungu hicho, kwa sababu tunapolitaja hili eneo si kama tunaweka Kifungu cha kutambua kosa na adhabu. Kwa hiyo ni kutambua tu kwamba hilo pia ni eneo ambalo Msajili wa Vyama ama Sheria hii ya *Political Affairs Laws* itatambua jambo hilo pia katika kufuatilia *financials. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hapo alipopendekeza Mheshimiwa Mbunge kukiingiza hichi Kifungu, kweli, yaani, *unless* mi ndiye sijaelewa. Mheshimiwa Kanyasu, kifungu kinasema; "*The principle Acts amended by adding immediately after Section 10(b) the following, documents to be maintained by a Political Party.*" Inaenda kwenye 10(c)(1)(d) ambapo umesema wewe iongezeke; inasema;

*10C.-(1) a fully registered Political Party shall at all times maintain the following documents:*

*(d) the party's financial and property management rules."*

*Now you are proposing* ikishasema yaani katika hizo *documents "The parties" financial and property management rules containing measures to avoid any funds from Illegal sources and repeating mechanisms"*?

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *that's what I mean...*

**MWENYEKITI:** *No, it can't go there,* kwa sababu hizi ni *documents* ambazo chama cha siasa kinapaswa kuwa nazo, yaani kikiulizwa lete kiwe nazo. Sasa hii tukiingiza hapa kwamba yaani "*the party's financial and property management rules*", yaani wanataka zile *rules* hasa unasema zile *rules* tuongezee hapo neno *containing measures to avoid any funds from illegal sources and reporting mechanism? Like how do the two sit together?* Naona ulisimama. Mheshimiwa *AG* sijui tuko pamoja hapo maana, au niko peke yangu.

Mheshimiwa Kanyasu, pendekezo lako ni zuri lakini hapo unapolingiza yaani hata sioni vinaendana namna gani; yaani kwa sababu nia yako ni kwamba, hivi vyama visiwe vina, *I don't know how to put it.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kanyasu sisi tulivyomwelewa ni kwamba anataka zile *document* nyingine ambazo zitawekwa pamoja na hizi nyingine kwenye chama angalau zioneshe uhalisia wa fedha zilizopo ili kuzuia hizo fedha nyingine haramu.

**MWENYEKITI:** Sasa hii ni chama kweli mnataka wafanye, yaani chama kijiwekee *measures* za ku-*avoid* kitakuwa kinatuambia nini yaani, siyo sisi ndiyo tutengeneze mifumo wa kujua hiki chama kinapokea ama hakipokei ama, yaani chama kituambie kwamba, yaani hiki kifungu kilipowekwa ndiyo penye shida! Kwa sababu hiki kifungu kinasema *document to be maintained by a political party.*

Sasa haya tunayaongezaje hapa ndiyo swali langu, kwa sababu tukiona tu neno *financial* hapa tukasema na haya yanaingia hapa kidogo jamani!

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kaamua kuniacha mwenyewe sasa mtihani, Mheshimiwa Tadayo

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani lengo la Mheshimiwa Kanyasu ni zuri, lakini mimi na-*tend* zaidi kukubaliana na mwelekeo wa kwako huo kwamba, nadhani kilichokuwa kinatakiwa hapa ni kama vile ambavyo tulikuwa tunasema kule kwenye *policy* kwamba chama kiwe na *gender policy,* basi chama kiwe pia na *policy against illicit financial flows, money laundering* na mambo yanayofanana na hayo. Nadhani hicho ndicho ambacho kinatakiwa, *rather than* kuwa tu na *document* ambayo imekaa pale haitatusaidia chochote, ni hayo mawazo yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Patrobas.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nadhani lengo kama lilivyosemwa kweli ni jema, lengo ni kutotumia fedha ambazo hazieleweki zimetoka wapi kwa maana ya utakatishaji wa fedha. Kwenye kifungu hiki cha 13(d), tukienda na *spirit* hiyo ya Mheshimiwa Kanyasu bado unaona kwamba inaingia na ndiyo maana Mheshimiwa *Chief Whip* Waziri alikubaliana kwamba haina tatizo isipokuwa tutakapokiingiza nakubaliana na wewe kwamba kitakuwa kimeleta *uncertainty*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa tu ni kwamba kwa sababu ya jinsi kilivyo hata sasa kwenye (d) ku-*maintain* zile *document* itakuwa ni pamoja na matakwa yaliyopo kwenye Sheria ya Gharama za Uchaguzi ambayo tayari tunayo, pia tunayo Sheria ya *Money Laundering* ambapo kama itatokea *fraud* ama wizi wa namna yoyote bado kwa sheria za sasa tunazo. Kwa hiyo ni kama

wazo la Mheshimiwa Kanyasu kwa kutumia hii *provision* iliyopo, bado liko *taken into board,* ahsante.

**MWENYEKITI:** Maelezo yenu mnanichanganya, mmesoma hiyo sehemu ya mwanzo ya hivi vifungu vinatokea wapi? hivi ni vitu vinavyokihusu chama, yaani hata hiki kifungu kinahusu *parties financial and property management,* yaani pesa za kwangu mimi pia na *properties* za kwangu mimi, sasa wewe pale ndiyo unataka uweke kifungu kinachohusu *illicit funds, like how do the two sit together,* mnanichanganya mnavyosema hakina shida, hakina shida vipi yaani tunakiwekaje hapa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa *spirit* ile ile ya alichokisema labda tunachanganya kwa sababu tunataka kuingiza pia hoja ya Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Soma kuanzia huko juu utaelewa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia hapa kwenye kifungu cha 13 kwa jinsi kilivyo ni sahihi ni *document* za chama chenyewe na *rationale behind* ya kutunga hii *provision* ya 13, ilikuwa ni hiyo hiyo ku-*maintain* masuala ya *finance* kwa ujumla na chama ki-*maintain.* Sasa itakapotokea yale ambayo Mheshimiwa Kanyasu anayasema, tayari kwa *provision* hii inaturuhusu kwa sababu sheria nchini zilizopo tayari Sheria ya Gharama za Uchaguzi na Sheria hii ya *Money Laundering* zinaweza kutusaidia kwenye kupata *solution* ambacho anakitaka Mheshimiwa Kanyasu hata kama tusipoingiza lile wazo ambalo amelisema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu wazo ni zuri lakini kifungu hiki na hapa uliposema kiingie kinahusu chama kiwe na taarifa kuhusu fedha zake na mali zake, ndiyo kinachosema. Sasa Kifungu hiki hiki

tunataka kuweka mazingira ambayo kinaweka chama kijiwekee makatazo kwenye hizo *document* zake chama kijiwekee makatazo. Sasa kukaa hapo kwa kweli itakuwa mtihani sheria tunayotunga jamani, naona Mwanasheria mwingine umesimama tutamalizia kwako tusonge mbele.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *line* yako ni sahihi sana, kwa sababu kama yale maneno ya Mheshimiwa Kanyasu yataingia hapa na hapa pana madhumuni yake na madhumuni ya msingi ni kutunzwa kwa hizi *financial and property management laws,* sasa hiyo hauwezi kujiwekea masharti ambayo kama atayavunja tena atachukuliwa hatua, kwa sababu sheria hii inasomwa na sheria zingine. Kwa hiyo, mimi nadhani sheria haiwezi ikatengenezwa katika misingi ya kufuata jambo fulani kwa sababu sheria zinasomwa *mutatis mutandis.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nikubaliane na wewe kwamba tukiache hivi hivi, ki-*flow* hivi hivi kwa sababu tutakapoyaweka yale maneno yatakuwa kama yanaanzisha jambo ambalo huyu anayetakiwa kulifanya, kimsingi atakuwa anajiwekea yeye mwenyewe tena tatizo na kweli hatakuwa tayari kufanya hivyo kwa kuwa linaweza kushughulikiwa na sheria nyingine, mimi nadhani hiki kiko sawa.

**MWENYEKITI:** Sawa, Mheshimiwa Kanyasu hoja yako imeeleweka, ungetamani kila chama kijiwekee utaratibu wa kudhibiti hizo fedha. Sasa ule utaratibu ukiwekewa hapa panakuwa kidogo siyo mahali pake, pengine kungekuwa na kifungu kingine mahali pa kupeleka lakini hapa ukiyaunganisha haya mawili kidogo inakuwa haileti ule mtiririko mzuri wa uandishi wa sheria pamoja na kwamba Serikali hawana shida. Nadhani watatazama huko mbele walete haya mapendekezo, wayawekee kifungu pahala lakini kuingia hapa kwenye (d) kidogo itakuwa ngumu katika ule utungaji tu wa kawaida *flow* inakuwa haikai sawa na pia inakuwa haihusiani na ile *opening party* ya hiki kifungu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Mheshimiwa Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba katika kifungu hicho pale kifungu cha (f) naomba yaingie maneno yatakayofanya vyama vifikirie kuweka kifungu ambacho angalau kinawezesha wale ambao wanateuliwa kwa ajili ya kugombea angalau asilimia 30 yao wawe ni wanawake, baada ya neno lile la mwisho kabisa ilipoishia *leaders*.

**MWENYEKITI:** Haya, Waheshimiwa nina uhakika tunapiga makofi kwa kusikia 30 *percent* lakini hapa mahali kinapotaka kuingizwa kifungu kinaangukia kwenye hoja zile zile nilizozitumia kwa Mheshimiwa Kanyasu. Yaani hapa inahusu *a registered political party shall at all times maintain the following documents: Rules for intra-party nomination of candidates and election of party leaders,* halafu uongeze *containing provisions to ensure...* Kama unataka hawa waweke hiki kawatake mahali pengine halafu ndiyo watakuja kutumia sheria hii kwamba haya ya 30 *percent* tutayakuta kwenye hii *document* iliyotajwa hapa, lakini hatuwezi sisi ku-*establish* juu ya kile ambacho ameombwa.

Waheshimiwa Wabunge, ni kama vile kitabu kiko hivi halafu wewe umeleta *cover* iko hapa juu. Kwa hiyo tukatafute mahali sahihi ambapo inabidi tuingize hiyo 30% *and then* chama kitakiwe sasa kwamba katika hizi *document* tutakapokuwa tunasoma hii *intra whatever* tukute na hii 30 % lakini sio kwamba tukute hii *intra party* halafu? Kwa hiyo hivi vifungu viwili vinaelekeana Mheshimiwa Manyanya. Kuna marekebisho mengine, Mheshimiwa Manyanya, karibu.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nikushukuru sana kwa jinsi ambavyo unatuongoza lakini unaweza ukaona kiu halisi ya jambo hili na hii kiu inatokana na kwamba Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Ibara ya 67(1)(b) kimesema kwamba huwezi kugombea kama

hujawa mwanachama wa chama fulani na uwe umependekezwa na hicho chama. Kwa bahati nzuri au ilivyo mpaka sasa niseme ni nzuri kwa sababu ni Katiba yetu, ni kwamba hatuna mgombea binafsi, kwa hiyo hakuna nafasi ya huyu mwanamke kujiamulia kwamba najipeleka nikagombee kama hujapitishwa na chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu kwenye hiki kifungu kinataka hivi vyama kutunza hizo *documents* lakini zisiwe tu *documents* kwa sababu huku mbele tumewaagiza hizo *documents* zioneshe *inclusion* zioneshe kwa mfano kwenye sera zao zioneshe kwamba zinaweka vipi makundi ya watu mbalimbali. Kwa hiyo iko hivyo, tukasema kwamba basi kwenye hizo *documents* isiwe tu bora *document* iwe ni *document* ambayo sasa kwa sababu vyama wamepata fursa kubwa yaani madaraka makubwa sana ya kuamua hata maisha ya watu ambao ni wanachama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ule uhuru huo kwa sababu unagusa maisha yetu tukasema kwa sababu hatuna sehemu nyingine kuingilia basi hapa hapa kwenye hiyo *document* yake iwe ina hivyo inavyotakiwa. Suala hili inawezekana ikaonekana kwamba labda tunatunga sheria wengine wanaweza kusema ya kibaguzi siyo ubaguzi kwa sababu kwenye Ibara ya 12 (5) kinatuambia ubaguzi haupo pale unapolenga kurekebisha mambo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Manyanya, hoja yako imeeleweka mahali unapotaka kifungu kiingie ndiyo siyo mahali pale. Siyo mahali pake kwa sababu yaani hicho unachokisema kinapaswa kuwa huko ndani tayari, sasa hatuwezi kukiwekea juu. Yaani kama tunaanzisha kifungu kwamba tuwatake hawa *intra-party* wawe na hiyo 30% *that is something else,* lakini kwamba hapa tulipoandika kwamba *document* zitakazokuwa *maintained* wa-*maintain document* hii halafu ndani yake kuwe na nini, aha tunatakiwa ndani yake tuwe tumeshasema pahala ili wanapotengeneza ziwemo, maana la sivyo itabidi twende kwenye kila kitu hapa, kuna vitu vingi. Mwanzoni hapa hamjapaona wamesema; *The parties' general policy which states the parties'*

*ideology including what else*. Haya *the parties' gender and social inclusion policy including what?*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu sasa tunataka *contents* ziwe na nini? Hizi *contents* hatuwezi kuzitakia hapa lazima tukazitakie *elsewhere* ila sasa kwenye *contents* ndiyo wawe wameweka hicho kitu, hatuwezi yaani kukipandishia juu sijui kama naeleweka? nadhani nimeeleweka lakini hoja yako imeeleweka ila mazingira ya hapa pa kuwekwa hiyo 30 *percent* ndiyo haiwezi kuingia hapo kwa utungaji wa sheria, pamoja na nia njema ya kwamba wote kwa kweli tunatamani hiyo idadi iongezeke.

Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 20

*(Ibara Mpya iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20

*Ibara Iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hichi kifungu cha 21 kwenye jedwali la 3(c) kwanza naipongeza Serikali kwa kuanzisha dawati la jinsia katika vyama vya siasa, lakini kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Vyama vya Siasa Msajili wa Vyama vya Siasa ndiyo mlezi wa vyama na tukirejea pia katika kifungu cha 6(a)(5) cha Sheria ya Vyama vya Siasa kimeelekeza vyama vya siasa kuzingatia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzingatia jinsia wakati wanatengeneza na kutekeleza sera, wakati wa uteuzi wa wagombea kwa ajili ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi wa viongozi wa vyama. Haya yote yamekuwa hayatekelezeki kikamilifu kwa muda mrefu na ndiyo maana hadi Serikali imekuja na hichi kifungu kipya cha 10(c) ambacho kinajaribu kuangazia maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nataka kupendekeza hapa ni kwamba, hili dawati ni lazima liunganishwe na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iweze kutekeleza jukumu lake kwa maana ya kwamba hivi sasa taarifa ambazo zitakusanywa kuhusiana na utekelezaji wa sera ya ujumuishi wa jinsia na makundi maalum pamoja na malalamiko ambayo yatakuwa yanapokelewa kwenye haya madawati yatabaki yana-*hang,* lakini ikiwa vyama vya siasa vinatakiwa kuwasilisha taarifa au ripoti kwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ina maana Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaweza kutekeleza hilo jukumu la kuangazia na kufatilia utekelezaji wa haya madawati ili madawati haya yawe na tija kwa sababu pasipo kufanya hivyo tunaweza tukajikuta malalamiko labda yanatolewa hayafanyiwi kazi lakini hakuna njia ya kuyafikisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pale kwa Msajili wa Vyama vya Siasa lipo Baraza la Vyama vya Siasa ambapo wanaweza wakajadili mienendo mizima yanayokusanywa kwenye dawati la jinsia ikawa agenda ya kudumu ili kuhakikisha hizi *document* zote ambazo vyama vya siasa vinatakiwa viwe navyo, kazi yote ambayo dawati

la jinsia inatakiwa lifanye zinafanyika kwa tija ili kukusudia lengo la kuanzisha dawati la jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiporidhika na maelezo ya Serikali nitatoa hoja na nitaomba Wabunge wenzangu waniunge ili tuweze kujadili.

**MWENYEKITI:** *Aaah! To be honest am not sure I was following.* Kuna tofauti gani kati ya kifungu chako unachopendekeza Mheshimiwa Neema na hichi kilichopo kwenye Muswada?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti iliyopo ni pale mwisho baada ya kusema *gender issues* iwekwe *comma and report to the Office of Registrar of Political Parties,* ili kuweka muunganiko baina ya dawati la jinsia na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iweze kupata taarifa ya mienendo ya malalamiko ambayo yanafikishwa kwenye vyama vya siasa namna ambavyo zinatatuliwa ikiwemo pia na utekelezaji wa sera ambazo wamejiwekea.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mifumo ya uendeshaji wa vyama vya siasa *it's a bit complex and tricky.* Kwa sababu sisi kama Serikali tuliona ni lazima kuwa na hii *basic provision* ambayo angalau itaangalia masuala hayo ya jinsia kwa ujumla kama tulivyoyaweka. Sasa tukisema hizi *complaints regarding gender issues* ziwe *connected* na Ofisi ya Msajili na kule kwenye Ofisi ya Msajili pia kwa sababu sheria yake na yenyewe inafanya kazi ya kuvisimamia hivyo vyama na imetengeneza kanuni za ufatiliaji za kifungu kimoja hadi kingine ambacho kipo kwenye sheria kama hiki tutakachokiweka leo, sasa ukisema utengeneze mfumo mwingine utavifanya sasa vyama vya siasa badala ya kufuata ile mifumo waliojiwekea kwenye Katiba ya nidhamu na maadili, kuwe na mfumo mwingine *parallel* ambao utatengeneza *shortcut,* kwa mtu kama *complaints*

haitashughulikiwa kwenye chama atakuwa anaenda sasa moja kwa moja kwa Msajili. Kwa hiyo mwisho wa siku hii mifumo miwili inaweza ikaji-*contradict,* na ikigongana tunaweza tukapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiria kwa sababu hili dawati tunataka kulianzisha sasa na tutakapolianzisha Vyama vya Siasa kwenye Katiba zao watatakiwa sasa kulitambua maana yake tumesema ni lazima…

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba hakuna mahala niliposema kwamba mtu atakayewasilisha malalamiko kwenye chama cha siasa aende moja kwa moja kwenye Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, bali nilichosema ni kwamba vyama vya siasa viwasilishe taarifa ya utekelezaji wa hicho kifungu, nilitaka tu kusahihisha hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tuelewane hapa vizuri, Mheshimiwa Neema anasema, *provision relating to gender and social inclusion desk for coordinating the implementations of gender and social inclusion laws and policies and handling complaints regarding gender issues and personal with disabilities issues report to the office of the Registrar of the Political Parties.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilichokuwa nataka kusema ni kwamba, sijui, labda nielewe kwanini waripoti kwenye Ofisi ya Msajili badala ya kufuata labda ile mifumo ambayo imewekwa ndani ya

Chama ya kushughulikia masuala ya maadili? Kwa sababu kama haina shida hiyo, labda kama tuna shida na hiyo mifumo ambayo imewekwa kwenye Chama…

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kuna taarifa nyingine. Mheshimiwa Swalle.

**TAARIFA**

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa heshima na unyenyekevu sana nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri ambaye anafanya kazi nzuri sana siku ya leo humu ndani, anastahili maua yake sana Mheshimiwa Waziri Mhagama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni kwamba kama nimeelewa pendekezo la Mheshimiwa Neema Lugangira, anataka ku-*establish check and balance* kwamba hii *policy* ilivyo, iko *within the party,* hakuna mtu ambaye anafanya *scrutiny*. Kwa hiyo, nafikiri malengo ya mtoa hoja ni kwamba Chama baada ya kufanya hayo mambo yake, kiwe kinatoa pia taarifa kwa Msimamizi na Mlinzi wa Vyama vya Siasa. Ni hivyo ndivyo nilivyomwelewa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Hoja iko hivi, hii *third schedule* inasema hivi, "*made under section* 10(c), *basic provisions to be contained in the gender and social inclusion policy of a political party.*" *That is all, nothing more, nothing less*. Yaani hii inasema, mambo haya yaliyoandikwa (a), (b) na (c) yawemo kwenye ile sera inayohusu mambo haya. Sasa haya mengine tunayoyatafuta wakaripoti, wakaripoti wapi Mheshimiwa Neema? Kwa sababu hizi ni *contents* za ile *policy,* ndiyo zinazoangaliwa hapa, kwamba kwenye hiyo *policy* mtakayoweka wekeni na mambo mengine, lakini haya yasikosekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wewe. Msingi wa hoja yangu ni kwamba hapa tunajadili vifungu ambavyo vimeletwa na Serikali, lakini tukienda kwenye sheria ilivyo, pale kwenye vitu ambavyo vinatakiwa visomwe kwenye Katiba za Vyama vya Siasa suala la ujumuishi wa jinsia na makundi maalum halipo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ndiyo limewekwa hapa kwenye (c). Si ndiyo kuna *social inclusion! Gender and social inclusion.*

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imewekwa kama sera, lakini siyo kwenye Katiba za Vyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuelewa kwa jinsi ulivyoelewesha, nami lengo zima la kutoa hili pendekezo ni kuhakikisha kwamba hilo Dawati la Vyama vya Siasa litafanya kazi kwa tija na lazima kuhakikisha kwamba kuna ufuatiliaji.

**MWENYEKITI:** Sawa. Tunaenda pamoja kabisa na wewe. Hoja ni kwamba, haya maneno yanayoongezeka kwenye hii (c) ni kwamba hii *policy* si tumesema wawe nayo wale? Yaani hii ni *contents* za ile *policy,* wawe nayo. Wakishakuwanayo maana yake si ndiyo wametakiwa huku na (10) kwamba wa-*maintain* zile *documents,* lakini tumeamua *documents* nyingine wekeni, ila hii ya jenda tunataka tuwawekee kabisa *contents* zake hizi hapa, ziwe na *inclusion* ya sura hii. *That is all*. Hoja ya wataripoti wapi, kwa sababu hapa hatuja-*establish* utendaji kazi wowote. Hapa tumesema tu ile *policy* yao iwe na vitu gani ndani? Ndiyo hoja iliyopo hapa, sijui kama nimeeleweka Waheshimiwa?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatokea wapi?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeeleweka. Kwa hiyo, naomba kuiondoa Mezani. Ahsante.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado sijaelewa…

**MWENYEKITI:** Tutaeleweshana tu. Endelea na kuna mabadiliko yako hapa, kwa hiyo, yalikuwa yanafuata ya kwako, karibu. Kwa hiyo, endelea na ya kwako, unaweza kuunganisha na ambayo ulikuwa hujaelewa.

**TAARIFA**

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimesimama kwanza kwenye hoja ya Mheshimiwa Neema kwamba mimi bado nina hoja kwamba hoja yake haikupaswa kuondolewa, kwa sababu yeye alikuwa anazungumza *scope* ya hicho ambacho kinapaswa kuwemo kwenye *policy*. *Scope* kwamba wasiishie pale walipoishia hiyo *policy* ifike mpaka pale kwenye kutoa ripoti. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba hakuna sababu ya kuondoa hoja yake ambayo aliweka Mezani kwako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ngoja twende pamoja hapo kwenye (c). Uko hapo eh!

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** *Yes,* Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Hebu soma. Soma Kifungu kilivyo kwenye hii ya Serikali, kwenye Muswada kwa maana hiyo.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, (c) "*the provisions…*"

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa anzia hapo juu kwenye hayo maneno yenye herufi kubwa halafu ruka nenda kwenye (c).

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** "*Basic provisions to be contained in the gender and social inclusions policy of a political party*." Sasa (c) inasema: "*provision relating to gender and social inclusion desk for*

*coordinating the implementations of gender and social inclusion laws and policies and handling complaints regarding gender issues.*" Kwa hiyo, akataka aongeze, "*and report those issues to the other authority.*"

**MWENYEKITI:** *Okay. Why would you single out only* (c)? *If you want the report to be taken to the Registrar of Political Parties, why would you want just a party of the policy to be taken to the Registrar of Political Parties and not the entire policy?*

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimeelewa, mtoa hoja hana tatizo na *reporting* ya *part* (a) na (b). Yeye anataka tu *reporting* kwenye *issue* ya *gender* kwenye (c).

**MWENYEKITI:** Sasa hoja iko hivi, (a), (b) na (c) zote ni *contents* za *policy*. Twende kwenye (b) ama twende (a), inasema hivi: "*basic provisions to be contained in the gender and social inclusion policy of a political party,* (a) *provisions relating to programs for promotions of gender and social inclusions.*" *Why wouldn't you want that to be reported to the Registrar of Political Parties? And* (b) "*provision relating to programs for capacity building for women, youth and persons with disability to become leaders in or outside the party.*" *Why wouldn't you want that information's to go to the registrar?*

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nadhani kwa hoja yako, kama dhamira ni hiyo, maana yake vifungu vyote labda angependekeza viwe *reported*.

**MWENYEKITI:** Ni kwa sababu gani unajua hajapendekeza na ndiyo maana amekubaliana na hoja yangu Mheshimiwa Neema, hapa juu tumesema, *third schedule made under section* 10(c); *so, we go to* 10(c), 10(c) inasema: "*a fully registered political party shall at all times maintain the following documents.*" Hizi *documents* zote Chama kinapaswa kuwanazo, ila tumeamua zinazohusu *gender and social inclusion* tuziwekee *schedule*. Ndiyo tumeweka *schedule* hapa kwamba, jamani eeh, nyingine zote tengenezeni, ya *gender*

kaangalieni kule *schedule,* ndiyo *contents* zake lazima ziwemo. *That is all. (Makofi)*

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani niondoe *jam.* Nimeelewa kimsingi. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Shukrani.

Waheshimiwa Wabunge, hii 21 ilikuwa pia na marekebisho. Mheshimiwa Neema kwanza alikuwa na marekebisho mawili. Siyo! Kabla hatujaenda kwenye marekebisho ya Serikali, Mheshimiwa Neema kwenye Kifungu hiki alikuwa na hoja nyingine ukiacha hii ya (c), sasa nampa nafasi kwenye hii hoja yake nyingine. Mheshimiwa Neema Lugangira. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye hii hoja napendekeza kwamba kiongezwe kifungu kidogo cha (d) pale kwenye Ibara ya 21. *Third, schedule* iongezwe Ibara ndogo hiyo ya (d) ambayo sasa isomeke: "*provisions that ensure gender consideration during intraparty candidate nominations by at least thirty percents*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la pendekezo hili ni kwamba Sheria ya Vyama vya Siasa kwenye *section* 6(a) (5) inasema kwamba vyama vinatakiwa kuhamasisha ujumuisho wa jinsia na kuzingatia makundi yote katika uteuzi wa wagombea ambayo ni (a) halafu (b) ni uchaguzi wa viongozi ndani ya Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ambacho kipo kwenye sheria katika hii *section* 6(c), (a) (5), kwa muda mrefu kimekuwa hakitekelezeki ipasavyo, ndiyo maana hadi hivi sasa tukiangalia uwakilishi wa wanawake, Wenyeviti wa Vijiji ni asilimia 2.1, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ni asilimia 12.6, Wenyeviti wa Vitongoji ni asilimia 6.7 na Wabunge wa Majimbo Wanawake ni asilimia 9.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa muktadha huo, ninachojaribu kupendekeza hapa ni kwamba Vyama vya Siasa viwe na mfumo ama vifungu ambavyo vitaonesha namna gani ambavyo teuzi za wagombea katika uchaguzi wa ndani ya Vyama vya Siasa zitaweza kuzingatiwa kwa asilimia 30 kwa maana ya jinsia zote, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahaa, hebu toa mfano, watu wanagombea, Wenyekiti labda wa chama; nikitaje Chama gani jamani? Chagueni. Chama gani?

**WAJUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jahazi Asilia.

**MWENYEKITI:** Jahazi Asilia. Ehee, tolea mfano wa chama kimojawapo, nafasi mojawapo ili niipate picha. *(Kicheko)*

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie mfano labda kuna hicho Chama cha Jahazi ulichosema, kuna uchaguzi wa kwenye Kata labda Udiwani Kata, halafu wamejitokeza watu ambao wamechukua fomu labda 20, na hicho Chama cha Jahazi katika kanuni zilizojiwekea na katika Katiba yake ni kwamba labda ikiwa nafasi ni moja watachaguliwa labda wagombea watatu au wanne; tuchukulie labda watatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika wale 20 ambao walichukua fomu, walikuwepo labda wa jinsia Ke na Me. Sasa Chama katika kuchagua wale wagombea katika hiyo *intraparty* ya uchaguzi, yaani wanapofanya ile *selection* kama ni watatu, wafanye kwa kuzingatia jinsia. Kwa hiyo, *at least* pale ambapo kuna mwanamke ambaye ana vigezo ambavyo vinatakiwa, basi naye aweze kupata fursa ya kushindana. Kwa sababu kwa jinsi ilivyo, mara nyingi unaweza kukuta jinsia moja yaani anakoseshwa fursa ya kushindana. Hicho ndiyo nilikuwa namaanisha kwa mfano wa muktadha wa huo.

**MWENYEKITI:** Haya. Nadhani haya mambo yalikuwa na semina nyingi, bahati mbaya sijahudhuria hata moja. Tuendelee kueleweshana jamani, nielewesheni vizuri, hiyo inasaidiaje kwenye kumleta mwanamke kwenye uongozi? Tuitungie sheria hapa, *how does it help?* Jamani mmeielewa hoja? Akina mama, akina baba, wa *he for she* mmeelewa hoja? *(Kicheko)*

Sawa. Basi naona wote mmenyamaza, ngoja niwaambie mimi nilivyoelewa. Mimi nimeelewa kwamba, Mheshimiwa Neema anataka katika hii *gender and social inclusions policy* ya chama cha siasa mle kwenye ile *policy* yao waweke pia mambo yanayohusu uteuzi wa wagombea ndani ya chama kuwa kwa angalau asilimia 30. Si ndiyo! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnajua ile asilimia 30 iliyoko kwenye Katiba imefanya kazi, ni kwa sababu ile asilimia 30 haipelekwi kugombea na wanaume. Tunagombea wenyewe, yaani peke yetu akinamama. Hii nyingine tukiweka kwa mfano hapa, si tunataka kuweka! Maana hatutaki tu kuweka, tunataka kuweka kwa ajili ya kuongeza idadi ya wanawake kwenye nafasi za uchaguzi. Si ndiyo jamani! Hii ya kusema wanaume wameteuliwa wawili, mwanamke lazima awepo mmoja, inatuongezeaje idadi ya wanawake? Haya, kwenye hoja hii mimi sina *heart feelings. (Kicheko)*

Mheshimiwa Mushashu. Mheshimiwa Mushashu kisemeo hakisemi?

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakibonyezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijibu pale uliposema kwamba itaongezaje namba za wanawake? Ukiangalia Miswada yote tuliyopitia na hii ya Vyama vya Siasa, tumechangia humu kwa wingi wetu kwamba labda tunashindwa kuwapata wanawake kugombea kusudi tuje kuwapata kwenye hizo nafasi za uongozi kwa sababu hawateuliwi na vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka tuweke *provisions* hapa kwenye Vyama vya Siasa, wahakikishe kwamba wanapoteua wale wagombea, wahakikishe kwamba wale walioteuliwa *at least 30 percent* ni wanawake, kwa sababu wanaweza kuamua kuchagua jinsi moja. Sasa sisi tunasema ili waweze kuwemo kwenye mchakato, lazima wateuliwe. Kwa hiyo, wateuliwe kiasi gani? Siyo chini ya asilimia 30. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Mushashu, ngoja tuelewane vizuri. Hii ni *intraparty,* maana yake ndani ya Chama. Maana yake ndani ya chama wakati tunaenda kupigiwa kura tuseme za maoni, wanawake wanaweza kuwa wote watatu, lakini angalau mmoja awe mwanamke, si ndiyo! Wanaweza kuwa wawili au watatu. Sasa tufanye ni mmoja ndani ya chama, halafu ikatokea kwenye Kata, maana ndiyo mfano uliotokea. Kwenye Kata zile kura za maoni zimepigwa, huyu mwanamke kawa namba tatu na mbili, tatu na mbili kila mahali walikopelekwa. Hii inatofautisha vipi na *thirty percent* ya kukiambia chama kwamba wale mnaowateua; kwa sababu wewe umeleta hoja mpya kama nimekuelewa vizuri. Kwa maana ya kwamba, wanapoenda kugombea tuseme Majimbo kwa mfano, siyo yako 264, kila chama kinapoenda kusimamisha 264 kiwe na asilimia angalau 30 kwenye wale 264. Kama nimeelewa hoja vizuri Mheshimiwa Mushashu. Nimekuelewa vizuri au hapana?

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nirudi kwenye ngazi ya Jimbo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ngazi ya nini?

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nirudi kwenye hiyo ngazi ya Jimbo moja.

**MWENYEKITI:** Ehe!

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanateuliwa watu wa kwenda kugombea Ubunge wa Jimbo,

badala ya kupendekeza labda majina ya wanaume watatu peke yao, tunataka wale ndani ya Jimbo kati ya wale watatu watakaopendekezwa kusudi kupelekwa mbele ya watu wachague mmoja, *at least thirty percent* wawe wanawake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kila chama huwa kinateua mmoja. Sasa ndani ya chama ndiyo ilikuwa hoja ya Mheshimiwa Neema, kwamba ndani ya chama chako, watu wawepo watatu, mmoja angalau awe mwanamke. Kule nje ndiyo kunakoleta watu, ndani ya chama kunaletaje watu? Maana hii ni *intraparty*.

Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nifafanue.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa fafanua tu.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ni kwamba tunachosema hakihusiani na chama kile ulichosema Chama Y, kimteue kuwa…

**MWENYEKITI:** Taja hata Chama cha Mapinduzi maana ndiyo tuko humu ndani.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatusemi kwamba Chama cha Mapinduzi kwa sababu tu labda wametokea wanawake labda katika wale watatu kwamba lazima kimteue mwanamke. Tunachosema ni kwamba, katika ule ushindani wa kura za maoni, ndiyo pale vyama viweke huo utaratibu kwamba katika zile kura za maoni wanawake wapate fursa ya kugombea ule uchaguzi wa ndani, ni njia moja ya kujengea uwezo wanawake, yaani waweze kujitokeza kugombea, siyo kwamba kuteuliwa kuwa wagombea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MJUMBE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ni nani aliyesema taarifa? Mliosimama mko wengi. Aliyesema taarifa ni nani? Wengine nadhani wanataka kuchangia. Mheshimiwa Swalle halafu Mwenyekiti.

**TAARIFA**

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nitoe taarifa kwenye ambacho amesema Mheshimiwa Neema. Msingi wa hoja yake, labda kidogo niwarudishe kwenye sheria ambazo tunazo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii sheria ya *Political Parties Act*, kile kifungu cha 6(a)(5) unakuta kimetoa wajibu vyama ku-*promote gender, that is number one*. Hawa waandishi wa sheria walikuwa makini sana, hawakuishia hapo. Walipotuleta kwenye *amendment* ambayo imechukua muda wetu mrefu hapa ku-*discuss,* wameamua kuanzisha kifungu kipya, kifungu cha 10(c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo ambayo wamesema katika Kifungu hiki. Kwenye (c)(1)(b) wanataka vyama view na *gender and social inclusion policy*. Hawajaishia hapo wamekuja kwenye jedwali jipya kwenye 21(e) ambako huku na kwenyewe, kwenye (a) wameweka tena wajibu mwingine. Vyama viwe na *programs* maalum za ku-*promote gender, number two* wamewataka vyama wawe na *program* za kufanya *capacity building* kwa *gender.*

**MWENYEKITI:** Sawa, twende kwenye 30%.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja ya Mheshimiwa Neema ni nini? Wakishafanya mambo yote haya, matokeo yake tutayapimaje? Ndiyo wanasema, tuongeze kifungu (d) kinachosema wawe pia na kifungu ambacho kinasema wakishahamasisha hawa wanawake, angalau 30% wagombee ndani ya Chama kwenye *nomination* yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wateuliwe kwa ajili ya kwenda kwenye kura za maoni ndani ya chama. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Wateuliwe kwenda kwenye kura ya maoni ndani ya chama. Haya Mheshimiwa Dkt. Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nizungumze kwa niaba ya Kamati yetu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunakaribia kurejea kwenye Bunge lingine.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ilifika mbele ya Kamati na tuliipima. Tukaangalia uzoefu wa kura za maoni ndani ya Vyama vya Siasa na tukaona hoja hii haiwezi kutekelezeka kwa sababu, Uchaguzi natolea mfano kama Chama chetu cha Mapinduzi Uchaguzi wa 2015, kwenye Jimbo langu kulikuwa na wagombea 10 sijui walikuwa 30. Hakuna mwanamke au mwanaume ambaye alizuiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna uchujwaji, kwa hiyo, hatuwezi kutengeza sheria ambazo tutashindwa kuzisimamia, kwa sababu kwenye hivyo Vyama vya Siasa inategemea mazingira ya wakati ule. Tunakwenda kwenye kura za maoni uchaguzi ujao. Hatujui tutatumia mfumo gani, watachuja wagombea waje watatu au wataacha wagombea wote tukachujwe na wapigakura? Kwa hiyo, sisi tuliona hili jambo kwa sasa halitekelezeki na hatuwezi kulitengenezea sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, baada ya Mwenyekiti kuzungumza naona bado kuna watu wawili wamesimama. Jamani tumalize saa 10.30 hii na Bunge linalokuja linaanza saa 11.00. Sijui kama wote mna misuli humu ndani, maana hii inaunganishwa mpaka saa 2.00 usiku.

Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nadhani dhamira ya aliyeleta marekebisho ya kifungu hiki ni kwamba kile Kifungu cha Sheria, Kifungu cha 6(a)(5) katika Sheria ya Vyama vya Siasa. Kinaweka msingi wa Vyama vya Siasa kukuza Usawa wa Kijinsia.

**MWENYEKITI:** Twende kwenye kifungu alichopendekeza, 30%.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes!* Kwa hiyo, msingi ule ambao umewekwa kwenye sheria, nadhani anachokusudia lazima uonekane kwenye michakato ya kisiasa. Kwa hiyo, yeye anachopendekeza ni nini *minimum threshold*…

**MWENYEKITI:** Hii imeshaeleweka Mheshimiwa, tusaidie tuanzie pale alipozungumza Mwenyekiti. Kwa chama ambacho kimejiwekea utaratibu kwamba, kila anayechukua fomu nendeni wote mkapigiwe kura. Hiki kifungu wao watakitekelezaje wakiweka kwenye *policy* yao, watakitekelezaje? *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaweza kwa sababu inabidi wazingatie *minimum threshold.* Kwa hiyo sheria ikianza wao wata-*comply.*

**MWENYEKITI:** Ngoja, ili tuwe tumeelewana vizuri. Mimi Mbeya Mjini ndani ya Chama cha Mapinduzi, tulikuwa wagombea 33. Wote 33 tuliwekwa kwenye ile karatasi ya kura za maoni. Pale kila mtu ali-*tick* anayemtaka, wala hakukuwa na mchakato wa chama sijui kumuondoa nani hawakutoa yeyote. Mazingira hayo hii *policy* yetu hapa ya kwamba, *provision that ensure gender consideration during*

*intra-party candidate nominations, supposed a particular party doesn't do nominations, they only do it once*. Hii 30% tutaipataje? *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani msingi ni kuenndelea kuhamasisha usawa wa kijinsia na uanze kuonekana kwenye michakato ya kisiasa.

**MWENYEKITI:** *Super!*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumalize nimewaambia pale tunaunganisha Bunge hili. Mnaona muda ule? Mko tayari *eeh?*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Naomba nitoe ufafanuzi kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Manyanya. *Naam! (Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, tunashukuru kwa hii *debate*. Niseme kwamba, nadhani huu mkanganyiko ni wa namna ya kulizungumzia lile jambo na imetokana na tunavyotumia mifumo ya aina tofauti. Lengo kamili ambalo mimi nimeliona hapo lilikuwepo ni ndani ya chama katika kumtoa mgombea kwenda kushindana na wagombea wa vyama vingine. Hapo ndiyo nadhani lengo lilikuwa ni hilo.

**MWENYEKITI:** Kama lengo ni hilo halitaweza kuingia hapa kwenye *Political Parties' Affairs Laws Amendment*. Ilipaswa iingie kule kwenye sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kwa

sababu tukiingiza hapa ni kule kwenye vyama. Je, ni chama gani hicho ambacho kitateua?

Nimeuliza hapa wakati Mheshimiwa Mushashu anazungumza ili tuwe tunaongea *holistically* kwa sababu tukitengeneza sheria hatufanyi masihala. Ndiyo maana tumekaa hapa kuanzia asubuhi. Kwa kweli, Wabunge kila mtu yuko *serious* kweye jambo hili. *(Makofi)*

Sasa tunapotunga sheria ya namna hii mtakumbuka mwanzoni wakati tukitunga ile sheria nikasema je, siyo kuingilia kwenye vyama? Ni chama gani ambacho kitaambiwa hivi wale unaoenda kuwasimamisha kwenye majimbo hakikisha wako *a minimum of 30%* ama *even 50%*. Ni jimbo gani wataambiwa ninyi kwa sababu wenzenu wa jirani wamechagua mwanaume, ninyi chagueni mwanamke. *(Makofi)*

Hoja maana yake ni nini? Hizi *provisions* zilizowekwa hapa Waheshimiwa Wabunge ya kuvitaka vyama vihamasike, vihamasishe wanawake, vijana, watu wenye ulemavu. Hoja ndiyo hiyo vihamasishe (viwe na hizo programu za kuwafanya wawe na utayari wa kwenda kugombea). Hapa tunapotaka kuiweka na taratibu za vyama ziko tofauti na sisi wenyewe humu ndani tunakiri kwamba, ziko tofauti. Tukishaweka hapa maana yake ni nini?

Mheshimiwa Keisha nadhani nilisema tumalize hapa. Mheshimiwa Khadija Taya.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo wangu nilichokuwa nataka kukisema ni kwamba, sisi hapa tunatunga sheria na mlengo wa dunia sasa hivi ni kumnyanyua mwanamke na vijana na watu wenye ulemavu. Kama tukitengeneza sheria hapa kwamba, Vyama vya Siasa vinatakiwa *view* na mtazamo huu. Ni vyama vyenyewe vitaweza kuhangaika na kutafuta hao wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa sababu, lengo ni kukuza uwezo wa hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke akuzwe, kijana akuzwe na mtu mwenye ulemavu akuzwe. Kwa hiyo, jambo la hao wanafanyaje au linatekelezeka au halitekelezeki ni wao sasa kwenye vyama waamue lakini sisi sheria tuitengeneze hapa.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Nyongo.

**TAARIFA**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, twende mbele turudi nyuma tunatengeneza sheria na sheria lazima tutunge sheria inayotekelezeka. Vyama vya Siasa katika kutafuta kuongoza ni kwamba kila chama cha siasa kinaitafuta Serikali. Kinatafuta kwenye ngazi ya chini kwa maana ya Udiwani, Ubunge na Urais. Mwisho wa siku tunakwenda kwenye *competition* ya kwenda kuomba kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tunakubaliana na Vyama vya Siasa kumuwezesha mwanamke au *gender* yoyote lakini, tunapoingia kwenye kufanya *nomination* ili twende kwenye uchaguzi kwa maana ya mashindano. Kila chama cha siasa kitaangalia nani anafaa katika eneo lake. Awe mwanaume awe mwanamke, anayekubalika ili watu wamchague chama kiweze kuongoza. Sasa ukiweka sheria ya kulazimisha kwamba Jimbo a na Jimbo b lazima awe mwanamke au mwanaume, Vyama vya Siasa haviwezi kutekeleza hilo.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ule utaratibu wa kwamba, Katiba inaeleza wanawake lazima 30% wawemo. Huo ni utaratibu ambao unafanywa na Vyama vya Siasa kuchagua wanawake uendelee kutekelezwa na vyama vya siasa viendelee ku-*promote* wanawake na makundi maalum. *Once*

inapofika kwenye uchaguzi wamchague wanayeona anafaa kwenda kupigiwa kura na waweze kushika Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tulimalize hili, Katiba imeweka msingi imara kabisa. 30% ya Wabunge Wanawake tulionao humu ndani wanatokana na ile ya kwenye ya kwenye Katiba. Namna pekee imeweza kutekelezeka ni kwa sababu ni sehemu ya *affirmative action,* ni kwa ajili ya wanawake pekee. Hii tunayoweka hapa, mmesema dunia nzima. Jamani mimi ndiyo Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. *(Makofi)*

Kama kuna mtu anatamani wanawake wawe wengi Bungeni, mimi ni mmojawapo. Katika kutamani kwangu huko siyo kwa kuweka jambo ambalo kwa sasa hivi sheria zinazohusika hatujazisema kule. Pia ndani ya chama, sisi hapa tumeshasema kila chama kina utaratibu wake. Wengine kuna mmoja ni mmiliki wa jimbo na wananchi wanamkubali kama yeye ndiyo mmiliki wa jimbo. Vyama vingine gombeeni hata 300 mtapigiwa kura wote. Vyama vingine wewe ndiyo peke yako unagombea.

Sasa tukisema hawa watu watakiwe maana yake hapa tunatengeneza utaratibu mwingine wa vile vyama vikaseme nini kule. Je, hii *forum* ya sasa hivi hapa ndicho tunachotaka kukipata? Mkishanijibu hapo tusonge mbele jamani.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa msingi wa majadiliano na jinsi ambavyo umetuongoza kwa nia ya kuendelea kujielimisha. Endapo ikibaki kama ilivyo bila *percentage* itakuwa ni sawa au itakuwa siyo sawa?

**MBUNGE FULANI:** Ni sawa.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili tu ya kuelewa nilitaka kufahamu.

**MWENYEKITI:** Sawa ama siyo sawa. Sijaelewa swali lako.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kufahamu kwenye hii sentensi ilivyoandikwa *provision that ensure gender consideration during intra-party candidate nomination,* ikiishia hapo itakuwa ni sawa au siyo sawa katika lengo la kuelewa?

**MWENYEKITI:** Hapa inabidi tuweke kwamba chama ambacho kinakuwa kinafanya *nomination.*

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** *Okay!*

**MWENYEKITI:** Maana yake lazima uweke hayo mazingira. Si tumeelezana hapa jamani kwamba, kila chama huwa kinaamua. Kingine hakifanyi nomination. Sasa hii provision tutalazimisha vyama kwenda kufanya nominations? Nia ni njema lakini hiyo nia yetu njema…

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Mimi nimekulewa nilitaka tu kuuliza jambo jingine. Sisi kama Wabunge tunavyotoa maoni yetu hapa, je ni sawa kuambiwa na Mbunge mwingine kwamba umeleta hoja za shirika fulani?

**MWENYEKITI:** *Eeh!*

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoka hapa Mheshimiwa Shangazi amekuja kuniambia hivyo. Kwa hiyo nataka kujaribu kuelewa je ni sawa?

**MWENYEKITI:** Jamani hizo hoja nyingine huwa zinajibiwa wakati wa Bunge, siyo wakati wa Kamati. *(Kicheko)*

Haya, Waheshimiwa Wabunge. Hoja ya kuweka huu msingi ni kwa sababu kwanza tuelewane Waheshimiwa tumalize hili. Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Hatutaweza kutunga sheria kwenye haya mabadiliko tunayotaka kuyaweka kwa sura ambayo itapeleka ujumbe tofauti kwenye sheria ambazo zipo tayari tumeshatunga hapa Bungeni.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo lengo na kwa sababu nia yetu wote ni kuongeza idadi ya wanawake tuendelee kupigania hiyo hoja yetu ya kuongeza wanawake. Ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanawake wengi wanashiriki. Sasa chama kitakachoamua kutumia *nomination* au hapana mimi nisingependa kwenda kuvitengenezea sheria kila chama namna kinavyoendesha chaguzi zake huko ndani, kwa sababu kwa sasa hapa siyo sehemu yangu ya kutengeneza hayo.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Neema aliuliza kama ni sawa kuweka hapa hiyo *percent* ama tukiitoa je, itakuwa ni sawa? Yenyewe itabidi tukirekebishe kifungu pengine tuseme, kwa chama kinachotumia utaratibu wa *nominations* ndiyo kiende na hii hapa. Kwa chama ambacho hakitumii maana yake wanawake, watu wenye ulemavu kila mtu anaruhusiwa kwenda. Sasa lile la pili kidogo kwa sababu sijamsikia Mbunge anashindwa kulitolea maelezo lakini *just calm down.*

Haya, Waheshimiwa Wabunge nadhani tumeelewana. Nyinyi mnafahamu kwenye hoja za wanawake niko vizuri. Kw ahiyo kifungu hiki kwanza, ningetamani hata wangekuwa zaidi, hata wangesema 50% hata 70%, kwa nini iwe 50%? Wanaume wanaweza wakawa 90%, sisi tukawa 10% na mambo yakaenda. Kwa hiyo hata wao wanaweza wakawa 10% sisi tukawa 90%. Kwani lazima iwe 30% siyo lazima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mazingira kidogo yananipa ugumu wa kutengeneza hayo masharti hapa. Sisi sote tuendelee huko kwenye vyama vyetu kuhakikisha mambo yanakaa vizuri na hatuleti hii mikanganyiko. Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo na hapa tulikuwa

tumeshawasikiliza Waheshimiwa wote wenye marekebisho yao. Sasa ngoja nitazame niliyoambiwa kwamba, ni ya Serikali. Ni yapi hayo jamani? Katibu yako wapi ya Serikali kwenye hiki kifungu?

Sawa, Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 21kina marekebisho ya Serikali, wanaongeza neno *initiatives* baada ya neno *programs*. Haya, kwa hiyo tukatumie hizi *programs and initiatives* kwenye ku-*promote gender and social inclusion*. Poleni sana kinamama jamani. Naona wamama wanasikitika kama vile hivi Spika tupo naye ama vipi? Msiwe na wasiwasi tuko wote na Bunge lijalo wanawake watakuwa wengi humu ndani. *(Makofi)*

Siyo kwa lengo la kuwatoa wanaume hapana, wanaume mtakuwepo lakini wananwake tutakuwa wengi pia. Msiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapendekezo ya Serikali ya kufanya *re-numbering* baada ya kuongeza vile vifungu viwili.

**MWENYEKITI:** Haya, mabadiliko ya kubadilisha namba za vifungu yanaafikiwa?

*(Mabadiliko ya mpangilio wa Ibara yaliyopendekezwa na Serikali yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea. *(Kicheko)*

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuketi. *(Makofi/Kicheko)* Waheshimiwa Wabunge usikivu. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na kwa mujibu wa Kanuni ya 102(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2020. Naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima, imeupitia Muswada wa Sheria ibara kwa ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2023 *(The Political Affairs Laws (Amendment]Bill 2023)* kama ulivyorekebishwa au kubadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa ya mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws (Amendment]Bill 2023)*.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa, kwa lengo la kuimarisha nafasi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kama Msimamizi wa mwenendo ya Vyama vya Siasa pamoja na kuimarisha uzingatiaji wa Sheria na Kanuni katika Shughuli za Vyama vya Siasa**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu kwa kusoma mara ya tatu maana yake sisi tumeshakamilisha kazi yetu ya kutunga sheria. Kwa hivyo, tutampelekea Mheshimiwa Rais ili aweze na yeye kuweka saini.

Nitumie fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Ofisi yako nzima. Nawashukuru sana kwa kuzileta sheria hizi Bungeni lakini pia kuwa wasikivu kwa maoni yaliyotolewa na Wabunge na wadau mbalimbali. Mmetoa ushirikiano mkubwa sana, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii mmefanya kazi nzuri sana, tunawapongeza na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote mmetoa michango ya maana, mizito na kwa kweli imeonesha namna ambavyo mliwasilikiliza wadau mbalimbali ambao walileta maoni yao na kwa kweli hayo maoni mmeyatendea haki, mmeyaleta mbele ya Bunge. Bunge mengi limeweza kuyafanyia kazi na yale ambayo hayakufanyiwa kazi kipindi hiki, basi yataweza kufanyiwa kazi huko baadaye.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mmefanya kazi buwa sana na nawashukuru sana. Pia kwa uvumilivu kuendelea kuwa humu ndani tangu tulipoanza Bunge saa tatu mpaka sasa. Utayari wenu, kwamba mpo tayari tunaendelea sasa na shughuli nyingine mbele lakini mambo manne kwa haraka ambayo wadau walikuwa wameyasema sana na Serikali ilikubaliana na Kamati mambo haya lazima yasemwe kwa ufupi kabisa.

Kwanza, ni Tume yetu ya Taifa ya Uchaguzi, Rais atakaposaini Muswada huu tukimpelekea sasa itakuwa ni Tume Huru ya Uchaguzi ya Taifa. Neno huru lilisisitizwa na siyo tu neno huru pia na mambo mengine sasa yaliyoingia kwenye sheria hii, yanaashiria kwamba, mambo yale ambayo yalikuwa yamezungumzwa na wadau mengi yamefanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mojawapo lingine ambalo ni la pili. Ni kuhusu Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti sasa hawatateuliwa moja kwa moja na Mheshimiwa Rais na sasa watapendekezwa kwa Mheshimiwa Rais na Kamati ya Usaili. Kwa hiyo, ni jambo ambalo wadau walilisema sana na Serikali imelifanyia kazi.

Jambo lingine ni Wakurugenzi kuwekwa kwenye sheria kwa maana ya kusimamia uchaguzi sasa imetoa mwanya ama mawanda mapana zaidi ya nani wanaweza kuteuliwa kuwa wasimamizi wa chaguzi katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

La mwisho ni kuhusu Tume ya Uchaguzi kusimamia chaguzi zote nchini. Kwa hiyo, hili nalo ni jambo ambalo wadau walilisema sana na muhimu likasikika kwamba limefanyiwa kazi na upande wa Serikali. Tunawashukuru kwa kweli kwa ushirikiano mliouonesha. Wahesnimiwa Wabunge mmefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Sasa kwa utaratibu wetu Bunge huwa linaanza kwa muda, hatutaweza kuendelea sasa hivi kwa maana ni saa Kumi na Moja kasoro robo. Kwa hiyo, inabidi tuanze saa 11:00 kama ilivyoada na mimi sina maneno ya kuendelea kuzungumza hapa mbele mpaka

ifike saa kumi na moja ili tuendelee. Kwa hiyo, tutapata hayo mapumziko ya dakika kumi hapo, halafu Bunge litaendelea baada ya hapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Bunge mpaka saa kumi na moja kamili, muda mfupi ujao. *(Makofi)*

*(Saa 10.47 Jioni Bunge Lilihairishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 5) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa Dkt. Eliezer Feleshi aje asome hoja yake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa misingi ya haki, malengo sahihi, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Dhamira yake njema, weledi na uzalendo wake tunauona dhahiri kupitia miswada inayowasilishwa na Serikali Bungeni na kwenye hatua ya ukamilishaji wa kazi hizo yeye akiwa sehemu ya Bunge. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, (Mbunge), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vyema vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuishauri na kuisimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Balozi Profesa Kennedy Godfrey Gaston kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bwana Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa umakini wa hali ya juu na kusikiliza, kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali kupitia wadau wote waliohusika na sheria zilizopendekezwa kurekebishwa imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2023)* unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria nne zilizoainishwa katika Sehemu ya Pili hadi Sehemu ya Tano ya Muswada. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utekelezaji wa masharti ya sheria husika pamoja na kuondoa upungufu uliobainika katika utekelezaji wa masharti ya sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2023, kama ulivyowasilishwa unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

(1) Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442, *(The Electronic Transactions Act, Cap. 442)*.

(2) Sheria ya Taifa ya Leseni na Usajili wa Viwanda, Sura ya 46, *(The National Industries (Licensing and Registration) Act, Cap. 46)*.

(3) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, *(The Public Audit Act, Cap. 418)*.

(4) Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sheria Na. 10 ya Mwaka 2022. *(The Tanzania Investment Act, Act No. 10 of 2022)*.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tano. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442 ambapo kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya msamiati "*certificate*" uliotumika katika Sheria hiyo lakini haukuwa na tafsiri. Aidha, inapendekezwa kuongezwa tafsiri ya misamiati mipya "*root certification authority*" na "*subscriber*" ambayo imetumika kwenye vifungu vipya vya 35(A) na 35(B) vinavyopendekezwa kuongezwa. Lengo la marekebisho katika kifungu hiki ni kutoa ufafanuzi wa misamiati muhimu iliyotumika na inayopendekezwa kutumika kwenye Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 6 na 7 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha utaratibu wa kubainisha usahihi na usalama wa saini za kielektroniki kuainishwa katika kanuni. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya

Sheria hiyo yanayohusu usahihi na usalama wa saini za kielektroniki. Kifungu cha 34 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza majukumu ya mdhibiti wa huduma za mifumo ya kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, vifungu vipya vya 35(A) na 35(B) vinapendekezwa kuongezwa, ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya habari, mawasiliano na teknolojia ya kuteua taasisi miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo, ili kutekeleza majukumu ya uidhinishaji wa watumiaji wa mifumo. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha mfumo wa udhibiti wa utambuzi wa watumiaji wa mifumo ya kielektroniki na seva.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Taifa ya Leseni na Usajili wa Viwanda, Sura ya 46 ambapo Kifungu cha Pili kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha tafsiri ya misamiati mbalimbali kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika katika Sheria husika. Kifungu cha Tatu kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuboresha maelezo ya pembeni ili kuwianisha maelezo hayo na maudhui ya kifungu husika.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 10, 17, 18, 19, 20, 22, 23 na 25 vinapendekezwa kurekebishwa, na kifungu cha 15 kinapendekezwa kufutwa ili kuhamisha majukumu ya kiutendaji kutoka kwa Bodi kwenda kwa Msajili. Kwa mujibu wa marekebisho haya inapendekezwa kuwa Bodi itekeleze jukumu la kumsimamia Msajili na kumshauri Waziri kuhusiana na maendeleo ya sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuweka masharti yanayohusiana na uteuzi wa wajumbe na muundo wa Bodi. Aidha, kifungu hicho kinapendekeza kuongezwa kwa Jedwali. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa Sheria na kuwezesha masharti kuhusu vikao na taratibu nyingine za Bodi kufafanuliwa katika Jedwali.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 12 na 16 vinapendekezwa kufutwa kwa kuwa, majukumu ya ushauri yaliyokuwa yanatekelezwa na Kamati ya Ushauri ya Mkoa yanapendekezwa kuhamishiwa kwa Bodi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 13 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya. Lengo la marekebisho haya ni kuweka takwa kwa mtu anayekusudia kuanzisha kiwanda kuomba leseni kwa Msajili. Kifungu cha 14 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yanapendekezwa kujumuishwa katika kifungu cha 13.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yameainishwa kwenye Jedwali.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa, ili kuongeza adhabu kwa makosa yaliyoainishwa kwenye Sheria husika. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza utii wa sheria. Kifungu cha 29 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni kuhusu masharti ya vyeti vya usajili na leseni na uteuzi wa wakaguzi wa viwanda. Lengo la marekebisho haya ni kupanua wigo wa maeneo ambayo Waziri anaweza kuyatengenezea kanuni.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 ambapo Kifungu cha Tatu kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta tafsiri ya msamiati "*public authority*". Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utata unaoweza kujitokeza kutokana na uwepo wa tafsiri mbili tofauti kwa msamiati mmoja katika Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sheria Na. 10 ya Mwaka 2022 ambapo kifungu cha 19 kinapendezwa kurekebishwa, ili kutoa kinga kwa wawekezaji wote, hata wale ambao hawana vyeti vya vivutio.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 29(A) kinapendekezwa kuongezwa, ili kuweka masharti yanayohusiana na hadhi ya wawekezaji wa kigeni wanaowekeza nchini. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje wanaowekeza nchini.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 32(A) kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayohusiana na utatuzi wa migogoro inayoweza kujitokeza kati ya wawekezaji na taasisi za Serikali zinazosimamia masuala ya uwekezaji. Lengo la marekebisho haya ni kuweka bayana taratibu za utatuzi wa migogoro kati ya taasisi za Serikali na wawekezaji pamoja na kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya uwekezaji kutengeneza kanununi zitakazoainisha namna na taratibu za utatuzi wa migogoro ya wawekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha Maelezo ya Muswada, kwa heshima sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (Na. 5) WA MWAKA 2023 *(THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (No. 5) BILL,* 2023) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya

Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2023).

**Mheshimiwa Spika,** napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa misingi ya haki, malengo sahihi, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Dhamira yake njema, weledi na uzalendo wake tunauona dhahiri kupitia miswada inayowasilishwa na Serikali Bungeni na kwenye hatua ya ukamilishaji wa kazi hizo yeye akiwa sehemu ya Bunge. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** ninawapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** ninawashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vyema vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuishauri na kuisimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, (*ndc.*) na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano

wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Balozi Profesa Kennedy Godfrey Gastorn kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bw. Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mbunge wa Madaba) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mbunge wa Nkenge) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kusikiliza, kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali kupitia wadau wote waliohusika na sheria zinazopendekezwa kurekebishwa imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2023) unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Nne (4) zilizoainishwa katika Sehemu ya Pili hadi Sehemu ya Tano ya Muswada.

Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utekelezaji wa masharti ya sheria husika pamoja na kuondoa upungufu uliobainika katika utekelezaji wa masharti ya sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2023, kama ulivyowasilishwa unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria zifuatazo:

1. Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442, (The Electronic Transactions Act, Cap. 442);

2. Sheria ya Taifa ya Leseni na Usajili wa Viwanda, Sura ya 46, (The National Industries (Licensing and Registration) Act, Cap. 46);

3. Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, (The Public Audit Act, Cap. 418); na

4. Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sheria Na. 10 ya Mwaka 2022. (The Tanzania Investment Act, Act No. 10 of 2022).

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tano. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442 ambapo kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya msamiati "certificate" uliotumika katika Sheria hiyo lakini haukuwa na tafsiri. Aidha, inapendekezwa kuongezwa tafsiri ya misamiati mipya "Root Certification Authority" na "subscriber" ambayo imetumika kwenye vifungu vipya vya 35A na 35B vinavyopendekezwa kuongezwa. Lengo la marekebisho katika kifungu hiki ni kutoa ufafanuzi wa misamiati muhimu iliyotumika na inayopendekezwa kutumika kwenye Sheria hiyo.

Vifungu vya 6 na 7 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha utaratibu wa kubainisha usahihi na usalama wa saini za kielektroniki kuainishwa katika kanuni. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha

utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hiyo yanayohusu usahihi na usalama wa saini za kielektroniki.

Kifungu cha 34 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza majukumu ya mdhibiti wa huduma za mifumo ya kielektroniki.
Vifungu vipya vya 35A na 35B vinapendekezwa kuongezwa ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya habari, mawasiliano na teknolojia ya kuteua taasisi miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo ili kutekeleza majukumu ya uidhinishaji wa watumiaji wa mifumo. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha mfumo wa udhibiti wa utambuzi wa watumiaji wa mifumo ya kielektroniki na seva.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Taifa ya Leseni na Usajili wa Viwanda, Sura ya 46 ambapo kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha tafsiri ya misamiati mbalimbali kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika katika Sheria husika. Kifungu cha 3 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuboresha maelezo ya pembeni ili kuwianisha maelezo hayo na maudhui ya kifungu husika.

Vifungu vya 10, 17, 18, 19, 20, 22, 23 na 25 vinapendekezwa kurekebishwa na kifungu cha 15 kinapendekezwa kufutwa ili kuhamisha majukumu ya kiutendaji kutoka kwa Bodi kwenda kwa Msajili. Kwa mujibu wa marekebisho haya, inapendekezwa kuwa Bodi itekeleze jukumu la kumsimamia Msajili na kumshauri Waziri kuhusiana na maendeleo ya Sekta ya Viwanda.

Kifungu cha 11 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuweka masharti yanayohusiana na uteuzi wa wajumbe na muundo wa Bodi. Aidha, kifungu hicho kinapendekeza kuongezwa kwa Jedwali. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa Sheria na kuwezesha masharti kuhusu vikao na taratibu nyingine za Bodi kufafanuliwa katika Jedwali.

Vifungu vya 12 na 16 vinapendekezwa kufutwa kwa kuwa majukumu ya ushauri yaliyokuwa yanatekelezwa na Kamati ya Ushauri ya Mkoa yanapendekezwa kuhamishiwa kwa Bodi.

Kifungu cha 13 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya. Lengo la marekebisho haya ni kuweka takwa kwa mtu anayekusudia kuanzisha kiwanda kuomba leseni kwa Msajili. Kifungu cha 14 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yanapendekezwa kujumuishwa katika kifungu cha 13.

Kifungu cha 21 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yameainishwa kwenye Jedwali.

Kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu kwa makosa yaliyobainishwa kwenye Sheria husika. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza utii wa sheria. Kifungu cha 29 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni kuhusu masharti ya vyeti vya usajili na leseni na uteuzi wa wakaguzi wa viwanda. Lengo la marekebisho haya ni kupanua wigo wa maeneo ambayo Waziri anaweza kuyatengenezea kanuni.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 ambapo kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta tafsiri ya msamiati "public authority". Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utata unaoweza kujitokeza kutokana na uwepo wa tafsiri mbili tofauti kwa msamiati mmoja katika Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sheria Na. 10 ya Mwaka 2022 ambapo kifungu cha 19 kinapendezwa kurekebishwa ili kutoa kinga kwa wawekezaji wote hata wale ambao hawana vyeti vya vivutio.

Kifungu kipya cha 29A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayohusiana na hadhi ya wawekezaji wa kigeni wanaowekeza nchini. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje wanaowekeza nchini.

Kifungu kipya cha 32A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayohusiana na utatuzi wa migogoro inayoweza kujitokeza kati ya wawekezaji na taasisi za Serikali zinazosimamia masuala ya uwekezaji. Lengo la marekebisho haya ni kuweka bayana taratibu za utatuzi wa migogoro kati ya taasisi za Serikali na wawekezaji pamoja na kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya uwekezaji kutengeneza kanununi zitakazoainisha namna na taratibu za utatuzi wa migogoro ya wawekezaji nchini.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb.),
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
2 Februari, 2024

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja imeungwa mkono, ahsante sana.

Sasa tunaendelea. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa niaba yake anakuja kusoma Mheshimiwa Seif Gulamali. *(Makofi)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (Na. 5) Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Spika, Utangulizi. Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (Na. 5) Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Tatu, Kikao cha Kumi kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 10 Novemba, 2023. Kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1), ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulielekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati Ilivyotekeleza jukumu la uchambuzi wa muswada; katika kutekeleza jukumu hilo, kamati ilikutana na Serikali tarehe 5 Januari, 2024 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Jaji Eliezer Mbuki Feleshi, Mbunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kuhusu Maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya mikutano na kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearings)* kuanzia tarehe 6, tarehe 8 hadi tarehe 10 Januari, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mablimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele

ya Kamati kuasilisha maoni yao. Nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 19 Januari, 2024 Kamati ilikutana tena na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba, kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada, ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Muswada; Utangulizi. Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (Na. 5) Bill, 2023)* ukiwa umegawanyika katika Sehemu Tano; na unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Nne kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni kama zifuatazo: -

(a) Marekebisho ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki *(The Electronic Transaction Act, CAP. 442)*

(b) Marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Leseni na Usajili wa Viwanda, Sura ya 46 *(The National Industries Licensing and Registration Act, CAP. 46)*

(c) Marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 *(The Public Audit Act, CAP. 418)* na

(d) Marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania *(The Tanzania Investment Act (No. 10) of 2022)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu Masharti ya utangulizi. Inajumuisha Ibara Na. 1 inayohusu jina fupi na Ibara ya 2 inayoelezea marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazofanyiwa marekebisho na maudhui yake. Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu pamoja na maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria mbili kati ya sheria nne zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho, kama zilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki *(The Electronic Transaction Act, CAP. 442)*. Marekebisho haya yanafafanuliwa katika Ibara ya 3 – 8 ya Muswada. Kamati ilielezwa kuwa, marekebisho kwenye Sheria hii kwa ujumla wake yanalenga kuweka mfumo wezeshi wa kuimarisha usalama wa mawasiliano yanayohusiana na Miamala ya Kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, masuala yanayohusu usalama wa taarifa za miamala ya kielektroniki, ni nyeti na muhimu kwa Taifa letu ambayo ni sehemu ya dunia ya mtandao. Aidha, marekebisho pia yanatoa ufafanuzi wa msamiati unaotumika, uliotumika na unaopendekezwa kutumika kwenye sheria. Kwa muktdha huo, sheria inapendekeza kuweka utaratibu wa kubainisha usahihi na usalama wa *signs* za kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, pia muswada unapendekeza kuongeza majukumu ya mdhibiti wa huduma za uthibitishaji ili kuhakikisha usimamizi na udhibiri bora wa mifumo ya kielektroniki. Aidha, marekebisho yanayopendekezwa yatampa mamalaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Habari, Mawasiliano na

Teknolojia, kuteua taasisi miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo ili kutekeleza majukumu ya uidhinishaji wa watumiaji wa mifumo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania *(The Tanzania Investment Act No. 10 of 2022)*. Marekebisho haya yanafafanuliwa katika Ibara ya 26 – 29 ya Muswada. Kamati ilielezwa kuwa, marekebisho kwa ujumla yanalenga kuboresha tafsiri ya msamiati uliotumika kwenye sheria hii ili kuwalinda wawekezaji, kwa wale ambao hawana vyeti vya vivutio vinavyotolewa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, muswada unapendekeza kuweka masharti mapya yanayohusiana na hadhi ya wawekezaji wa kigeni wanowekeza nchini ili kuweka usawa kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje, wanaowekeza nchini.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa sehemu kubwa ya Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, isipokuwa kwenye marekebisho ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki *(The Electronic Transaction Act, CAP. 442)* na marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania *(The Tanzania Investment Act No. 10 of 2022)* ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki *(The Electronic Transaction Act, CAP. 442)*; Kamati ilielezwa kuwa, kwa sasa Mamlaka ya Uidhiniashaji wa Hati za Usalama wa Elektroniki itakuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*, ingawa upo uwezekano wa Mamlaka zingine kufanya hilo jukumu la uidhinishaji wa hati hizo. Kamati ilishauri kuondoa takwa la ulazima kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia, kuteua taasisi miongoni mwa taasisi zilizo

chini ya Wizara hiyo ili kutekeleza majukumu ya uidhinishaji wa watumiaji wa mifumo. Tunaipongeza Serikali kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania *(The Tanzania Investment Act No. 10 of 2022)*; katika Ibara ya 29 ya Muswada, Kamati ilipendekeza kifungu kinachoongezwa cha 29A, kinachozungumzia hadhi ya mwekezaji wa kigeni kwenye Sheria ya Uwekezaji, Kamati iliishauri Serikali kuiandika upya Ibara hiyo ili kuondoa dhana ya kuwa, wawekezaji wanafanya mambo yasiyofaa na kuweka usawa kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa sekta ya uwekezaji katika nchi, huchangiwa na uwepo wa sheria bora ambazo zinaweka mazingira rafiki ya uwekezaji, kwa wawekezaji wazawa na wa kigeni. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushuri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba majina ya Wajumbe wote wa Kamati yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndugu Onorious Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati, kwa utaratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Kamati kuhusu hoja, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho, kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya Kamati, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA. 5 WA MWAKA 2023 *[THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.5) BILL, 2023*]- KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

1.0 **UTANGULIZI**

1.1 **Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2023)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na tatu, kikao cha kumi kwenye Bunge la12, tarehe10 Novemba 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala,

Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 5 Januari, 2024 ili kupokea maelezo ya Mhe. Jaji Eliezer Mbuki Feleshi (Mb) Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mikutano wa Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearings*) kuanzia tarehe 6, tarehe 8 hadi tarehe 10 Januari, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya Wadau. Mnamo tarehe 19 Januari, 2024 Kamati ilikutana tena na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.5 wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2023]* ukiwa umegawanyika katika sehemu tano (5) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria nne (4) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

a) Marekebisho ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki (The Electronic Transactions Act (CAP 442);

b) Marekebisho ya Sheria ya Taifa ya leseni na usajili wa viwanda, Sura 46 (The National Industries (Licencing and Registration) Act (CAP. 46);

c) Marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 (The Public Audit Act, [CAP. 418]); na

d) Marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania. (The Tanzania Investment (Act No 10 of 2022).

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi, inayojumuisha **Ibara ya 1** inayohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoelezea marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika sheria mbalimbali.

### 2.2 Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria mbili kati ya sheria

nne zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

**2.2.1 Mheshimiwa Spika**, sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki (The Electronic Transactions Act (CAP 442).** Marekebisho hayo yanayofafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 8 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilielezwa kuwa Marekebisho kwenye Sheria hii kwa ujumla wake yanalenga kuweka mfumo wezeshi wa kuimarisha usalama wa mawasiliano yanayohusiana na miamala ya Kielektroniki. Ikumbukwe kuwa masuala yanayohusu usalama wa taarifa za miamala ya Kieletroniki ni nyeti na muhimu kwa Taifa letu ambalo ni sehemu ya dunia ya mtandao. Aidha, marekebisho pia yanatoa ufafanuzi wa misamiati iliyotumika na inayopendekezwa kutumika kwenye sheria.

**Mheshimiwa spika**, kwa muktadha huo, sheria inapendekeza kuweka utaratibu wa kubainisha usahihi na usalama wa saini za kielektroniki. Muswada pia, unapendekeza kuongeza majukumu ya mdhibiti wa huduma za uthibitishaji ili kuhakikisha usimamizi na udhibiti bora wa mifumo ya kielektroniki. Aidha, marekebisho yanapendekeza yatampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia kuteua taasisi miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo ili kutekeleza majukumu ya uidhinishaji wa watumiaji wa mifumo.

**2.2.2 Mheshimiwa Spika**, sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania. (The Tanzania Investment (Act No 10 of 2022))**. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 26 hadi Ibara ya 29 ya Muswada.
**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Marekebisho kwa ujumla yanalenga Kuboresha tafsiri za misaiati iliyotumika kwenye sheria hii, ili kuwalinda uwekezaji wa wawekezaji kwa wale ambao hawana vyeti vya vivutio vinavyotolewa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Aidha, Muswada unapendekeza kuweka masharti mapya

yanayohusiana na hadhi ya wawekezaji wa kigeni wanaowekeza nchini ili kuweka usawa kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje wanaowekeza nchini.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwenye **Marekebisho ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki (The Electronic Transactions Act (CAP 442)** na **Marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania (The Tanzania Investment Act No 10 of 2022)** ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

#### 3.1.1 Marekebisho ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki (The Electronic Transactions Act (CAP 442).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa kwa sasa mamlaka ya uidhinishaji wa hati za usalama wa kielektroniki itakuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ingawa upo uwezekano wa mamlaka zingine kufanya hilo jukumu la uidhinishaji wa hati hizo. Kamati ilishauri kuondoa takwa la ulazima kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia kuteua taasisi miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo ili kutekeleza majukumu ya uidhinishaji wa watumiaji wa mifumo. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.1.2 Marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, The Tanzania Investment (Act No 10 of 2022).

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 29 ya Muswada, Kamati ilipendekeza Kifungu kinachoongezwa cha 29A kinachozungumzia hadhi ya Mwekezaji wa Kigeni kwenye sheria ya Uwekezaji. Kamati iliishauri serikali kuiandika upya Ibara hiyo ili kuondoa dhana kuwa wawekezaji wanafanyiwa mambo yasiofaa na kuweka usawa kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje.

**Mheshimiwa Spika,** ukuaji wa sekta ya Uwekezaji katika nchi huchangiwa na uwepo wa Sheria bora ambazo zinaweka mazingira rafiki ya Uwekezaji kwa Wawekezaji wazawa na wa Kigeni. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb – **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe

10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb –Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 **Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**,baada ya maelezo hayo ya Kamati naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
2 Februari, 2024

**SPIKA:** Ahsante sana mwakilishi wa Mwenyekiti kwa wasilisho hilo linalohusu mawazo ya Kamati. Waheshimiwa Wabunge, sasa kama ulivyo utaratibu, nimeletewa majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia hoja hii. Baada ya Wabunge hao kumaliza mchango wao, mtoa hoja atakuja ahitimishe hoja yake, halafu tutaingia kwenye zoezi la kutunga sheria.

Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Muswada huu wa marekebisho ya sheria mbalimbali, mimi nitajikita kuchangia mabadiliko ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki ambao ni Sura 442.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya Miamala ya Kielektroni, kwa mara ya kwanza ilipitishwa mwaka 2015 na ina miaka tisa ikiwa kwenye *operation*. Sheria hii ya Miamala ya Kielektroniki inajumuisha miamala yote ambayo tunaifahamu, kama miamala ya kutumiana fedha kwa njia ya *M-PESA, TIGO PESA, Airtel Money,* Halopesa na kadhalika. Pia, miamala ya kutumiana fedha kwa njia za kibenki na kadhalika. Kwa hiyo, ni sheria ambayo inasimamia *transactions* ambazo ni muhimu na ni nyeti sana.

Mheshimiwa Spika, sasa, mabadiliko ya sheria hii ya miamala ya kielektroniki inakusudia kufanya marekebisho kwenye vifungu vinne. Kifungu cha 3, kifungu cha 6, kifungu cha 7 na kifungu cha 34. Hivi ndivyo Vifungu ambavyo sheria hii ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali katika eneo hili la Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, ndivyo vimeletwa kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, sasa wote tunafahamu, hakuna jambo ambalo ni nyeti na muhimu na ambalo linapaswa kuwa salama kama *transaction* ya hii miamala ya kieletroniki na hasa inayohusu *movements* za fedha. Unapofanya muamala ya elektroniki, kwa mfano *M-PESA*. Mimi ninapomtumia *M-PESA* mama yangu ambaye

yupo Jimboni, kinachokwenda siyo fedha. Kinachokwenda ni taarifa tu ya maandishi lakini hiyo taarifa ya maandishi yeye akiipata, ndiyo hiyo anakwenda kwa Wakala ndiyo inakuwa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ule usalama na uhakiki ni kitu muhimu sana katika *transactions* nyeti za kifedha kama hizi. Sasa, sasa hivi Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* inaboresha mfumo wake wa kudhibiti na kuhakikisha usalama katika hii Miamala ya Kielektroniki. Kwamba, unapotuma fedha kutoka chanzo kwenda kwa mtu anayefikiwa, basi kuwe na usalama 100%. Kusiwe na uwezekano wowote wa mtu hapa katikati kuweza ku-*tap* au ku-*hijack* au kuingilia mawasiliano na anaweza kubadilisha *transaction*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajua miamala ya fedha mtu akiongeza sifui moja sifuri mbili, basi *figure* imebadilika kabisa. Sasa, kwa namna ambavyo dunia inakwenda, haya mambo ya kiteknolojia na ya kielektroniki yanabadilika haraka sana. Kama *TCRA* wasipoboresha mfumo wao wa kudhibiti miamala ya kielektroniki, huko mbele ya safari inaweza kutokea hatari hiyo ya watu kuingilia hizi *transaction* za kifedha na kuweza kuathiri *transaction* hizo.

Mheshimiwa Spika, sasa, sheria hii inabadilisha vifungu hivi ili *TCRA* (Mamlaka ya Mawasiliano) ijenge huo mfumo sasa na imeshaanza kujenga. Inaendelea kuujenga na kuuboresha ili mfumo huo uweze kuhakikisha usalama asilimia 100 katika *transactions* za miamala za kielektroniki. Kwa hiyo, lengo la sheria hii ni kuhakikisha huyu mdhibiti wa miamala yote hii ya M-PESA, ya *TIGO PESA*, miamala ya kibenki, *movement* za fedha ambazo zinapita kwenye miamala ya kielektroniki, kusiwe na *possibility* yoyote ya mtu katikati, kutoka kwenye chanzo kwenda kwenye mtu wa mwisho hapa katikati kuweza ku-*hack* na kuweza kubadilisha *figure* au jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili kwa sasa halijatokea. Unaweza ukaliona ni jambo dogo au rahisi lakini bila kufanya maandalizi

mazuri ya uhakika kwenye mifumo yetu, linaweza kuleta hasara mbele ya safari. Ndiyo maana sasa hivi Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaboresha mifumo yake ya kudhibiti hizi *electronic transactions* na ndiyo maana imeleta mabadiliko katika hivi vifungu. Kifungu cha 3, cha 6, cha 7 na cha 34 cha Sheria iliyopo ya Miamala ya Kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, badiliko hili linakuja kwa sababu, hii sheria ilitungwa mwaka 2015. Sasa hivi inakaribia miaka tisa kumi. Kiteknolojia huu ni muda mrefu sana. Mambo yanabadilika kwa kasi sana. Kwa hiyo, msipojilinda na kujiweka sawa, mbele ya safari mnaweza mkakumbana na tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, ninawashauri Wabunge wenzangu, tuunge mkono mabadiliko ya hivi vifungu vinne vya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki ili Mamlaka ya Mawasiliano iweze kuboresha, kuendelea na kukamilisha uboreshaji wa mfumo wake wa udhibiti ili tusiwe katika hatari yoyote ya hii miamala ya kielektroniki kuweza kuwa *hacked* na watu ambao siyo waaminifu na kuweza kusababisha watu kuingia hasara. Unatuma fedha zinakwenda zinafika *figure* nyingine, kutokana na wajanja kuweza kuingilia katikati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lengo la Mamlaka ya Mawasiliano ni kuhakikisha usalama, usahihi na udhibiti ili hii miamala ya kifedha iweze kuwa salama na wananchi wetu waweze ku-*transact* salama. Kwa sababu, huko tunakokwenda sasa hivi, tunaenda kwenye *society* ambayo itakuwa haitumii fedha taslimu *(Cashless Society)*. Huko tunakokwenda mbele ya safari, karibu *transactions* zote zitakuwa ni kidijitali (kielektroniki). Ni vizuri tui-*support* mamlaka yetu inayosimamia mambo hayo kwa kuipa sheria ambazo zitaiwezesha kujenga mifumo ambayo itaweza kudhibiti hii miamala iweze kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono mabadiliko haya ili tuwe na usalama katika … ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii. Mimi nitachangia miswada miwili tu kati ya hii. Ule wa Sheria ya Uwekezaji, pamoja na ile Sheria ya Taifa ya Leseni na Usajili wa Viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaipongeza Serikali kwa kuleta marekebisho haya katika wakati huu. Marekebisho katika hizi sheria mbili nimeyasoma, yanapendekeza mambo ambayo kwa kweli yataboresha utendaji katika sekta hii na kupunguza zile hatari ambazo zingeweza kuwahatarisha walaji. Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan alijipambanua toka mwanzo sana kwamba anakusudia kuifungua nchi hii kiuchumi na maeneo mengine, ni dhahiri kwamba sheria pia zinapaswa kufunguka ziwe rafiki, kama ambavyo marekebisho haya yamekuja. Ziwe rafiki katika maana ya kufungua fursa, pia, ziwe rafiki katika maana ya kuwalinda walaji, tusijekupata wawekezaji ambao ni hatari kwa walaji.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 27 ya Muswada huu ambayo inarekebisha kifungu cha 10 cha hii Sheria ya Uwekezaji, inarekebisha kifungu cha 3 kwa kutoa tafsiri ya 'Mwekezaji wa Kigeni' ambayo Ibara hii inatafsiri Mwekezaji wa Kigeni kwamba, ikiwa ni mtu binafsi, basi awe ni mtu ambaye si raia na ikiwa ni kampuni, basi iwe ni kampuni ambayo imesajiliwa kwa sheria za nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa, hapa naomba mtoa hoja atakapokuja kufunga, atueleweshe kidogo kwa sababu, kwa mujibu wa kanuni zetu sasa hivi, kampuni ambayo imesajiliwa hapa Tanzania lakini zaidi ya 50% ya Hisa wamiliki wake wakiwa watu wa nje, inatafsiriwa kama kampuni ya nje. Hili limetulinda sana katika masuala yetu ya Haki ya Ardhi na kadhalika. Kwa hiyo, ninahisi kwamba, kanuni hizi na *practice* hii ya kuzichukulia hizi kampuni

kuwa ni za nje, inaweza ikakongana na hii tafsiri sasa inayokuja kwamba, kampuni ya nje ni ile tu ambayo imesajiliwa kwa mujibu wa sheria ambazo siyo za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili katika Sheria hii ya Uwekezaji ni marekebisho kuhusu kuongezwa kwa kifungu cha 29(a) ambacho kwa ujumla kinawapa hadhi sawa wawekezaji wa kigeni na wale wawekezaji wa ndani. Nakubali kwamba lazima tuwe na kifungu cha namna hii kwa sababu pia ni kuendana na mikataba ya kimataifa ambayo tumesaini.

Mheshimiwa Spika, mikataba ya kimataifa yote huwa inatekelezwa kwa mujibu wa mazingira na sheria zetu za hapa ndani. Sasa lipo tatizo kwamba wawekezaji wetu wa hapa ndani unaweza ukasema, sawa ni sawa sawa na wawekezaji wa kigeni, lakini wawekezaji wa nje wana fursa ya kuchukua hata mikopo nje ambayo ina riba ndogo sana ukilinganisha na mikopo yetu ya hapa. Kwa hiyo, ni vizuri basi kama tunataka kwenda kulingana na mifumo ya dunia na mikataba ya kimataifa, basi uwepo utaratibu wa kuwarahisishia wawekezaji wetu masharti hasa ya mikopo, wapate mikopo kwa namna ambazo ni rafiki na riba ziweze kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kuyachongea ma-*bank* lakini jana tumeona jinsi ambavyo yame-*post* faida kubwa ambazo wamepata, ambazo zimevunja rekodi. Ni vizuri pia hiyo hali ikaji-*reflect* kwenye kuwasaidia wawekezaji wetu wa ndani kwa kuwapunguzia riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ni muhimu sana kuwatengenezea wawekezaji wetu wa ndani mazingira ya kuweza kukopa nje. Hii ili waweze kukopa nje, ni lazima iendane na Serikali kuwa tayari kutoa *Government guarantee* kwa ajili ya wawekezaji wetu wanaokopa nje. Hili naamini linawezekana kwa sababu, ni sawa Serikali inaweza ikampa mwekezaji *guarantee* lakini wakawa na *counter guarantee* ya hapa hapa ndani kwetu, *local*, ama ikawa ni *insurance* au ni hizi

mali zetu zisizohamishika. La maana ninalosema ni kwamba, ili tuone faida ya marekebisho haya ambayo yanasema kwamba wawekezaji wa ndani na wa nje wawe na hadhi sawa, basi ni lazima wawekezaji wa ndani nao wawekewe mazingira rafiki ili ule uwanja wa mapambano uweze kuwa sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye kwa kifupi kabisa kwenye marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Leseni na Usajili wa Viwanda. Ibara ya 13 ya marekebisho haya ambayo yanarekebisha kifungu cha 10 inaunda bodi ambayo ndiyo itakayomsimamia msajili. Kwa kweli hili jambo ni lakupongeza sana, kwa sababu ninachokiamini mimi ni kwamba msajili ni mtaalamu. Yeye atakuwa anapokea maombi ya leseni, anayachuja kitaalamu, anasimamia vile viwanda kitaalamu. Sasa bodi pengine inaweza ikahusisha watu wengine kama akina sisi hapa ambao sio wanasayansi kwa sababu viwanda ni sayansi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napongeza sana mabadiliko haya ya muundo kwamba sasa msajili awe ndio Mtendaji Mkuu, asimamiwe na bodi. Pengine itatupunguzia matatizo mengi sana ya viwanda vya watu fulani tunaowafahamu tunayoyaona huko Mikocheni, ambapo unaingia tu uwani unakuta mtu ana kiwanda cha ajabu sana, unajiuliza hata alipataje leseni. Pengine utoaji leseni ulikuwa hauzingatii sana viwango vya kitaalamu na vya kisayansi na hiyo inaweza ikatibiwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, katika *schedule* kule kwenye nyongeza ambayo imetengenezwa chini ya kifungu cha 11 (4), bodi inaruhusiwa ku-*coopt,* yaani sijui nisemeje kwa Kiswahili vizuri, lakini ku-*coopt* wataalamu katika kufanya shughuli zake. Nadhani kifungu hiki ni cha muhimu sana na ikiwezekana bodi ipewe uwezo mkubwa wa kutumia wataalamu. Kwa sababu kama nilivyosema, viwanda ni sayansi. Nina hakika zitakuja kesi nyingi sana ambazo bodi inatakiwa kushughulikia ambazo ni za kiutaalamu wa hali ya juu sana. Kwa hiyo, ni vizuri bodi itakayoteuliwa itumie vizuri kifungu hiki kwa

sababu hakuna mtu ambaye ana ujuzi wa kila kitu, lazima tukubali kutumia wataalamu.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, kwa kweli nilishawishi Bunge lako Tukufu kwamba tupitishe Muswada huu kama sehemu ya kuunga mkono dhana ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ya kufungua nchi yetu kiuchumi na katika sekta nyingine zote, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mtoa hoja, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, uje uhitimishe hoja yako. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukushukuru sana wewe mwenyewe tena kwa kunipatia fursa hii. Pia nashukuru sana na niwashukuru sana wachangiaji ambao walipata fursa ya kushiriki kwa njia moja au nyingine kwenye Muswada huu. Nirejee tu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yote kwa sababu Muswada huu ulipowasilishwa mara ya kwanza kwenye Kamati ni kweli tulijipa fursa ya kuhakikisha kwamba wataalamu wanaohusika na maboresho makubwa ambayo maudhui yake yanawasilishwa kwenye Muswada huu unafika mbele ya Kamati na kujenga uelewa wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, kwa kuwasilisha maoni ya Kamati na maudhui yake, vile vile Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, kwa jinsi ambavyo amejaribu kuelezea kwa kina umuhimu wa maboresho makubwa yanayowasilishwa kupitia hii sehemu ya Sheria ya *Electronic Transaction Act*. Namshukuru Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo kwa yote ambayo amechangia.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Tadayo kwamba baada ya kupitia jedwali letu kuondoa kile kifungu cha 27, kwa sababu tumeki-*delete*, kwa hiyo, nafikiri hofu aliyokuwa nayo, sasa haipo. Pia kwa maana ya wawekezaji wetu wa ndani kulindwa au kuwekewa mazingira rafiki kwa wao pia kuweza kushiriki

kwa ukamilifu kwenye uwekezaji, ukiangalia kwenye jedwali letu la marekebisho kwenye kifungu cha 29A utaona kwenye ile ibara ndogo ya (3), kuna mambo ambayo yameandikwa pale kwamba bila kuathiri masharti yaliyowekwa kwenye kifungu kidogo cha kwanza, "hatua zozote ambazo zitafanywa kwa kuwapatia fursa hao wawekezaji kutoka nje (kwa mfano kwenye (b)) hazitaizuia Serikali kuchukua jitihada zozote za kuwawezesha wawekezaji wa ndani."

Mheshimiwa Spika, sasa hatua hizi zinachukuliwa katika ngazi mbalimbali. Kwa mfano, kwa kupitia kituo chetu cha uwekezaji *(TIC)*, wanapopata maombi ya wawekezaji wa nje, kabla ya kuwaelekeza kwenye maeneo mengine, mojawapo huwa ni kuangalia maeneo hayo kama kuna wawekezaji wa ndani ambao wanafanya, na kujenga hoja kwa kuwaelekeza maeneo mengine ambayo hayajaguswa.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo Mheshimiwa Tadayo, inaendana na kuhakikisha hawa wawekezaji wa ndani wananufaika vile vile na vile vivutio vyote ambavyo vimetolewa na hii sheria yetu ya uwekezaji. Kwa hiyo, hatua madhubuti kabisa ambayo imechukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita na Mheshimiwa Rais wetu kuhakikisha kwamba jitihada kubwa ambayo nchi yetu inazifanya kuvutia hawa wawekezaji wa ndani, ni kuweka mazingira ambayo ni rafiki na ndiyo maana hata mawanda ya marekebisho yaliyokuja kwenye Sheria ya Uwekezaji mojawapo ni kuhakikisha kwamba mifumo hata ya utatuzi wa migogoro inazidi kuwekwa katika namna ambayo itaepusha kuwepo kwa migogoro ya kiuwekezaji ambayo itaipatia Serikali hasara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kwa haya yote ambayo yameletwa kwa Sheria ya Uwekezaji, hata ile Sheria ya Viwanda kama ambavyo mnaona majukumu makubwa sasa ambavyo yamegawanywa kwa bodi na kwa msajili. Hii ikiwa ni sheria vile vile ya Muungano hii ya maendeleo ya viwanda, ni kuhakikisha kwamba nchi yetu inaenda na ule

Mpango wa Maendeleo pamoja na jitihada zote ambazo zimeshawekwa na nchi yetu kuhakikisha kwamba tunapiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hii Sheria ya *Electronic Transaction Act*, nafikiri ni hatua ya kujivunia kwa sababu wote tunajua na kama hata ilivyojitokeza kwenye mijadala ya sheria zilizotangulia leo asubuhi, niliona ule wasiwasi wa jinsi ambavyo *artificial intelligence* inaweza ikaingilia haki za watu wengine. Kwa hiyo, kwa maudhui yaliyoletwa hata kwenye marekebisho ya sheria hii, mkiangalia mojawapo inacholenga sasa ni kuondoa uwezekano wa kuwa na watu ambao hawajahakikiwa na mamlaka zinazostahili kuweza kuingilia mawasiliano ya watu. Pili, kuwa na udhibiti wa kutosha kupitia *TCRA*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru tena kwa mara nyingine na Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Tutaendelea na utaratibu wetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment [No.5] Bill, 2023)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21

Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29

**MWENYEKITI:** Serikali inabadilisha kifungu kilichopo kwenye muswada, wanaweka kingine, yaani wanaondoa kilichopo, wanaweka kingine ambacho kipo kwenye Jedwali la Marekebisho.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kifungu kimoja kufutwa Serikali inapendekeza marekebisho ya mpangilio *(renumbering)*.

*(Mabadiliko ya mpangilio wa Ibara yaliyopendekezwa na Serikali yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments [No.5] Bill of 2023)* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments [No.5] Bill of 2023)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa nitawahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbaliambali (Na.5) wa mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments [No.5] Bill, 2023)*.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbaliambali (Na.5) wa mwaka 2023 (The Written Laws Miscellaneous Amendments [No.5] Bill, 2023) uliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Zipatazo Nne kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria Hizo. (*A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in Order to Keep the Laws Updated with Some Challenges Observed in its Implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Hebu rudia hayo maelezo ya kiswahili hapo juu ama soma yote kwa pamoja *long tittle*.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Zipatazo Nne kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo Yamejitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti Katika Sheria Hizo. *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in Order to Keep the Laws Updated with Some Challenges Observed in Its Implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Zipatazo Nne kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu Ambayo Yamejitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti Katika Sheria hizo. (A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in Order to Keep the*

*Laws Updated with Some Challenges Observed in Its Implementation) Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu. Kusomwa kwa Muswada kwa mara ya tatu kunaashiria kwamba Bunge limemaliza kazi yake ya kutunga sheria hii. Kama ilivyo ada tutampelekea Mheshimiwa Rais ili naye afanye kwa sehemu yake kwa matakwa ya Katiba yalivyo.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. Baadhi ya mambo ambayo yameelezwa humu ni yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyasemea na mengine Serikali imekuwa ikiyapokea moja kwa moja kutoka kwa wadau mbalimbali wanaotumia ama wanaoguswa na sheria hizi. Kwa hiyo, nawapongeza sana kuleta Muswada huu. *(Makofi)*

Pia nawapongeza kwa ushirikiano mkubwa mlioutoa kwa Kamati, nimeona hapa mmeleta mapendekezo mbalimbali ya kubadilisha baadhi ya vifungu baada ya kushauriana na Kamati. Tunawashukuru sana Serikali kwa usikivu huo. *(Makofi)*

Nitumie fursa hii kuishukuru sana tena Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kazi nzuri waliyoifanya. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii, mmefanya kazi kubwa sana na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kadri kila mmoja alivyoshiriki, tunawashukuru sana. Kwa hioy, zoezi letu la kutunga sheria hii tumeshalikamilisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nina jambo dogo tu. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nafikiri kwa sababu tulishapitisha hapa Sheria ya Miswada kuwa inaletwa katika lugha ya Kiswahili ama Kiingereza, sheria zinazobadilishwa ambazo zipo kwenye lugha fulani pengine wakati wa mabadiliko ziletwe katika lugha ile ili iwe rahisi kuoanisha. Kwa sababu hapa nilikuwa naona ile sehemu ya ufunguzi inakuwa Kiingereza halafu maneno yenyewe

Kiswahili, halafu mabadiliko haya angalau mliyoyaleta mengi yanahusu wawekezaji. Sasa unawaza, kama tuliweka kwa Kiingereza na sasa tumeleka kwa Kiswahili, ni dhahiri kwamba mtalamizika kutafsiri kwa sababu ndiyo sheria tuliyoitunga inawataka hivyo.

Ni vizuri kama sheria ipo kwa Kiswahili, marekebisho tulete kwa Kiswahili iwe rahisi kufuatilia, na sheria iliyopo kwa Kiingereza basi marekebisho yake yaletwe kwa Kiingereza ili tuweze kufuatilia ile sheria iliyopo na hii Sheria inayobadilisha ili iwe rahisi. La sivyo na sisi wenyewe kidogo itatupa shida. Mimi mwenyewe bado nina changamoto, naendelea kujifunza utungaji wa sheria kwa Kiswahili siyo rahisi sana.

Kwa hiyo, tuendeee kuyatazama hayo ili sheria zetu tunavyozitunga, hata hii inayopitiwa mtu atakuwa anasoma Kiingereza, Kiswahili, Kiingereza Kiswahili. Kwa hiyo, ni vizuri kama sheria imetungwa kwa Kiingereza, basi mabadiliko yake yaje kwa Kiingereza halafu mtaenda kutafsiri Kiswahili na zile zilizotungwa Kiswahili mabadiliko yake yaje kwa Kiswahili halafu mtapeleka kwa Kiingereza, itaturahisishia kufuatilia kwa karibu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kuwashukuru tena sana kwa uvumilivu ambao mmeuonesha siku ya leo mpaka tumemaliza kazi zilizokuwa mbele yetu kwa ajili ya kutunga sheria hizi nne. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kujitoa kwenu kwa ajili ya kazi hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.02 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 5 Februari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*